# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Kumi Na Tisa – Tarehe 8 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kusimama.

Waheshimiwa Wabunge juzi, Jumamosi tarehe 06 Mei, 2017, Taifa letu lilipoteza jumla ya watu 36 kati yao 33 wakiwa ni wanafunzi wa shule ya msingi ya *Lucky Vincent Academy* ya Mjini Arusha. Ajali hiyo ilitokea Wilayani Karatu, Arusha baada ya basi walilokuwa wakisafiria watoto hao kutumbukia katika korongo.

Waheshimiwa Wabunge, huu ni msiba mkubwa sana kwa Taifa letu, inasikitisha sana. Kwa niaba yenu nilituma salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, lakini pia, tunawatakia pole wazazi wote walioguswa na msiba huu, wanajumuiya wa shule ya *Lucky Vincent* wote, Wana-Karatu, Wana-Arusha na Watanzania wote.

Waheshimiwa Wabunge, miili ya wanafunzi hao na wengine ambao wamefariki katika ajali hiyo itaagwa rasmi leo katika tukio litakalofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amri

Abeid, Mkoani Arusha. Natambua kwamba shughuli hiyo itakuwa na viongozi kadhaa wa Serikali wakiongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutoka vyama mbalimbali ambao tayari hivi sasa wako Mjini Arusha.

Na sisi kwa hapa Bungeni naomba tuungane nao kutoa pole nyingi kwa msiba huo na ushiriki wetu katika msiba huo mzito wa Taifa, iwe ni kwa kusimama kwa dakika moja kuwakumbuka watoto wetu na wenzetu na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu.

Waheshimiwa Wabunge naomba sasa tuendelee kusimama kwa dakika moja kwa kumbukumbuku hiyo.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walisimama Kimya kwa Dakika Moja kuwaombewa watu 36 waliopoteza maisha katika ajali ya gari Karatu wakiwemo wanafunzi 33, walimu wawili na dereva mmoja wa Shule ya Msingi ya Lucky Vincent Academy ya Mjini Arusha)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Kufuatia hili ambalo nimelizungumza hivi sasa, Wahshimiwa Wabunge, na kutokana na ushauri ambao nimeupata kutoka kambi zote mbili za Bunge hili; nimepata ushauri ambao kama mkinikubalia naomba sasa iwe ni uamuzi wetu.

Waheshimiwa Wabunge, pande zote wameshauri kwamba tukubali sisi Wabunge kutoa posho yetu ya siku moja kuipeleka kule ambako posho hiyo itagawiwa sawasawa kwa wafiwa wote moja kwa moja kwa wafiwa wote, hasa kwa wazazi na kadhalika, kwa maana ya ndugu wa marehemu moja kwa moja. Naomba tu niwaulize, mnaafiki jambo hilo Waheshimiwa Wabunge?

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nawashukuruni sana. Katibu! *(Makofi)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mheshimiwa Mbunge afuatae aliapa Kiapo cha Uaminifu:-

Mhe. Catherine Nyakao Ruge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Katibu, tunaendelea.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Swali la kwanza kwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, litaulizwa na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Rhoda!

Na. 155

## Upatikanaji wa Ajira kwa Vijana wa Katavi

**MHE. RHODA E. KUNCHELA** aliuliza:-

Ipo changamoto kubwa ya ukosefu wa ajira kwa vijana wa Mkoa wa Katavi. Na hii ni kutokana na miundombinu mibovu inayosababisha wawekezaji kushindwa kuwekeza.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kusaidia vijana hao wapate ajira na kuwa na mazingira ya kuwawezesha kujikwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali kusaidia vijana wa Katavi pamoja na maeneo mengine kupata ajira na kuwa na mazingira wezeshi ya kujikwamua kiuchumi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia masuala ya ukuzaji ajira katika mipango ya maendeleo, hususan kutambua na kubaini mahitaji ya nguvu kazi katika maeneo husika. Kutenga na kuendeleza maeneo ya uzalishaji wa biashara kwa vijana, kuwezesha nguvu kazi kuwa na ujuzi wa kujiajiri, kuwezesha upatikanaji wa mitaji na vitendea kazi kwa makundi ya vijana, kukuza soko la bidhaa na huduma za wajasiriamali hasa vijana.

Mheshimiwa Spika, pili, kutekeleza programu ya miaka mitano ya kukuza ujuzi inayolenga kuwawezesha vijana takribani 4,419,074 kupata ujuzi wa kuajiriwa au kujiajiri katika

sekta mbalimbali. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 vijana 1,469 wamepatiwa mafunzo ya ushonaji wa nguo kupitia viwanda vya *Mazava Fabrics* na *Took Garment.* Vijana 3,900 wametambuliwa na watapata mafunzo ya kurasimisha ujuzi wao kupitia *VETA.* Vijana 100 kati ya 1,001 wameanza mafunzo ya ujuzi kwa kutengeneza bidhaa za ngozi katika Chuo cha *DIT,* Mwanza.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuandaa na kuana kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Ajira kwa Vijana katika Sekta ya Kilimo *(National Strategy for Youth Involvement in Agriculture)* ambao unaweka mazingira wezeshi ya kuvutia vijana kujishughulisha na kilimo kwa kuwezesha upatikanaji wa ardhi, mitaji, pembejeo za kilimo, masoko, mafunzo ya ujuzi wa kilimo na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo itasaidia pia kushirikisha vijana wote wa Tanzania, wakiwemo vijana wa Katavi kupata mazingira wezeshi ya kujikwamua kiuchumi. Aidha, Serikali itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya barabara inayounganisha mikoa yote nchini ikiwemo Mkoa wa Katavi kwa lengo la kuchochea uwekezaji na kukuza fursa za ajira nchini.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mheshimiwa Rais kabla ya Mei Mosi alitoa kauli akiwa Hai kwamba anaondoa kero ndogo ndogo za ushuru ambazo wanalipishwa watu ambao wanafanya biashara ndogo ndogo, akina mama pamoja na vijana.

Swali langu ni kuwa kauli hii ya Rais ililenga kuondoa kero ya huu ushuru ndogo ndogo katika Halmashauri ya Hai peke yake au katika masoko yote Tanzania nzima likiwemo Soko la Buzogwe, soko kubwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Soko la Mpanda Hoteli na masoko madogo yote yaliyoko katika Mkoa wa Katavi? Kauli hii pia inawalenga watu wa Mkoa wa Katavi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nilitaka kufahamu, kumekuwa na wawekezaji ambao wamekuwa wakienda kuihadaa Serikali kuomba maeneo kwa ajili ya uwekezaji, ikiwepo katika Kata ya Kekese ambako kuna mwekezaji ambaye alichukua eneo zaidi ya eka 1,000 akiwahadaa wananchi kwamba anahitaji kuwapatia ajira. Lakini mpaka sasa shamba lile analitumia kwa manufaa yake binafsi, hakuna ajira zozote alizotengeneza katika hilo shamba lililopo katika Kata ya Kekese, Manispaa ya Mpanda. Nini tamko la Serikali kumuwajibisha mwekezaji huyu kwa sababu anatumia pesa za wananchi na watu wa Katavi, vijana pamoja na akina mama wanahangaika hawaelewi nini cha kufanya?

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa wananchi wakitoa ardhi halafu Waziri ndio awajibike kujibu, si itakuwa taabu kidogo! Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nilikuona! Majibu tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli suala la ushuru na tozo ndogo ndogo limekuwa kero ya muda mrefu kwa wakulima wa nchi hii na Rais alikwishatoa maelekezo kuanzia wakati wa kampeni na katika mikutano mbalimbali kwamba, Serikali iangalie namna ya kupunguza, kama si kuondoa kabisa shuru tozo na hizi ambazo zinashumbua wananchi na zitaondolewa sio kwahalmashauri moja moja kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Mheshimiwa avute subira ya siku chache sana zijazo hazizidi 13 atasikia kwa kiwango gani Serikali itafutilia mbali tozo na ushuru mwingi sana ambao unasumbua wananchi mbalimbali. Tunadhamiria kufanya hivyo na tuseme tu kwamba nina hakika kila mtu atafurahi jinsi tutakavyokuwa tumeshughulikia hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa upande wa mashamba ambayo wawekezaji mbalimbali wameyachukua kwa lengo la kuyaendeleza halafu hawayaendelezi uko utaratibu unaofanywa na Wizara yetu ya Kilimo ya Ardhi, mashamba

haya yanafuatiliwa na wale wote ambao hawatekelezi masharti yale yaliyo katika mikataba yao. Mashamba haya yako katika hatua mbalimbali, mengine yameshachukuliwa yamefutwa, mengine yanaendelea kufanyiwa utaratibu wa kuyafuta ili yarejeshwe kwa wananchi au mikononi mwa Serikali.

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tuendelee na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la Mheshimiwa Josephina Thabitha Chagula.

Na. 156

**Hitaji la Wodi ya Wagonjwa na Wazazi Hospitali ya Kharumwa**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Serikali ilipandisha hadhi Kituo cha Afya Kharumwa kuwa Hospitali ya Wilaya Nyang'hwale.

Je, ni lini Serikali itaongeza majengo kwa ajili ya wodi za wagonjwa na wodi za wazazi katika hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA SERIKALI ZA MIKOA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya ya Ngang'wale ilitengewa ruzuku ya maendeleo isiyokuwa na masharti *(LGDG)* kiasi cha 533,822,000 kwa ajili ya ujenzi wa miradi, ikiwemo sekta ya afya. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 186.6 zimeshapokelewa. Fedha hizo zinapaswa kutekeleza miradi ambayo ni kipaumbele cha halmshauri kilichowekwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imeongeza ruzuku ya maendeleo hadi shilingi bilioni 1.038 sawa na ongezeko la asilimia 95. Vipaumbele vya matumizi ya fedha hizo ikiwemo ujenzi wa wodi, vitapangwa na halmashauri zenyewe kwa kuzingatia fursa na vikwazo vilivyopo.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia moyo wananchi wa Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kharumwa kilipopandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale lakini bado hakijapata watumishi wa kutosha kulingana na hadhi hiyo ya Hospitali ya Wilaya. Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha pamoja na vifaa tiba vya kutosha katika Hospitali hiyo ya Wilaya ya Nyang'hwale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na msongamano mkubwa sana katika Hospitali zetu hizi za Rufaa kama vile Bugando na kwingine ukitaka kuonana na Daktari Bingwa; je, Serikali, haioni ni muda muwafaka sasa kuweza kupeleka Madaktari Bingwa wa watoto pamoja na akina mama katika hospitali zetu za Wilaya, ili kuondoa usumbufu huo usiokuwa wa lazima kwa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali mazuri sana tena mazito. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mazito ya Nyang'hwale.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ndiyo maana kwa haja ya Waheshimiwa Wabunge wa Geita hasa ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Omar na Mheshimiwa dada yangu Josephine, katika Kituo hiki cha Afya cha Kharumwa kwanza, jambo kubwa tutakalolifanya, licha ya zile bajeti ambazo wenyewe wamezitenga, hivi sasa tutaenda kufanya

ukarabati mkubwa wa kituo kile, tutajenga *theatre* ya kisasa. Lengo kubwa ni kwamba, wale Wasukuma wenzangu wa pale waweze kupata huduma nzuri. Kwa hiyo tutawekeza juhudi hii ya kutosha katika kile, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge naomba nikutoe hofu katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tunafahamu kwamba changamoto kubwa ni changamoto ya wataalam na bahati nzuri kama ninavyofahamu hata zoezi hili la uhakiki wa watumishi hewa kwenye maeneo mbalimbali tumepata ripoti kwamba idadi ya watumishi hasa katika sekta ya afya, imeathirika sana. Pamoja na watumishi hewa, lakini pia kuna suala zima la ku-*forge* vyeti. Sasa hivi Serikali iko katika harakati mbalimbali za kuwaajiri watumishi wapya. Naomba nikutoe hofu Mheshimiwa Josephine kwamba tutakapotoa ajira hizi mpya, ambazo si muda mrefu Wizara ya Utumishi watatoa maelekezo nini cha kufanya, tutaelekeza watumishi katika eneo letu hili la Nyang'hwale ili wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja hii nyingine ya msingi hasa suala zima la madaktari bingwa ni kweli na ndiyo maana leo hii, hasa magonjwa yale ya akinamama, wakati mwingine watu wengi wanatoka mikoani wanaenda Dar es Salaam kwa ajili ya kwenda kuwaona *gynecologists.* Na kwa sababu hii Serikali yetu inaangalia jinsi gani itafanya ili kuweka uwiano mzuri katika kada mbalimbali zitakazoajiriwa, lakini lazima kuelekeza hawa wataalam katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutapunguza hii changamoto ya wananchi ambao wengi wao kwenda muhimbili au kwenda sehemu nyingine yoyote ya mbali kwa kujisafirisha inakuwa kazi kubwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nasema hoja yako imekubaliwa, na katika hili Serikali tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba tunapeleka watalaam bingwa katika maeneo yetu haya.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Janet Mbene, swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mhehimiwa Spika**,** ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mazingira anayozungumzia Mheshimiwa Chagula hayana tofauti na mazingira mengi ya Wilaya zetu na mikoa yetu ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ileje ilibahatika kupata fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya ambayo imejengwa na sasa hivi imesimama karibu miaka miwili. Nataka kuomba kuuliza, je, Wizara ya TAMISEMI iko tayari kuimalizia hospitali hiyo kwa sababu ni hospitali kubwa na kwamba kama ingetumika vizuri ingesaidia kiasi kikubwa sana. Sasa hivi wagonjwa wetu wa-*referral* wanakwenda Malawi. Kwa sababu Mbeya ni mbali zaidi, wanakwenda Malawi kutibiwa sasa hii si sahihi. Mheshimiwa Waziri atuambie, je, itawezekana kututengea fedha bilioni 1.3 kwa ajili ya kumalizia hosptali ile?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wananchi wetu wanakwenda nchi jirani.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba tulichukulie jambo hilo kwa uzito wake na nakumbuka Mheshimiwa Mbunge hata wakati tunajadili mambo mbalimbali hasa katika jimbo lake la Ileje na hata kituo chake cha kimoja cha afya alikuwa akizungumzia suala zima la changamoto ya afya katika Halmashauri ya Ileje. Naomba nikuhakikishie kwamba tutahakikisha tunakamilisha hizo Hospitali za Wilaya ili kupunguza changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili liko maeneo mbalimbali, liko Mvomero, Kilolo na maeneo mengine hospitali zime-*stack.* Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge siweze kuthibitisha kwamba *by* kesho tutatoa fedha, tunachokifanya Serikali kwa sababu tulikuwa na mchakato mpana wa kuhakikisha tunakabati vituo vya afya vipatavyo 100 na zoezi hili la kukarabati vituo vya afya 100 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litaanza ndani ya mwezi huu au mwezi ujao.

Mheshimiwa Spika, vilevile tutapeleka maelekezo makubwa kwenye Hospitali za Wilaya ambazo hazijakamilika, na tukimaliza hili tutakuwa tumehakikisha kwamba jukumu la Serikali yetu katika kuwahudumia wananchi litakuwa limefika mahali pazuri.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishie kwamba kwanza katika zile fedha za *LGDG* ambazo mwanzo zilikuwa sasa hivi tutaelekeza na kuweka nguvu vya kutosha ili fedha zote zipatikane. Vilevile tutazisimamia vizuri ili tuhakikishe kwamba tunamaliza suala hili la miundombinu ili wananchi wetu waweze kupata afya bora.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itashikirikiana nawe katika jimbo lako kuhakikisha sekta ya afya inakwenda vizuri.

**SPIKA:** Wahemishiwa Wabunge tuendelee, kwa sababu ya muda. Swali na Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo kwa niaba yake Mbunge jirani Mheshimiwa J.J.

Na. 157

**Kituo cha Mabasi Ubungo**

**MHE. JOHN J. MNYIKA (k.n.y MHE. SAED A. KUBENEA)** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuhamisha Kituo cha Mabasi cha Ubungo na kukipeleka eneo la Mbezi katika Jimbo la Kibamba lakini mpaka sasa jambo hilo halijatelekezwa.

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani ktaika kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, mradi wa kuhamisha Kituo cha Mabasi unatarajiwa kutumia kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tayari Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* umeanzisha kampuni ya ubia ya *Mzizima Properties Limited* ambayo itahusikana usimamizi na uendeshaji wa shughuli za kituo za kila siku. Kazi inayoendelea ni kutafuta Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kuthibitisha usanifu wa mwisho wa kina wa mradi ili kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi cha Mbezi Luis zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 28.71 zitakazotolewa kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Jiji na LAPF. Gharama halisi zitajulikana baada ya usanifu wa kina *(detailed design)* utakapofanywa na Mtaalam Mshauri.

**MHE. JOHN J. MNYIKA.** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Inasikitisha majibu yanatoka ya namna hii, hili suala ni la tangu mwaka 2012 kilipovunjwa kituo cha mabasi cha Ubungo; na mwezi Oktoba, mwaka 2014 aliyekuwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alitamka kwamba kituo kitaanza kujengwa na akatoa mpaka muda mfupi wa kukamilika kwa kituo, lakini majibu mpaka sasa mwaka 2017 yanakuja namna hii.

Sasa swali, ni lini hasa hiki kituo kitakamilika ili kuondoa msongamano ulioko Kituo cha Ubungo ambacho kimeshavunjwa na kiko kwenye hali mbaya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kituo hiki kinajengwa pembeni ya barabara ya Morogoro, na siku chache zilizopita *TANROADS* wametoa *notice* kwa wananchi wote wanaoishi pembezoni ya barabara ya Morogoro mita 121 kutoka katikati

ya barabara kila upande. Kuweza ndani ya siku 28 kubomoa majengo yao. Ndani ya siku 28 mita 121 pande zote mbili za barabara kutoka katikati ya barabara. Sasa kwa kuangalia umbali ambao *TANROADS* umeutaja ni wazi ubomoaji huu utahusu kituo cha sasa cha mabasi ya kawaida ya Mbezi kilichopo. Vilevile kama umbali ni huu wa mita 121 kutoka katikati ya barabara hata hiki kituo kipya kitaguswa.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Serikali ama Waziri mwenyewe ama Wizara hii ya TAMISEMI ama Wizara ya Ujenzi ijibu; kwa sababu huu umbali utaingilia hiki kituo ni kwa nini Serikali isitengue hili Tangazo lilitolewa na *TANROADS* la siku 28 ili majadiliano kwanza yafanyike kuhusu huu upana wa barabara sababu ni upana mkubwa sana ambao hauko kwenye barabara yoyote Tanzania? Mita 121 pande zote mbili za barabara kutoka katikati, naomba majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** MheshimiwaMwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika kwanza umesema kwamba muda umepita sana, ni kweli. Tuelewe kwamba hata suala zima la kituo hiki ni kituo mkakati sana nadhani na wewe liko katika jimbo lako pale. Ni kituo mkakati ambacho ukiangalia sasa hivi hata hizi barabara za kwenda kasi zinaishia pale Mbezi Mwisho. Nashukuru sana tumepata ushauri wa kamati ya TAMISEMI, walipofika kukagua kile kituo wametoa mapendekezo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, hata suala hili la la *reserve* ya barabara waliliona na wakasema ikiwezekana sasa Jiji la Dar es Salaam na kushirikiana na *LAPF* lifanye mkakati ili kuhakikisha kwamba wenye zile nyumba za jirani wanalipwa fidia ili ni kuongeza kituo. Vilevile wameenda mbali zaidi kwa kusema kwamba kwa uzoefu uliokuwepo maeneo mbalimbali yanapojengwa vituo ili watu watu wakatishe inabidi kutengeneza madaraja ya juu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wakapendekeza hata ikiwezekana kujengwe *tunnel* kupitia katika kituo Mbezi cha zamani, kwa hiyo ilikuwa ni ushauri mbalimbali. Hata hivyo

jambo hili linaitaji fedha nyingi sana, na kuhusu suala la fedha tunafahamu, wasitani wa shilingi bilioni 28 si jambo dogo; ndiyo maana kuna kitu *negotiation* kilifanyika kati ya Jiji na wenzetu wa *LAPF* na jambo hili bahati nzuri tulivyokwenda *site* siku ile watu wote walikuwepo pale *site* ili kukubaliana nini kifanyike. Yote hii ni kwa sababu *LAPF* wameonekeana kwamba wameshafanya mambo mazuri ya mfano. Kwa mfano pale Msamvu wamejenga *stand* ya kisasa. *LAPF* wamekuwa *commited,* wamesema kwamba tunataka tutengeneze *stand* ambayo hapa Dar es Salaam itakuwa ni *stand* kubwa ambayo ita-*accommodate* magari mengi zaidi kwa ajili ya eneo lile.

Kwa hiyo suala la lini mradi utaanza naomba nikuhakikishe, kwa sababu *LAPF* walishakuwa *committed* katika utoaji wa fedha, kwa sababu Jiji halitoi fedha; isipokuwa wataingia katika ile *joint venture business* ambayo itafanyika vizuri na kwa bahati nzuri na wewe Mheshimiwa Mnyika utakuwa miongoni mwa wafaidika kwa sababu *stand* ile nawe itanufaisha kwenye mapato katika Jiji lako la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu uvunjaji, kwamba ikiwezekana tutoe tamko hapa ili suala hili lisitishwe. Mimi niseme kwamba Serikali imesikia hiyo *concern* yako basi kama Serikali itaangalia nini kifanyike kwa ajili ya maslahi mapana kwa ajili ya Dar es Salaam lakini pia kwa wakazi wa Tanzania. Hata hivyo tumependekeza kwamba wataalam wetu wa *detailed design* waangalie vya kutosha ili ikiwezekana zile barabara ziweze kusogea mpaka hapa Mbezi Luis Mwisho; kwa sababu hata tukijenga ile *stand* kubwa pale bila kuitanua ile barabara vya kutosha bado tutakuwa na changamoto kubwa sana kwa sababu magari yatazidi kufungana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mambo haya yote kama Serikali inayachukua kwa maslahi mapana kwa mustakabali wa nchini yetu ili kukuza uchumi wetu na wananchi waweze kusafiri vizuri.

**SPIKA:** Tunaendelea Wahemishiwa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora swali na Mheshimiwa Rashid Abdalla Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 158

**Ulipaji wa Watumishi katika Halmashuri ya Lushoto**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Halmashauri ya Lushoto ina mzigo mkubwa wa kulipa mishahara ya watumishi ambapo inatumia zaidi ya shilingi 28,000,000 kila mwezi kulipa mishahara ya watumishi ambao kimsingi mishahara yao ilipaswa kulipwa na Hazina kupitia Utumishi.

Je, ni lini Serikali itawatua wananchi wa Lushoto mzigo huu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri za Wilaya wapo watumishi wanaolipwa kutoka Serikali Kuu na wapo watumishi wanaolipwa kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmshauri husika *(own source).* Utaratibu huu ulianzishwa baada ya kuonekana kuwepo kwa mahitaji maalum yanayowasilishwa na waajiri kutaka kuwaajiri watumishi wa ziada tofauti na ukomo wa bajeti ya mishahara ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kuna jumla ya watumishi 116 ambao waliajiriwa katika utaratibu huo wa mapato ya Halmashauri (*own source)* kwa kuwa Halmashauri hiyo iliona inaweza

kumudu gharama za kuwalipa mishahara kutokana na vyanzo vyake vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote kuzingatia uwezo wao kabla ya kuamua kuajiri watumishi kwa kutumia vyao vyao vya mapato.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, swali ya nyongeza kama lipo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, yapo pamoja na majibu ya Serikali ambayo kimsingi hayajatatua tatizo lengo lilikuwa ni Serikali itutue huu mzigo. Kama utakumbuka ni kwamba mapato ya ndani yanatakiwa yaende kwenye makundi maalum ikiwepo wanawake na vijana zile asilimia 10. Sasa Halmashauri inapotumia pesa zote hizi kwa ajili ya kulipa watumishi ambao ni jukumu la Serikali, je, Serikali haioni kwamba hili linaendana na kinyume na dhana nzima ya utawala bora?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa uhitaji huu wa kutumia *own source* kulipa watumishi wa ndani bado unaonekana mahitaji yapo kwa sababu Serikali Kuu haiajiri na kwa sasa wakati wa zoezi zima hili la uhakiki wa vyeti Halmashauri ya Lushoto imepoteza zaidi ya watumishi 115. Serikali inatoa tamko gani la kufidia hili pengo ambalo wafanyakazi hawa wametoka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora majibu ya swali hilo muhimu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, pamoja kwamba anasema kwa upande mmoja alikuwa hajaridhika, nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia suala zima la ajira hizi zinazofanyika kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kusema yafuatayo; kama Serikali hatu-*entertain* sana ajira hizi kwa

kutumia mapato ya Halmashauri. Tunatambua kwamba mapato haya ya Halmashauri au *own source* yanatakiwa kwenda katika vipaumbele vingi na ndiyo maana tuaendelea kusisitiza ni vema Halmashauri zetu kupitia kwa waajiri ambalimbali na Maafisa Utumishi wahakikishe wanaweka mapendekezo yao na makisio yao ya Ikama ili kipindi ambapo tunaajiri basi waweze kupata mgao wa ajira kwa wakati sahihi bila kuathiri uwezo wao Halmashauri katika kulipa.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukipata changamoto nyingine, wako ambao walikuwa wakiajiri kupitia hizi *own source* lakini unakuta hawafuati taratibu. Nipende kuweka angalizo kupitia Bunge lako, mchakato wa ajira hizi za *own source* unatakiwa usitofautiane na mchakato wa ajira zingine kama zinazofanyika katika Serikali Kuu na kulipiwa na Serikali Kuu, lakini vilevile hata katika sifa na miundo ya kiutumishi inatakiwa pia isiwe c*ompromised*, sifa zile zile kwa mujibu wa miundo ya maendeleo ya kiutumishi. Kwa hiyo, nimeona niseme hayo kwanza kabla sijajibu swali lake kwa undani.

Mheshimiwa Spika, nipende kumtoa hofu Mheshimiwa Shangazi, wao walipoleta haya mahitaji walionekana wanauweza kulipa, lakini nimuhakikishie tu katika mwaka huu ujao wa fedha 2017/2018 kwa Halmashauri ya Lushoto tumewatengea ajira nafasi 252 ambapo kati ya hizo kwa kada za afya tumewatengea nafasi 54, kwa upande wa elimu nafasi 132 kilimo nafasi 10, mifugo nafasi tano na nafasi nyinginezo 51.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watumishi walioathirika katika zoezi la vyeti *fake,* kama nilivyosema katika siku nne zilizopita, tayari tumeshatenga nafasi 15,000 kwa ajili ya kuzibia zile nafasi 9,932 pamoja na nafasi zingine za ziada zaidi ya 5,000 katika maeneo mbali mbali yenye upungufu mkubwa na mahitaji.

**SPIKA**: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo na Makazi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

Na. 159

**Bomoa bomoa na migogoro ya Ardhi Jimbo la Tabora Mjini**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Jimbo la Tabora Mjini hususan katika Kata za Mpera, Malolo, Mbugani na Ng'ambo (Kidongo Chekundu) kuna migogoro ya muda mrefu ya ardhi na bomoa bomoa ya nyumba za wananchi.

Je, Serikali inafanya juhudi gani kuhakikisha inamaliza migogoro hiyo ya ardhi ambayo ni kero ya muda mrefu kwa wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Ardhi, Nyumba, Maendeleo na Makazi, Mheshimiwa Angeline Mabula.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA, MAENDELEO NA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na migogoro ya ardhi mingi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi katika Jimbo la Tabora Mjini hususani katika kata za Mpera, Malolo, Mbugani, Ng'ambo na Kidongo Chekundu. Migogoro mingi inahusiana na madai ya fidia, kuingiliana kwa mipaka, kutozingatiwa kwa taratibu za uendelezaji, uvamizi wa maeneo yaliyopangwa kupimwa na kumilikishwa na miliki pandikizi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na migogoro hiyo Serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya urasimishaji wa maeneo yote ambayo yalikuwa yamevamiwa na kujengwa kiholela ili kuweka

miundombinu ya huduma muhimu katika maeneo hayo. Vilevile Serikali imeimarisha ushirikishaji wa sekta binafsi katika kuanga na kupima viwanja kwa kushirikiana na wananchi ambapo makampuni binafsi ya upangaji na upimaji yaliyosajiliwa yameshaanza kufanya kazi ya kupanga na kupima katika maeneo ya Uledi, Kariakoo na Inala. Aidha, Mpango Kabambe wa Mji wa Tabora, *(Tabora Master Plan 2015 - 2035)* utatoa dira ya upangaji usimamizi na uendelezaji wa ardhi katika mji wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia imekuwa ikisisitiza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha uwepo wa fedha kwa ajili ya kulipia fidia kabla ya kufanya zoezi la uthamini wa mali kwa ajili ya utoaji wa ardhi ili kuzuia uwezekano wa kuibuka kwa migogoro ya ardhi inayohusiana na fidia. Aidha, wamiliki wa ardhi wamekuwa wakishirikiana na makampuni binafsi ya upangaji na upimaji katika hatua zote za upangaji na upimaji wa viwanja katika maeneo yao ili kuhakikisha kuwa maslahi ya pande zote yanalindwa.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongezana ninaomba kuiuliza Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba hii migogoro kweli ipo na ni ya muda mrefu, Jimbo la Tabora Mjini linazungukwa na kambi nyingi za Jeshi ambazo migogoro mingi inapelekea kuhatarisha amani miongoni mwa wanajeshi pamoja na raia. Ni lini sasa Serikali au Serikali ina mpango gani wa kuwakutanisha wanajeshi wahusika ili waweze kukaa na wananchi kuweza kutatua migogoro hiyo ya ardhi iliypo Tabora Mjini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali inafanya uhakiki mbalimbali kuanzia watumishi wa Serikali na mpaka leo tumeona wale wa vyeti, lakini ni lini Serikali itafanya uhakiki wa hawa Maafisa wa Ardhi ambao wanaingiza migogoro kwa makusudi kati ya wananchi pamoja na Serikali kwa kufanya mpango wa kugawa viwanja; kwa mfano kiwanja kimoja kutolewa zaidi ya mtu

mmoja *(double allocation).* Maafisa hao wapo na hawajafanyiwa uhakiki ili wachukuliwe hatua. Ni lini Serikali itafanya uhakiki wa hawa maafisa wanaoleta migogoro ili na wao wachukuliwe hatua?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA, MAENDELEO NA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu ni kweli alichokisema kwamba maeneo mengi ambayo yamezungukwa na Majeshi na wala si majeshi tu hata watu wengine wa kawaida, kumekuwa na migogoro baina ya wananchi na pande ya pili inayomiliki wakiwemo Jeshi. Kuhusu zoezi alilouliza, mimi nimwambie tu kwamba naomba wananchi wa Tabora wawe na subira kwa sababu tayari zoezi la kuhakiki maeneo ambayo yana migogoro na yale ambayo yanamilikiwa na Jeshi limeshaanza. Upande wa wenzetu Wizara ya Ulinzi wameshaunda kamati ambayo imeanza kupitia katika maeneo na mimi nikiri tu wazi na ni-*declare interest* kwamba hata kwenye Wilaya yangu pia kulikuwa na tatizo hilo lakini tayari Kamati ile imeanza kupita na wanafanya uhakiki wa mipaka.

Mheshimiwa Spika, na wanapofika katika maeneo yale wanahusisha uongozi wa eneo husika. Kwa hiyo, wakifika pale lazima uongozi wa Wilaya na uongozi wa Mitaa au Vijiji vinavyohusika watahusishwa ili kuweza kubaini ile mipaka iliyokuwepo toka mwanzo. Wenzetu Jeshi wameenda mbali zaidi, kwa yale maeneo ambayo watakuwa hawayahitaji baadae watasema nini cha kufanya katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na kuyarejesha pia kwa wananchi; lakini ni baada ya uhakiki kwasababu mengine yako *strategically* huwezi kuyaondoa leo na kuwapa wananchi. Kwa hiyo, uhakiki huo Mheshimiwa nikuhakikishie umeshaanza, unafanyika na Tabora watafika na tatizo litakuwa *solved*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amezungumzia suala la uhakiki wa maafisa ambao wanaingiza mgogoro kati ya

Serikali na wananchi. Mimi niseme tu kwamba katika ziara ambazo tunafanya mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri kila tunapopita tukikuta kuna tatizo hatua zinachukuliwa palepale. Ni juzi tu hapa alikuwa Lindi ambako tumekuta kuna mtu kamilikishwa eneo kubwa la wananchi zaidi ya ekari 4,000 lakini Mheshimiwa Waziri ame-*declare* pale pale kwamba ardhi ile irudi kwa wananchi na yule mtumishi amesimamishwa. Hata hivyo mimi pia nilipopita katika maeneo yale kuna wafanyakazi idara hiyo tumewatoa katika eneo lile na kuweza kutafuta wale wengine wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa upande wa Maafisa Ardhi wale ambao ni wateule ni jukumu la Halmashauri, tukiona kwamba huyu mtu hafanyi kazi yake vizuri ni lazima tumuondoe na tunaleta jina lingine kwa maana ya ku-*propose* ateuliwe kuwa Afisa Ardhi Mteule; kwa sababu wale nao wasipofanya kazi yao vizuri hawa wadogo wa chini wanaharibu kazi zaidi. Kwa hiyo, ni jukumu letu sote katika maeneo yetu kuona wasiofanya kazi vizuri wachukuliwe hatua kwa sababu mamlaka ya ajira yako pale pale katika maeneo yao, kwa maana ya Mkurugenzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mbunge wa Rombo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuna zoezi linaendelea katika mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Kata za Kitendeni, Tarakea, Reha na Nanjara katika Jimbo la Rombo. Nyumba za wananchi zinawekwa ‘X’ na wameamriwa kuzivunja. Sababu wanayopewa ni kwamba wanataka kuhakiki mpaka wa Kenya na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nyumba hizi na wananchi hawa wameishi katika maeneo hayo kabla hata ya uhuru. Sasa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, uko tayari kusimamisha zoezi hili ili wananchi wale wa Kikerelwa, Nayeme na maeneo mengine wapewe maelezo ya kutosha

kuhusu zoezi hilo na labda pengine uko tayari tuongozane wewe na mimi kwa ajili ya kwenda kuwapa hawa wananchi maelezo ya kuridhisha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo la kuongozana mpaka mpate ruhusa ya Spika. Mheshimiwa Naibu waziri majibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunilinda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli zoezi la uhakiki katika mipaka yetu linaendelea, lakini naomba tukumbuke kwamba usalama wa nchi yetu hii tusipouangalia sisi wenyewe tunaweza tukajikuta tunaiingiza nchi katika matatizo. Kwa sababu wananchi wanapokuwa wanaingiliana katika yale maeneo ndipo hapo hapo uharifu unakuwa ni mkubwa zaidi, huwezi kujua ni nani amefanya zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la kuhakiki mpaka tunakwenda sambamba na ile eneo ambalo ni *no man's land* lazima libaki wazi, lakini pia ile *buffer zone* inayotakiwa kuwepo pale lazima hatua zinazotakiwa zionekane kubaki. Kwa hiyo, lazima tu katika lile eneo pawe wazi ili kuweza kutambua na kuainisha mipaka ilivyo na ile *no man's land* imekaa namna gani. Na hili tatizo pia lipo hata upande wa Tunduma, Uganda na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niwaombe tu kamba tunapofanya zoezi hili kama kuna mtu ambaye amevunjiwa tofauti na utaratibu pengine hakustahili kuvunjiwa hilo ndilo tunaloweza tukalisikiliza. Kwa wale waliojenga kwenye maeneo ambayo hayaruhusiwi kujengwa yanatakiwa yabaki wazi zoezi litaendelea kwa sababu ya kuangalia usalama wa nchi yetu ili tuweze kuudhibiti uingiaji holela katika maeneo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimwa Mariam Kisangi, swali linalofuata kwa Wizara hiyo hiyo ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 160

**Serikali Kutoa Vibali vya Ujenzi wa Maghorofa Kando Kando ya Barabara Kuu**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Kumekuwa na ujenzi wa nyumba za ghorofa kando kando ya barabara kuu na Serikali ndiyo inatoa vibali vya ujenzi huu ambapo baada ya muda maghorofa hayo yanaweza kubomolewa na mwenye jengo kulipwa fidia.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuainisha maeneo yenye mipango ya maendeleo ili kuepuka gharama kubwa ya kulipa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MANDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na ujenzi wa nyumba za ghorofa na za kawaida kando kando ya barabara kuu na barabara nyingine. Kasi ya ujenzi wa nyumba hizo huchochewa na kuimarika kwa miundombinu hususan barabara za kiwango cha lami. Uimarishaji wa barabara za lami huvutia wawekezaji kujenga nyumba za biashara, vituo vya mafuta, mahoteli pamoja na makazi. Hali hii ni ya kawaida katika uendelezaji miji kwa kuwa uboreshaji miundombinu hususan barabara hupandisha thamani ya ardhi katika eneo husika na kuvutia ujenzi wa majengo ya ghorofa.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza uwezekano wa kubomoa au kulipa fidia maeneo yaliyoendelezwa kwa ujenzi wa nyumba za ghorofa, Serikali imejiwekea mikakati ifuatayo:-

(i) Kuanisha meneo yote ambayo yameiva kiundelezaji upya *(areas ripe for redevelopment)* ili kuoanisha matumizi ya sasa na ya baadaye.

(ii) Kupanga maeneo hayo ili uendelezaji wake uendane na thamani ya ardhi na kuboresha sura ya miji. Mipango kina ya uendelezaji maeneo haya ni kama vile Kariakoo, Kurasini, Temeke, Msasani, Oysterbay, Magomeni na Ilala.

(iii) Kwa upande wa miji mingine, upangaji wa maeneo haya unazingatiwa katika utayarishaji wa mipngo kabambe *(master plan)* ya miji husika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za ghorofa kando ya barabara kuu hauna budi kufuata taratibu za mipango miji, uhandisi, mazingira na masharti ambayo muendelezaji hupewa katika kibali chake cha ujenzi. Natoa rai kwa taasisi zenye mamlaka ya kutoa vibali vya ujenzi ambazo ni Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa pamoja na Majiji kuzingatia masharti ya uendelezaji wa miji ili kuzuia uwezekano wa kubomoa maghorofa na kulipa fidia.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna ujenzi mkubwa unaoendelea katika barabara za Morogoro, Kilwa, Bagamoyo na Pungu, lakini Serikali inatoa hati pamoja na vibali vya ujenzi kwa wananchi hawa wanaojenga pembezoni mwa barabara. Inapotokea wakati wa upanuzi wa barabara wananchi hawa wanaambiwa kwamba wamefuata barabara na hawastahili kulipwa fidia.

Je, kwa nini sasa Serikali wanatoa vibali kwa wananchi wanajenga mpaka wanamaliza nyumba hasa

nyumba ya ghorofa mpaka inaisha pasipo kutoa ushauri wa kitaalam kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi wanapenda maendeleo, wanajenga majumba makubwa ya ghorofa na nyumba za kawaida pembezoni mwa barabara lakini wanakosa kuelewa matumizi sahihi ya ardhi iliyopo. Je, Serikali wako tayari kutoa elimu kwenye kata, vijiji na mitaa ili kuwaeleza wananchi wetu waelewe matumizi bora ya ardhi kuingana na mipango ya maendeleo iliyopangwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza ameuliza juu ya utolewaji wa vibali katika maeneo ambayo pengine hayakustahili kupewa vibali hivyo na baadaye yanabomolewa. Naomba kupitia Bunge lako hili Tukufu nitoe wito kwa halmashauri zote; kwa sababu tuna imani kila halmashauri inazo ramani za mipango miji katika maeneo yao; na ujenzi wowote unaoendelea unaangalia ile Mipango miji yao au *Master Plan* ambazo zinakuwepo zinasema nini katika maeneo hayo. Hili limekuwa likifanyika maeneo mengi na Mwanza ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba, katika hili na ambalo tumekuwa tukilitolea maelekezo mara kwa mara. Pale ambapo uongozi wa Halmashauri husika utatoa kibali tofauti na matumizi ya eneo ambalo limetajwa au ambapo mtu kapewa kibali kwenda kujenga, halmashauri hiyo ijue itakuwa tayari kulipa fidia hasa kwa wale ambao waliohusika katika kupeleka vibali ambavyo vinakwenda kinyume na utaratibu kwa sababu tunazo ramani na *master plan* zetu. Kwa hiyo, niseme hili ni jukumu la kila Halmashauri kujiridhisha kwanza kabla ya kutoa vibali vya ujenzi kwenye maeneo. Tusingependa wananchi wapate hasara kwa kujenga halafu baadaye anabomolewa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amezungumzia kuhusu kutoa elimu sahihi kwa wananchi ili watambue. Niseme tu kwamba, sasa hivi tuna miji zaidi ya 13 ambayo inaandaa

mipango miji yake, *I mean* kwa maana ya kuwa na *master plan.* Kabla ya *master plan* ile kutekelezwa lazima kunakuwa na ushirikishwaji wa jamii, ukiangalia sasa hivi katika Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na maeneo mengine ambayo *master plan* zinaendelea ikiwemo na Musoma lazima kunakuwa na ushirikishwaji wa wananchi. Unapowashirikisha pale ndipo wanatakiwa na wao pia watoe mawazo yao ili kuweza kuona na watambue *master plan* ile inakwenda kujengeka namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme elimu itaendelea kutolewa. Wizara tunavyo vipindi maalum ambavyo mara kwa mara Maafisa wetu huwa wanakwenda wanatoa na hata tunapofanya ziara tunatoa, kwa hiyo hili litaendelea kufanyika. Vile vile tuziombe, halmashauri kwa sababu unapokwenda ku-*implement master plan* utekelezaji wake lazima jamii iliyopo pale itambue. Pale mtu anapojenga nyumba ya kawaida wakati kwenye *master plan* yako inaonesha ni ghorofa, gharama ile utaibeba wewe ambaye unatoa kibali kujenga eneo ambalo tayari una *Master Plan* na bado unakiuka taratibu.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Salma. Sasa hapa tuna Salma kadhaa sasa sijui tuwe tunatofautishaje; Salma wa CCM na Salma wa *CUF*. Sasa nilikuona Mheshimiwa Salma wa *CUF. (Makofi/Kicheko)*

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Sheria ya Fidia inasema kwamba watu walipwe ndani ya miezi sita, lakini katika Jiji la Dar es Salaam kwa sasa kuna uwekaji wa alama za X kwenye nyumba za wananchi usioeleweka na alama hizo zinawekwa hazina muda maalum hasa kwenye nyumba ambazo zipo pembezoni mwa barabara na maeneo mengine katika Jiji la Dar es Salaam. Unakuta alama ya X imewekwa miaka mitano, mitatu au sita; yule mwananchi haelewi hii alama ya X inakuwaje? Naomba niiulize Serikali, ni kwa nini alama ya X inapowekwa yule mtu asilipwe fidia ndani ya miezi sita awe ameshalipwa na kuondoka katika eneo lile? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni wazi Sheria ya Ardhi kifungu namba 13(2) na (3) kinaelezea mtu unapotaka kuchukua eneo fidia ilipwe ndani ya miezi sita na kama hukulipwa ndani ya miezi sita basi kuna hali halisi ya kuweza tena kuchaji gharama hiyo kulingana na *rate* iliyopo katika *financial institution* kwa kipindi hicho. Hata hivyo, hii imekuwa haifanyiki kutokana pengine na wachukua ardhi wenyewe kutokuwa tayari kufanya ile kazi kwa wakati. Hii tumeisemea na tumeipigia kelele na ndiyo maana kukaja na ile Sheria ya Uthamini ambayo tumeifanya hapa; ambayo inazungumzia suala la baada ya miaka miwili kama mtu hajaweza kulipa fidia ule uthamini uliofanyika mwanzoni wote unakuwa umefutika. Hii ilikuwa imefanyika hivyo mwanzoni kwa sababu ile sheria ilikuwa inaachia mtu anaweza akaenda miaka 10 mpaka 20 hajalipa.

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema baada ya kupitisha ile sheria hivi sasa ndani ya kipindi kilichotajwa lazima fidia ile ilipwe na hakuna kuchukua ardhi ya mtu kama hujalipa fidia, hili kila siku tunalirudia. Tunasema kuanzia sasa, kwa sababu wananchi wengi wameteseka katika masuala ya ulipaji fidia. Hakuna kuchukua ardhi ya mtu kama mwekezaji au yeyote anayechukua ardhi ile hajaweza kulipa fidia kwa gharama iliyopo katika soko baada ya kuwa imefanyiwa uthamini kwa kipindi hicho. Vinginevyo wananchi tunasema wasitoe maeneo yao kama hawajathibitishiwa katika kutoa eneo lile.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika hilo hilo, kuna shughuli zingine ambazo zinafanyika za kiserikali ambazo ukiing'ang'ania ile ardhi unakuwa umekwamisha mambo mengine. Sisi ndani ya Serikali tunajipanga vizuri kuona kwamba yale maeneo ambayo yanatumika kwa ajili ya manufaa ya umma tutayafanyia utaratibu wa haraka na mapema ili wananchi wale wasiweze kulalamika.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein, Mbunge wa Chambani.

Na. 161

## Ongezeko la Uwekezaji Katika Sekta ya Utalii Nchini

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la uwekezaji katika sekta ya utalii nchini:-

Je, Serikali imejipanga vipi ili kukabiliana na ongezeko hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na ongezeko la uwekezaji katika miundombinu na mahitaji mengine yanayochangia ukuaji wa sekta ya utalii nchini; ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hoteli za aina na madaraja mbalimbali, uimarishaji wa vyombo vya usafiri kuelekea ndani ya hifadhi na maeneo mengine yeye vivutio na uboreshaji wa vifaa mbalimbali vinavyotumika kuhudumia watalii; mambo ambayo kwa kiwango kikubwa hutekelezwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali, pamoja na mambo mengine, ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege uliokamilika na unaoendelea, ununuzi wa ndege mbili uliokamilika na zingine nne zinazotarajiwa kuja nchini katika siku za karibuni, zote ni jitihada zinazochangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa sekta ya utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yamewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii ambapo mwaka 2016 idadi hiyo iliongezeka kutoka jumla ya watalii 1,137,182 wa mwaka 2015 hadi jumla ya watalii 1,284,279 kwa mwaka 2016. Hii ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 12.9 na ongezeko

linaloendelea kuonekana katika hifadhi moja kwa moja ikiwa ni pamoja na eneo la Hifadhi la Ngorongoro na Hifadhi za Taifa zinazosimamiwa na *TANAPA.*

Mheshimiwa Spika, ili kufanya ongezeko hilo liwe na tija na endelevu Wizara yangu imejikita katika kusimamia ubora wa huduma na utoaji huduma, kutangaza zaidi vivutio hususan vivutio vipya na kusambaza shughuli za utalii nchi nzima hususan Ukanda wa Kusini *(The Southern Circuit)* ili kutimiza azma ya Serikali kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/2017 – 2020/ 2021 unaoainisha utanuaji wa uwigo wa mazao ya utalii *(diversification of tourism products)* kama mojawapo ya hatua muhimu za kuchukua *(key interventions)* katika kukuza utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa wito wa sekta binafsi kuongeza mbinu, bidii na mitaji kuunga mkono jitihada za Serikali katika kukuza utalii na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Mbunge wa Chambani, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu marefu ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza. Nchi yetu imejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii na ni dhahiri majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonesha nchi yetu inaona utalii ni mbuga na wanyama tu; na ni dhahiri kwamba ukanda wa bahari unawekwa katika majibu kuonekana tu kama nao upo. Ni dhahiri pia kwamba nchi yetu sasa hivi ina eneo kubwa la bahari kuanzia Tanga mpaka Mtwara lakini utalii wa baharini kama *diving, fishing* na *snorkeling* unakua kwa kasi na una fedha nyingi sana. Je, Serikali ina mpango gani madhubuti sasa wa kukuza utalii wa baharini katika nyanja hizo za *fishing, diving* na *snorkeling? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna matatizo makubwa ya upatikanaji wa umeme na maji katika maeneo ya uwekezaji na hili wawekezaji wanalalamika sana hata

huko ambako unasema kwamba *TANAPA* wanafanya kazi pamoja na Ngorongoro. Wawekezaji wanalalamika kwamba kuna urasimu mkubwa wa kupata vibali vya uchimbaji wa visima au kupeleka umeme kwa ajili ya kutumia katika hoteli zao. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kweli kabisa wa kuondoa urasimu na gharama kubwa kwa wawekezaji katika kupata huduma hizi muhimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa, swali sasa, ulisema majibu ya Naibu ni marefu na maswali yako sasa yamekuwa marefu zaidi.

Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama amesikia vizuri kwenye jibu langu la msingi nilipokuwa nazungumzia *diversification of tourism products* (utanuaji wa wigo wa vivutio vya utalii), kwa bahati mbaya kwenye swali la msingi alisikia Ngorongoro na Hifadhi za Taifa za *TANAPA* akasema ni wanyamapori tu peke yake, lakini ukweli ni kwamba pale Ngorongoro tuna kivutio kikubwa sana ambacho kina sifa kubwa duniani na sasa hivi ni mwelekeo wa watalii wengi sana kuja kuona chimbuko la binadamu duniani ambayo si wanyamapori, hilo ni suala tu la kihistoria.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu suala lake la kukuza utalii katika maeneo mengine, ametaja mfano mmoja tu wa eneo la fukwe za bahari. Huo ni mpango wa Serikali na tayari tumekwishafanya kazi ya awali ya kufanya tathmini ukanda mzima wa bahari kutoka Tanga mpaka Mtwara jumla ya kilometa 1,000 na tumebaini maeneo kadhaa ambayo yana umiliki wa aina mbalimbali, maeneo mengine yanamilikiwa na watu binafsi na watu kama hao. Kwa hiyo Serikali iko kwenye mpango wa kuweza kuangalia namna bora zaidi ya kuweza kuelekeza uwekezaji kwenye maeneo hayo ili tuweze kuweka vivutio hivyo vya *diving, fishing, snorkeling* na aina nyingine ya utalii wa bahari na utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la upatikanaji wa umeme na maji. Kwa ufupi kabisa, Serikali inayo taarifa juu ya changamoto hizo kwenye eneo hilo na tunachokifanya sasa hivi ni kushirikisha Serikali kwa ujumla wake; Wizara inayohusika na mambo ya umeme na ile inayohusika na maji, lakini pia kushirikisha wadau wa sekta binafsi wanaokwenda kuwekeza kwenye maeneo haya ya hifadhi ili tuweze kuona namna bora zaidi ya kurahisisha kuondoa urasimu, lakini pia kuwapunguzia walaji bei ya huduma hizi.

**SPIKA:** Waheshimiwa nawaona, Mheshimiwa James Mbatia nakuona lakini usiulize, nakuona Mheshimiwa Naghenjwa usiulize na wengine wote nawaona lakini msiulize, swali hili nampa Mbunge mpya, Mheshimiwa Catherine Ruge. Mheshimiwa Catherine Ruge, swali la nyongeza tafadhali, Mbunge mpya huyu.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi ya upendeleo. Napenda kuuliza swali la nyongeza kwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Mkoa wa Mara ni kati ya mikoa iliyobarikiwa kuwa na vivutio vya utalii vikubwa ikiwemo Mbuga ya Serengeti kwa upande wa mashariki *(Easten Corridor)* lakini pia upande wa magharibi *(Western Corridor).* Je, ni nini mkakati wa Serikali kwa upande wa *Western Corridor* ambao imeonekana umesahaulika lakini una vivutio vingi vya utalii *especially* kwenye Ziwa Victoria lakini pia kuna visiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Catherine, ahsante sana tunakushukuru, Waziri amekuelewa. *(Makofi)*

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Ina mpango gani wa kuendeleza utalii katika *corridor* ya Magharibi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza tafadhali. Mwanzo mgumu jamani. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, historia huwa inaandikwa namna hii na mimi nakuwa

ni Naibu Waziri wa kwanza kujibu swali la kwanza kutoka kwa Mbunge, Mheshimiwa Catherine Ruge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwanza Mheshimiwa Mbunge na napenda kumkaribisha katika jitihada hizi za kuweza kuwahudumia wananchi. Kuhusu swali lake la nyongeza kwa ufupi kabisa. *Western Corridor* anayoizungumzia ikiwemo eneo linalopakana na Serengeti upande ule wa magharibi, lakini pia Ziwa Victoria pamoja na visiwa vingine vyote ambavyo Mkoa wa Mara ni sehemu yake. Haya ni maeneo ambayo tayari Serikali imeshaweka mipango thabiti kabisa ya kuyaboresha.

Mheshimiwa Spika, hasa kuhusiana na Serengeti yako malango ya kuingia Serengeti yaliyozoeleka, mengi yanatokea upande wa Mkoa wa Arusha, lakini tumekwishaangalia hili na sasa kutokea Mkoa wa Mara, lakini pia kutokea Mkoa wa Shinyanga, tunakwenda kuboresha mageti ili tuweze kuwaruhusu watalii waingie kutoka kwenye kona zote zilizopakana na Serengeti ili kuweza kuruhusu idadi kubwa zaidi ya watalii kuingia katika maeneo haya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, tuko mbioni kuboresha maeneo hayo na wakati wowote ule tunamkaribisha Wizarani kuja kuleta maoni kwa ajili ya kuboresha utalii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu hayo mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tunaenda kwenye Wizara ya Maafande, swali linaulizwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka.

Na. 162

**Vijana Kufikiriwa Kujiunga na Jeshi la Ulinzi**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Kuna vijana zaidi ya 300 Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao wanajihusisha na kazi mbalimbali za kujitolea kama vile usafi, upandaji miti, kilimo cha mboga mboga na

matunda na wapo tayari kijiunga na Jeshi la Ulinzi kama wakifikiriwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwachukua vijana hao kujiunga na Jeshi hasa ikizingatiwa kuwa wana maadili mema na wameweza kujitolea?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa wa wananchi wa Tanzania kuajiriwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania unataka waombaji kuwa wamepitia Jeshi la Kujenga Taifa. Jeshi la Kujenga Taifa hutoa nafasi kwa kila mkoa. Vijana wanaopenda kujiunga na Jeshi hujadiliwa na kupitishwa na Kamati za Ulinzi na Usalama ngazi ya wilaya na mkoa husika. Kwa upande wa Zanzibar nafasi hizo hutolewa kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na idara maalum za SMZ. Ofisi hiyo ndiyo yenye wajibu wa kupeleka mgao huo katika mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana zaidi ya 300 wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao wanajihusisha na kazi mbalimbali za kujitolea na ambao wako tayari kujiunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, vijana hao wanashauriwa kuomba kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa mara nafasi zitakapotangazwa. Endapo watakuwa na sifa za kuajiriwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania naamini watapewa fursa hiyo kwa kadri ya nafasi zitakavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa

utaratibu aliousema ulishawahi kufanyika katika wilaya mbalimbali hapa nchini na baadaye tukaambiwa utaratibu huo umesitishwa, je, ni lini zoezi hilo litaanza tena ili vijana waweze kujiunga na Jeshi?

Mheshimiwa Spika, pili, ni nini kauli ya Serikali juu ya ajira ya Jeshi kwa vijana wenye maadili mema na uwezo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Tanzania kwa ujumla? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu niliousema haujasitishwa, bado utaratibu huu unatumika, kila mwaka tunachukua vijana kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia katika wilaya na mikoa yao. Kwa hiyo, utaratibu huo bado unatumika. Mwaka huu tumefanya zoezi hilo mwezi Desemba na tunategemea tutakapopata fedha baada ya bajeti basi awamu inayofuata utaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana anaowazungumzia Mheshimiwa Malembeka, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, ni kwamba tutakapotangaza tena kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, nitawaomba vijana hao waombe kupata nafasi za kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na ajira kwenda Jeshi la Wananchi zinapitia katika Jeshi la Kujenga Taifa. Si Jeshi la Wananchi peke yake, kwa sasa vyombo vyote vya ulinzi na usalama vimeamua kwa makusudi kwamba ajira zao zipitie JKT. Kwa hiyo Polisi, Magereza, Uhamiaji, Usalama wa Taifa, Jeshi lenyewe la Wananchi wa Tanzania wote wanachukua vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hiyo nitawaomba wajiunge huko ili hatimaye waweze kupata ajira hizo.

**SPIKA:** Waheshimiwa nawaona lakini ukiangalia saa yetu mtaona muda unakimbia na bado tuna maswali mawili, tuyatendee haki kwa siku ya leo. Hivyo, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la

Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula. Mheshimiwa Ntimizi, kwa niaba yake Mheshimiwa Maige.

Na.163

**Barabara ya Itigi – Nyahua – Tabora**

**MHE. ALMAS A. MAIGE (K.n.y. MHE. MUSA R. NTIMIZI)** aliuliza:-

Eneo la kilometa 89 la kipande cha Barabara ya Chaya – Nyahua katika Barabara ya Itigi – Chaya – Nyahua - Tabora bado halijaanzwa kutengenezwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kujenga kipande hicho kwa sababu kwa sasa hakipitiki kabisa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kipande hicho kinapitika wakati wote wakati mchakato wa ujenzi wa barabara hiyo ukiendelea?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Chaya hadi Nyahua yenye urefu wa kilometa 85.4 ni sehemu ya barabara kutoka Manyoni – Itigi – Chaya – Nyahua hadi Tabora yenye urefu wa kilometa 259.7. Zabuni za kumpata Mkandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara hii zilitangazwa tarehe 2, Februari, 2017 na ufunguzi ulifanyika tarehe 3, Aprili, 2017. Kwa sasa tathmini ya zabuni zilizopokelewa inaendelea. Mradi huu utagharamiwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka *Kuwait Fund.*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018, jumla ya shilingi bilioni 15.73625 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Chaya – Nyahua kilometa 85.4. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka wakati kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zikiendelea.

**SPIKA:** Ahsante kwa majibu Mheshimiwa Engineer Ngonyani, Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Barabara hii ambayo sasa hivi iko chini ya *plan* ya kujengwa kwa kiwango cha lami imekuwa na matatizo sehemu zile za Kizengi ambako madaraja yake ni mabovu na ikitokea dharura yoyote gari moja likazimikia barabarani magari mengine hayapiti. Je, katika kipindi hiki cha kungojea Serikali ina mpango gani wa kupanua Daraja lile la Kizengi?

Mheshimiwa Spika, pili, barabara hii inaunganisha Mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora lakini hatuoni uharaka wa kujenga barabara hii. Je, Serikali sasa inaweza kutuambia ni lini hasa ujenzi huu utaanza?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer* Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Almas Maige kwamba tulichokisema, ile sentensi ya mwisho, kwamba *TANROADS* itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili iweze kupitika majira yote hii ni pamoja na madaraja. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, matengenezo haya yanahusisha na madaraja.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, nimhakikishie kwamba taratibu tumezianza na tutaanza

kujenga hii barabara mara baada ya kukamilika *evaluation* na tukampata mkandarasi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tumalizie swali la mwisho la siku ya leo la Katiba ya Sheria, swali la Mheshimiwa Issa Mangungu.

Na.164

**Kuwaongezea Posho Wazee wa Mabaraza ya Mahakama**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Wazee wa Mabaraza katika Mahakama Kuu hasa Dar es Salaam husikiliza kesi zinazohusu mauaji na kulipwa sh. 5,000:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuwaongezea posho wazee hao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa Wazee wa Baraza katika Mahakama zetu na umuhimu wa kutoa posho kama motisha. Kutokana na umuhimu huo, Serikali ingetamani sana posho za wazee hao ziongezeke ili kuendana na hali ya uchumi, lakini kwa bahati mbaya posho hizo hutokana na bajeti ya matumizi mengineyo *(other charges)* ambazo hutengwa na Serikali kwa kila fungu.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Mahakama ya Tanzania ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.27 na mwaka 2017/2018, Mahakama imetenga shilingi bilioni 1.85 kwa ajili ya malipo ya posho ya wazee wa Baraza. Fedha kwa ajili ya Wazee wa Baraza ni fedha zinazotengwa katika

eneo la matumizi ya kawaida, hivyo Serikali kupitia Mahakama itaendelea kutenga au kuongeza posho kwa malipo mbalimbali zikiwemo posho kwa ajili ya Wazee wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala kwamba Wazee wa Mahakama wataongezewa posho zao kwa kadri bajeti itakavyokuwa inapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama Serikali inatenga bajeti, je, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba Wazee wa Baraza wanakopwa na hawalipwi kwa wakati posho zao na wengine mpaka wanafikia kukutwa na umauti wakiwa wanadai pesa nyingi sana idara ya mahakama, je, hilo analitambua?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kwa posho ya sh. 5,000 na uzito wa kesi wanazoamua wazee hawa hamuoni kwamba Serikali yenyewe inachochea vitendo viovu vya rushwa na mambo mengine katika mahakama zetu katika kutoa maamuzi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Profesa Paramagamba Kabudi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli yapo malimbikizo ya posho ya Wazee wa Baraza na mpaka sasa malimbikizo hayo ni sh. 335,479,000; na tunatarajia kwa fedha ambayo imetengwa mwaka huu kuweza kulipa malimbikizo hayo ya fedha hizo wanazodai Wazee Wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, pia tunatambua kabisa kwamba kiwango cha sh. 5,000 kwa mazingira ya leo ni kiasi kidogo ndiyo maana Serikali na Mahakama inafanya jitihada ya kuona uwezekano wa kuongeza posho hiyo, sio tu kwa

Wazee wa Baraza wa Dar es Salaam bali Wazee wa Baraza wa Mahakama zote nchini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa maswali umepita na ninyi wenyewe mnaona saa yetu. Nawashukuru sana kwa ushirikiano, wale ambao hamjapata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza ni kwa sababu ya muda wetu tu kuwa mdogo sana.

Wageni waliopo leo ni wageni 21 wa Mheshimiwa Catherine Ruge wakiongozwa na familia yake. Kwanza wale 21 naomba wasimame, wageni wa Mheshimiwa Catherine Ruge karibuni sana. Tumempokea Mheshimiwa Catherine, amefika salama na wenyewe mmeshuhudia tayari ameshakula kiapo hapa, karibuni sana na ahsanteni, mnaweza kukaa. *(Makofi)*

Kipekee niwatambulishe baba yake mzazi, Mzee William Ruge, naomba usimame, ahsante sana. Yuko *Gallery* ya Spika pale. Mama yake mzazi, Bi. Nchuta Ruge, ahsante mama. Mtoto wake, Magesa Robert. Ahsante sana mwanetu. Pia yupo dada, Eva Ruge. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Ningependa tu kuwakaribisha wageni wengine wote mliopo, mliokuja kujiunga nasi siku ya leo karibuni sana hapa Bungeni. Sasa tunaendelea na shughuli zetu, Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, naomba Mheshimiwa Waziri asonge mahali pake halafu…

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Miongozo tutachukua kesho. Halafu tunaendelea na uchangiaji sasa. Tunayo orodha naomba wajiandae, upande wa Upinzani ajiandae Saed Kubenea ambaye naambiwa hayupo eehh? Joseph Haule na Ole Meiseyeki kwa kuanzia. Upande wa CUF hakuna mchangiaji kwa leo...

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, majina tumepeleka jamani.

**SPIKA:** Ndiyo napewa karatasi sasa.

Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mheshimiwa Maulid Mtulia kwa kuanzia, lakini pia CCM Mheshimiwa Costantine Kanyasu, John Kadutu, Taska Mbogo wajiandae. Sasa nianze na Mheshimiwa Joseph Haule atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii nyeti iliyopo mbele yetu. Kabla ya kuanza niwape pole sana Watanzania wenzangu wa Jiji la Arusha na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huu mkubwa. Wananchi wa Mikumi tupo pamoja nanyi na tunaendelea kuwaombea marehemu walale mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia na-*declare interest* mimi ni Mwanamuziki, ni mwanamuziki bora kabisa wa *hip hop* Afrika Mashariki na kati na kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa hiyo hii Wizara inanihusu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia ya nchi yetu inaonesha tangu waasisi wa nchi hii walipokuwa wakifanya harakati kadha wa kadha walikuwa wakitumia sana sanaa. Nakumbuka Mwalimu Nyerere alikuwa akatumia wasanii

mbalimbali akina Mzee Mwinamila, akina Mzee Moris Nyunyisa ambao mpaka leo midundo yao inatumika kwenye taarifa za habari huko *TBC* wakati anafanya harakati za ku-*promote* vijiji vya ujamaa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia akina Mzee Mkapa walikuwa wakitumia sana wanamuziki wa mashairi kama akina Mzee Tambalizeni na watu wengine kama hao. Inaonesha ni jinsi gani ambavyo sanaa ni kitu muhimu na ni nyenzo muhimu sana katika Taifa kuonesha utamaduni, kuonesha mila lakini pia kufikisha ujumbe kadha wa kadha. Tunajua kwamba sanaa inatumia sana mafundisho lakini pia inakanya, inaonya na inasifia inapobidi; lakini kwa sasa kwa siku za usoni imeonekana wasanii kadha wa kadha wameonekana kuwa wakibanwa kutoa yale mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamependa kuwa wakisifiwa tu na wasanii wanapotoa mawazo mbadala wamekuwa wakipata rabsha kama ilivyotokea kwa msanii Roma ambaye ametekwa na akaja kuachiwa katika mazingira ya kutatanisha, lakini pia Msanii Ney wa Mitego ambaye alishikwa na baadaye akaja kutolewa kwa msamaha wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inawapa hofu sana wasanii kuweza kutoa kile walichokuwa wanakifikiria kwa sababu tunaamini msanii yupo huru na anatakiwa kutoa mawazo huru katika kulisaidia Taifa letu. Hata sisi tulipokuwa tukifanya muziki tulikuwa tunaimba nyimbo kama 'Ndiyo Mzee", "Siyo Mzee" na vitu vingine wengi mnavijua, Mheshimiwa Waziri ulisema wewe ni shabiki wangu mkubwa, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba mlikuwa mnajua jinsi ambavyo tumetumia sanaa hii kufundisha, kukanya, kuonya na kuburudisha pia.

Mheshimiwa Spika, wasanii wa Tanzania wamekuwa kwenye mazingira magumu sana na wamekuwa kwenye umasikini mkubwa. Mara nyingi tumekuwa tukiwatumia wasanii katika kampeni mbalimbali; tumekuwa tukiwatumia katika kampeni za malaria na hata katika chaguzi zilizopita

mmeona jinsi wasanii walivyokuwa wakitumika na baadaye mmewatumia kama Makarai na kuyaweka uvunguni.

Mheshimiwa Spika, tunajua Makarai yanatumika kwenye kujenga maghorofa na vitu vingine kama hivyo lakini tayari nyumba ikishakamilika yanawekwa uvunguni hayatakiwi hata kuonekana kwa wageni. Wasanii wa Tanzania wamekuwa wakitumika kwa *style* hiyo na wengi wamekuwa wakiwa maskini sana na hali yao ya uchumi imekuwa ngumu kwa sababu wamekuwa hawathaminiwi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa nikipiga kelele na kupaza sauti ya wasanii kwa sababu nataka niwaambie, katika nchi zilizoendelea kama Marekani, Uingereza Taifa lao linapata mapato makubwa sana kupitia sanaa zao. Takwimu iliyofanywa hapa Tanzania na *Rulu Art Promoters* inaonesha kwamba muziki peke yake unachangia takribani asilimia moja na zaidi ya pato la Taifa la Tanzania. Kwa hiyo, tunaona kabisa muziki umekuwa katika hali mbaya lakini bado inachangia asilimia moja. Naamini Wizara ikitumia umakini na ikijaribu kuwekeza zaidi katika Wizara hii, wasanii wa Tanzania wataweza kuchangia pato kubwa sana katika Taifa. Pia imesaidia sana kwenye kutoa ajira, wasanii wamejiajiri na kuajiri vijana wengi zaidi katika sekta hii ya sanaa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali ilitenga pesa kidogo sana ambayo ni bilioni tatu tu na katika hali ya kustaajabisha ni bilioni 1.19 ambayo ilikwenda kwenye nyanja hii na sasa hivi tunaweza tukaona katika bajeti hii imetengwa pesa ndogo ambayo kiukweli kabisa tunaona kama utani shilingi bilioni sita kwa sekta nzima ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kama kweli tuko makini kwenye kusaidia sanaa ya Tanzania ambayo imekuwa ikitoa ajira kubwa sana kwa wasanii na vijana wa Kitanzania, ilitakiwa tuweke pesa nyingi na hiyo pesa iweze kufika kwenye maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na malalamiko sana ya wasanii mfano wa filamu. Wasanii wa filamu wameandamana juzi wakiwa wanapaza sauti zao wakiwa wanataka haki zao za msingi. Hata hivyo niwaulize tu wasanii wenzangu wa filamu, huyu Bashite ameonekana kuwa na matatizo mengi na vyombo vya habari, amekuwa na matatizo mengi na Watanzania wengi wameonekana ambao wameonekana kuwa wanampinga, inawezaje mkamuweka akawa *front line* katika kutetea haki zenu za msingi? Tunaamini *movement y*oyote ambayo inatakiwa ifanyike kwenye kutetea haki inahitaji muungano wa watu wengi.

Mheshimiwa Spika, iwapo mngetaka kufanikiwa kwenye hili jambo mngemtumia kama Waziri wa habari kama alivyofanya *press conference* yake na Roma, tuliona vyombo vyote vikionesha mshikamano na umoja wao lakini sasa hivi tumeona mnamtumia Bashite ambaye anataka kujiosha kupitia ninyi na matokeo yake sasa Watanzania hawajawaelewa na ninyi wenyewe mmemeguka kwa sababu amekuwa na matatizo mengi na watu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu, sanaa ya filamu ya Tanzana inatoa ajira na sisi tuko hapa kwa ajili ya kuitetea na tunajua kwamba mna shida nyingi. Kwa mfano mdogo tu; kabla ya kufanya filamu, inabidi utoe shilimgi 500,000 kwenye Bodi ya Filamu kwa sababu tu ya kupeleka *script* yako, lakini ukishatoa *script* yako inabidi utoe tena shilingi 300,000= kwa ajili ya kupewa kibali cha ku-shoot. Ukishamaliza kutoa shilingi 300,000 na ukisha-shoot unapeleka shilingi 1,000 kukagua kila dakika ambayo unakuwa umeifanyia ile filamu. Ukitoa hiyo unakuja kupeleka tena unafunguliwa *file* pale *COSOTA,* unalipa zaidi ya shilingi 40,000. Baada ya hapo unapeleka *TRA* wanakupa *sticker* ambayo ni shilingi nane ndani, shilingi nane nje, jumla shilingi 16 kwa kila *copy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukimaliza hapo unaenda tena ku-*negotiate* na yule *distributor* ambaye ni Mhindi na ukishakubaliana naye kwa bei ambayo mliyokubaliana,

anakata asilimia 30 kwa ajili ya kupeleka kwenye kodi ya Tanzania. Unaweza ukaona jinsi ambavyo wasanii wa filamu wanaumia. Hata hivyo *strategy* waliyoitumia kwenye kutetea haki zao, wametumia mlango mwingine wa kutokea badala ya kutafuta *strategy* ambayo wangepata *support* yote. Kwa hiyo, nimwombe Waziri huu ni muda sasa wa kukaa chini na wasanii kuunganisha nguvu zote, tunahitaji Waziri wa Mambo ya Ndani, tunahitaji *COSOTA*, tunahitaji BASATA na Waziri wa Habari na Michezo tuweze kukaa chini na wasanii tuweze kujua shida zao ambazo zinawasumbua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la hati miliki; katika hii Sheria ya Hati Miliki namba Saba ya mwaka 1999 imepitwa sana na wakati. Wasanii wanaibiwa sana kazi zao, *piracy i*mekuwa kubwa lakini wezi wanaokamatwa na kazi hizo hamna adhabu kali ambayo wanapata. Tumeona kwamba kuna mtu alikamatwa na *container* zaidi ya bilioni sita zilikuwa zimetumika lakini baadaye anakuja kupigwa *fine* ya milioni tano. Mnaweza mkaona kwamba huu ni mzaha na inakatisha sana tamaa ya wasanii wa Tanzania katika hali kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi msanii Diamond alikuwa analalamika, *TRA* wamempelekea kodi ya milioni mia nne. Unaweza ukajiuliza kwamba adaiwa milioni mia nne kwa kiasi gani alichoingiza? *Downloads* ambazo inafanyika, mnaweza mkaona kwamba sasa hivi wasanii wanabawanwa, *TRA* wanatamani kuvuna kutoka kwa wasanii kitu ambacho bado hawajakipandikiza. Tumekuwa na ule msemo kama wa zamani kwamba shamba likiwa na bangi ni lako lakini likiwa na dhahabu ni la Serikali. Tunataka kuchuma kitu ambacho hatujakipanda. Ndiyo maana nasema, inabidi Serikali sasa ianze kuweka na kuwekeza kutoka kwenye shule za msingi mpaka Chuo Kikuu tuanze kuwajenga wasanii.

Mheshimiwa Spika, hata juzi, msanii Darasa alienda Arusha, *TRA* wakavamia *show* yake, wakasema kwamba haya mapato inabidi tugawane asilimia 18 yaani wameibuka tu *from nowhere.* Darasa ameenda Arusha kwa gharama

zake, ameenda kufanya matangazo, amelipa Ukumbi, wameenda wamefunga mageti saa 12 wanamwambia lazima tukate asilimia 18 pale Arusha, matokeo yake wamekuja kufungua mageti saa sita usiku, kijana wa watu aliyejiajiri kupitia muziki amepata hasara, amepata watu 200, 300 *TRA* wakakata hela zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *TRA* kama mnataka pesa kaeni chini na wasanii tutengeneze *strategy* nzuri itakayosaidia wasanii wa Tanzania wanapowekeza kupitia kitu kama hiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana

**SPIKA:** Muda umekwisha, naona Mheshimiwa alishaanza ku-*rap* tayari, tunakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea na Mheshimiwa Costantine Kanyasu na Mheshimiwa Abdallah Mtolea atafuata, nina tangazo. Napenda tu niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote kwamba juzi tarehe sita, siku ya Jumamosi palikuwa na michezo kadhaa kwenye uwanja wetu wa Jamhuri hapa Dodoma kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB.* Palikuwa na michezo ya aina tatu; palikuwa kwanza na mpira wa pete wenyewe wanauita *netball* ambapo *Bunge Queens* walishinda kwa mabao 19 na *NMB* 2. Kikosi cha *Bunge queens* kiliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika na nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Grace Kiwelu aliyefunga mabao mengi sana. Tunawapongeza sana *Bunge queens. (Makofi/Kicheko)*

Pia palikuwa na *Basketball* kati ya Bunge na *NMb* ambapo Bunge walishinda kwa mabao 39 na *NMB* 27. Nyota wa Mchezo huo alikuwa *Engineer* Ramo Makani, Mheshimiwa Ramo ni mzuri sana kwenye *Basketball. (Makofi)*

Vile vile pia palikuwa na mpira wa miguu *(football)* ambapo *NMB* haikupata kitu lakini Bunge walipata mabao mawili. Magoli ya Bunge yalifungwa na Mheshimiwa Omari Mgumba na Mheshimiwa Cosato Chumi. Nyota wa mchezo huo alikuwa *Goal-keeper* Mheshimiwa Hamidu Bobali ambaye aliokoa mikwaju mingi sana kutoka kwa *NMB* na tukaweza kushinda. *(Makofi)*

Nilipewa taarifa kwamba Mheshimiwa Jenister Mhagama pia ni mchezaji mzuri sana wa *Netball* lakini juzi tulim-*miss,* hatukuwa naye lakini tutajitahidi siku nyingine tukaone umahiri wake na yeye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge chachu ya ushindi wa siku hiyo ya juzi ambapo na mimi mwenyewe nilishuhudia mechi zote hizi tatu ni Mheshimiwa Salma Kikwete kwa aina yake ya ushangiliaji mkubwa sana, Mheshimiwa Janet Mbene pamoja na Kamati ya Ufundi na Hamasa iliyoongozwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani kama kawaida mtaalam, Mheshimiwa Joseph Selasini na kipekee kocha na mwelekezaji wa timu ya *Basketball* alikuwa ni Mheshimiwa Hawa Ghasia. Mheshimiwa Hawa Ghasia ni mtaalam kabisa wa *Basketball* alivyokuwa anaelekeza pale msingeweza kuamini Waheshimiwa Wabunge.

Pia mechi hiyo ya juzi ilitangazwa *live* na mtangazaji mahiri Mheshimiwa Amina Mollel, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Uongozi wa Bunge tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmeshiriki. Kama mnavyojua michezo ni afya, michezo ni furaha, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa na michezo kwa siku ambazo mpo Dodoma hasa siku za *weekend* basi ni vizuri kujitokeza pale uwanjani. Kwa kweli ni burudani ambayo hutajisikia kama umepoteza muda wako. Kwa hiyo ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi tuwe tunashiriki wengi zaidi, inasaidia katika kutuweka pamoja na kuonesha ushirikiano wa hali ya juu zaidi. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Constantine Kanyasu. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami naomba nianze kwa kutoa pole sana kwa familia zote ambazo zimeguswa na msiba ambao umetokea mjini Arusha kwa kipekee kabisa. Kwa kweli msiba ule ni pigo kubwa kwa nchi yetu, na tunafahamu kwamba kuna tukio linaendelea pale Arusha tunawatakia kila la heri na kwa kweli tunawapa pole nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yupo rafiki yangu mmoja yuko Marekani jana alinipigia simu akaniuliza na nikashindwa kutoa jibu na nilikuwa nataka watu wa Kiswahili watusaidie kutafuta, inawezekana likawa ni neno jipya ambalo linaitwa “Bashite” kutafuta maana ya Kiswahili ili liwekwe kwenye Kamusi. Kwa sababu kuna wakati walioko nje wanashindwa kupata *connection* ya mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nianze kwanza kwa kutoa shukurani nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwanza kwa kuonesha kwamba anajali michezo, lakini pili kwa upendeleo kabisa wa kuleta uwanja mkubwa wa michezo hapa Dodoma. Mikoa mingi sana haina viwanja vizuri vya michezo na ni nafasi pekee hii katika Mkoa wa Dodoma kupata uwanja ambao unaweza ukawa ni uwanja wa pili wa Kimataifa baada ya uwanja wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu katika suala hili, naiomba Wizara ihakikishe kwamba uwanja huu unakuwa na vitu vingi vya lazima. Hapa tunapoongea Tanzania hata pamoja na mchango mkubwa wa wasanii wa muziki, wasanii wa ngumi na aina nyingine za michezo, tuna maeneo machache sana ya michezo ya aina hii ambayo yapo. Hatuna ukumbi wa kisasa wa muziki, hatuna ukumbi wa kisasa wa ngumi, tuna maeneo tu ambayo ni ma-*hall* ambayo ni ya kawaida hayawezi kuhamasisha michezo hii ya Kimataifa. Kwa hiyo kuja kwa uwanja huu niombe wale ambao wanasaidia kwenye mipango wahakikishe kwamba uwanja huu unakuwa na *complex* ili uweze ku-*accommodate* michezo mingi na ya aina mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana wanamichezo wetu wengi, nianze na *under 17* ambao kipekee sasa wanaelekea Gabon kwa ajili ya michezo hiyo ya Afrika; niwatakie sana mafanikio mema.

Vilevile niwapongeze sana wachezaji wetu wa Kimataifa walioko nje ambao wanacheza mpira wa kulipwa kama Samatta, Ulimwengu na wengine, niwapongeze sana Mwanariadha Simbu, Cecilia, Ginoka, Magdalena, Emmanuel, hawa wameendelea kuiuza Tanzania kwenye ramani ya Kimataifa. Wasiwasi wangu ni mmoja tu; ni mchango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba mafanikio haya yanaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, ni bahati kubwa leo tunao akina Samatta, tunao hawa wanariadha wengine na kwa kweli kimsingi nchi hii kwa ukubwa wake na idadi yake ya watu, tungeterajia iwe na watu kama hawa zaidi ya 100.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa sasa kinachoendelea ni kwamba anajitokeza mmoja na yeye anakuwa kama wa dawa. Hii maana yake ni kwamba maandalizi ya kuwapata ha watu huku chini yamekuwa ni madogo na matokeo yake kila anayechomoza anachomoka kwa bahati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye eneo hili, miaka ya nyuma tulipata wanamichezo wengi sana walitokea kwenye Majeshi hasa JKT, Polisi na JWTZ. Nadhani sasa Serikali inapoelekeza kwenye kuchagua vijana hawa kutoka kwenye maeneo mbalimbali kwenye Wilaya iweke kipaumbele sana katika suala la michezo ili kuwapata vijana hawa wanaopelekwa kwenye maeneo haya waweze kuandaliwa vizuri waweze kuiwakilisha nchi yetu. Ni kwa sababu tu kwamba zamani pia tulikuwa na mashirika ya umma ambayo yalikuwa yanaweza kuwa na timu hizi za michezo. Baada ya mabadiliko ya sera, mashirika haya yakabadilisha mfumo matokeo yake ni kwamba hayana tena nafasi ya kuandaa wanamichezo wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani kwamba vyombo hivi vya dola ambayo kimsingi bado vina uwezo mkubwa wa kuwa na bajeti ya kutosha lakini na nafasi ya kuwaandaa vingeendelea.

Mheshimiwa Spika, nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kwa kweli niseme ni hotuba nzuri sana, nampongeza yeye pamoja na Naibu wake na Katibu wake Mkuu ambaye ni Mwalimu wangu, lakini napenda kusema upungufu kidogo ambao nimeuona hapa. Kwanza nilitarajia katika taarifa hii nione kwa kina inazungumzia uongozi mbovu na migogoro mingi iliyopo *TFF*. Kwa sababu ni kupitia mpira nchi yetu inaweza ikatengeneza wanamichezo wengine wapya kama Samatta.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa kabla timu ya Taifa ya Vijana haijaondoka, tulishuhudia vijana wale wanateremshwa kwenye basi kwa deni kubwa la kodi ambalo wanadaiwa *TFF* pamoja na *TRA*. Nikatarajia kuona ni namna gani sasa Wizara inaondoa aibu hii.

Mheshimiwa Spika, tuliona mwaka 2016 vyombo hivi vya mpira kama *FIFA*, *CAF* na *TFF* vilikuwa haviingiliwi na chombo chochote cha uchunguzi cha Serikali, lakini mwaka 2016 *FIFA*, *FBI* waliingia ndani, miaka kama kumi huko nyuma chombo cha Italia cha Usalama kiliingia ndani kuchunguza.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu sasa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wakati nachangia katika ripoti yangu mwaka 2016 na hasa nilipogusia suala la rushwa katika Chama cha Mpira cha Tanzania, nilimtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge na awaeleze Watanzania ni chombo gani *independent* ambacho kilifanya uchunguzi kama ilivyo *FIFA*, kama ilivyokuwa Italia na kama ilivyokuwa kwenye *CAF* hapa juzi, Rais mpya wa *CAF* alipochunguzwa kwa tuhuma za rushwa ambacho kiliihakikishia *TFF* kwamba sasa ilikuwa na uhalali wa kufanya maamuzi ya kuzishusha timu tatu za Majeshi ya Polisi na JWTZ, lakini pia na timu moja ya *Geita Gold Sport* ambayo ilishushwa daraja na kupandishwa timu nyingine kutoka nafasi ya tano kwa sababu za kuhisia.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo tunazungumza na nimetazama sijawahi kupata hiyo taarifa, pamoja na uchunguzi huo mkubwa uliofanywa na *PCCB*.

Mheshimiwa Spika, niliahidiwa hapa na Mheshimiwa Waziri, kwamba baada ya uchunguzi huo wahusika watapelekwa mahakamani na hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe angalizo hapa kwa Serikali, mahakamani mara nyingi tunashindanisha maneno na inawezekana kabisa kwamba mwenye haki akakosa haki mahakamani kwa sababu ameshindwa kujenga kesi. Hii maana yake ni kwamba pamoja na uchunguzi mzuri wa *PCCB* na ushahidi wote waliopewa na wahusika kwamba palikuwa na harufu ya rushwa kubwa *TFF*, mpaka leo inavyoonekana wale watu ambao walituhumiwa na ushahidi wote wanaelekea kuokoka.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nipate ushauri wa Mheshimiwa Waziri, ni kwa namna gani, ameitaja *TFF*, amezungumzia namna ambavyo anafikiria itaweza kusimamia michezo, lakini hajasema ni kwa namna gani anafikiria kuimarisha utawala bora kwenye *TFF*? Tunafahamu kwamba kwa mujibu wa sera, hizi ni taasisi ambazo zinajiendesha zenyewe, lakini kimsingi kama kuna rushwa, kama maamuzi yanayofanyika pale siyo ya haki, inakatisha tamaa wadau wa michezo.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, leo ni mwaka mmoja na nusu tangu *Geita Gold Sport* walipoomba *review* ya kesi yao baada ya kukata rufaa, *TFF* hawajawahi kutoa maamuzi wala hawajawahi kusema rushwa alitoa nani? Alipewa nani? Shilingi ngapi? Wameishia kwenda kumfungia mchezaji miaka kumi, wamemfungia kocha miaka kumi ambaye haijulikani pesa alitoa wapi, kwa sababu viongozi wake wote wanaonekana hawana hatia.

Mheshimiwa Spika, nilitaka pia Mheshimiwa Waziri aje atuambie hapa, inapotokea suala kama hili, ni nini hasa nafasi ya Serikali? Kwa sababu tukiruhusu hali hii kuendelea

tutafika mahali tutajikuta kwamba michezo ambayo inasemekana ni ajira haiwezi kuwa ajira tena. Wapo Watanzania wengi ambao sasa hivi wanafikiria wafike *level* ya Samatta, lakini kwa kukatishwa tamaa na matukio yanayoendelea katika *TFF* unaweza ukajikuta kwamba baadaye watu wote wanaona ni bora waachane na michezo wafanye kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, nimelisema hili kwa muda mwingi kwa sababu ni suala ambalo linaigusa timu ya Geita *Gold Sport* ambayo ni timu inatoka Geita, ambapo wananchi wa Geita waliipandisha kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka kusema, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais kuhusu kiwanja cha michezo, tumeona kwenye bajeti hii, lakini pia bajeti ya TAMISEMI, ni sehemu ndogo sana ya pesa ambayo inaelekezwa kwenye kuimarisha michezo. Kule kwetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu, tunakushukuru sana, wewe ni mwanamichezo inaelekea.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwataarifu kwamba kutokana na azimio ambalo leo mmelipitisha asubuhi ya leo ya kuchangia msiba wa watoto wetu 33, walimu wawili na dereva wa shule ya msingi Lucky Vincent Arusha ambao wamefariki kwa ajali ya gari Wilayani Karatu siku ya Jumamosi tarehe 6 Mei, michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo ningependa kuwataarifu baada ya mahesabu yetu ya kile mlichokiridhia ni kwamba tutakuwa tumetoa shilingi milioni 86. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo katika kuwaunga mkono, Ofisi yangu pia imetoa shilingi milioni 14. Hivyo jumla ya michango yote ambayo Bunge tutakuwa tumetoa itakuwa ni shilingi milioni 100. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, fedha hizi zinatumwa mara moja kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha kwa sharti la kwamba Mkuu wa Mkoa atahakikisha kwamba kila familia ya waliofariki itapata kiasi sawa cha fedha hizo ambazo Wabunge wamezitoa. Kama nilivyosema kwa msisitizo, zitakabidhiwa kwenye familia husika kwa ajili ya matumizi ya jambo hili na siyo vinginevyo. Nilitaka tu niwataarifu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia machache katika mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka salama na kunipa nguvu za kusimama mahali hapa asubuhi ya leo ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, pia naungana na Watanzania wengine wote kutoa pole kwa familia za marehemu waliopoteza maisha mwishoni mwa juma hili na tumwombe Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, lakini atupe nguvu na subira sisi wafiwa katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, nianze na *TBC*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza mambo mengi ya kuona namna gani anaweza kuiboresha *TBC*, lakini kwa maana ya kupanua usikivu wake na muonekano wake na kuiboresha yenyewe mambo ambayo yanahitaji sana fedha. *TBC* hii haihiitaji tu maboresho kwenye mambo ambayo yanatumia fedha inahitaji pia maboresho ya weledi na kujituma kwa wafanyakazi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TBC* imekuwa kituko na inashindwa kubeba hasa ile nafasi yake kama chombo na chanzo cha kutoa habari kwa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari ambazo zinarushwa na *TBC* kwanza zinakosa mvuto, watangazaji wenyewe ile kuchangamka tu, kwa sababu kuchangamka hakuhitaji Wizara ikutengee fedha ili uchangamke ukiwa *studio*. Mtangazaji anafanya kazi kama kalazimishwa, matokeo yake hata wanapozungumza habari za burudani ambazo ni za kufurahisha bado zinaonekana kama habari za msiba ambazo zinatia huzuni.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya kiweledi ambayo yanahitaji tu usimamizi mzuri na wafanyakazi hawa waambiwe kwamba *TBC* ndiyo chombo kinachotegemewa na wananchi. Kama hakuna mvuto wa kuingalia *television* hiyo, hivi mtu ata-*tune* vipi kwenye *television* ambayo haimfurahishi hata kwenye mambo yale ya kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli wa habari ambazo zinatangazwa na *TBC,* hivi juzi juzi hapa tulishuhudia kabisa habari ya kupikwa kwamba Rais wa Marekani, Donald Trump amesifia na kupongeza kazi zinazofanywa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Ni jambo zuri, lakini ukweli wenyewe wa habari ile ilikuwa ni ya kupikwa haikuwa ya kweli kutoka Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sasa unajiuliza, hivi jambo dogo kama hili *TBC* wanashindwa ku-*cross check,* kuthibitisha kwamba habari hiyo ni ya kweli! Tuna Ubalozi wa Marekani kutoka Bamaga kwenye Ofisi za *TBC* kwenda Ubalozi wa Marekani hazifiki hata kilometa tano. Hivi *TBC* ilishindwa kitu gani kwenda Ubalozi wa Marekani kuthibitisha kama kweli kuna habari hiyo ili watulishe habari ambazo ni za kweli na uhakika badala ya kutulisha habari za kupikwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwani Mheshimiwa Mtolea, wewe una uhakika gani kwamba habari hiyo siyo kweli?

**MBUNGE FULANI:** Walikanusha.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, habari hii ilikanushwa.

**SPIKA:** Ilikanushwa na nani?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, naamini kabisa na wewe habari za kukanushwa kwa taarifa ile ulizipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya sasa ndiyo yanawafanya Watanzania waache kuitegemea *TBC* kama chanzo cha taarifa na badala yake sasa tumejikita kwa *ITV* na *Azam TV* kwamba sasa zimekuwa kama *television* za Taifa badala ya *TBC. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri tu wakajitazama wenyewe ili waaminike na watu wengi wa-*tune* kwenye *TBC,* ni lazima wabadilishe namna ambavyo wenyewe wanafanya kazi zao za kila siku katika kituo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la ving'amuzi; wakati tunaimba kwamba tunabadilika kutoka *analogue* kwenda *digital,* zilikuja *concerns* kwamba watu watakaposhindwa kulipia ving'amuzi vyao watakosa kuangalia *television* na Serikali ilituaminisha kwamba kila muuza ving'amuzi atalazimika kuhakikisha kuna *local channels* angalau tano ziwe zinaonekana hata pale ambapo king'amuzi kitakuwa kimemaliza *bundle* lake. Kitu hiki sasa hivi hakipo.

Mheshimiwa Spika, usilipolipia king'amuzi huna *channel* utakayoiona na hata vile ving'amuzi vichache ambavyo wanaweka *channel,* basi hazizidi mbili. Ving'amuzi vingi usipokuwa na *bundle* hakuna *channel* yoyote utakayokuwa unaiona.

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania wanakosa fursa ya kuangalia *television* kwa sababu tu tumeingia kwenye *digital.* Sasa hili jambo ni la kisheria, linahitaji tu kusimamiwa kuhakikisha kwamba hizi sheria zinatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaouza ving'amuzi mnawafahamu, *TCRA* wako wapi? Kwa nini wasiangalie kama kweli zinakidhi hayo matakwa ya kuwa na *local channels* angalau tano ili ziwe zinaonekana pale ambapo watu watakuwa hawajalipia ving'amuzi vyao?

Mheshimiwa Spika, maisha yamekuwa magumu sana, siyo kila mmoja anaweza kulipia king'amuzi kila mwezi. Kuna miezi mingine mtu anashindwa kulipia. Sasa anaposhindwa kulipia, basi asikose uhuru wake wa kuangalia *television*. Kwa hiyo, tuwasaidie Watanzania hawa waendelee kuangalia *television* zao zisiendelee kubaki kama mapambo ndani ya nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni usalama wa waandishi wa habari. Kumekuwa na matukio hapa karibuni ya kuvamiwa waandishi wa habari wakiwa wanafanya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, najaribu kunukuu uvamizi uliofanyika katika kituo cha *Clouds,* lakini pia tukio lingine la kuvamiwa waandishi wa habari kwenye mkutano wa waandishi wa habari ulioitishwa na Chama cha Wananchi, *CUF* kule Mabibo. Matukio haya siyo ya kuyabeza, kwa sababu hao waandishi maana yake sasa hivi usalama wao wanapokuwa kazini umekuwa ni wa mashaka sana. Haturidhishwi kabisa na namna ambavyo Serikali ina-*react* katika kuyakabili matatizo haya. Serikali ina-*react very light* kama vile haya matukio siyo mazito kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, tunapowafanya waandishi wawe na wasiwasi katika kutekeleza majukumu yao, tunapoteza zile nguvu zao na *commitment* zao katika kufanya kazi zao kiweledi zaidi. Ni lazima Serikali iwe na mpango madhubuti

kabisa kuhakikisha waandishi wa habari wanafanya kazi katika mazingira yaliyo salama kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hapa kwenye suala la michezo, kwenye ukurasa wa 44 Mheshimiwa Waziri ameelezea sana michezo lakini amejikita zaidi kuelezea mpira wa miguu. Serikali isituaminishe kwamba tunapozungumzia michezo kwenye nchi hii, basi tunazungumzia mpira wa miguu pekee. Kuna michezo mingi katika nchi hii na ni lazima Serikali iisimamie yote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Mheshimiwa Waziri anazungumza tu hamasa za kuhakikisha *Serengeti Boys* inafanikiwa. Kuna michezo mingi zaidi ya huo ambao *Serengeti Boys* wanaucheza, sasa hao wanamichezo wengine Serikali inawasaidiaje? Tusisubiri tu mtu kashinda mbio huko, ndiyo tunamchukua tunamleta Bungeni hapa tupige naye picha. Tumewekeza nini katika kufikia mafanikio hayo?

Mheshimiwa Spika, tunawekeza kwa *Serengeti Boys* lakini sifa tunataka kuzichukua kwa watu wanaokimbia riadha, hili haliwezekani. Ifike mahali tukubali kabisa huu mchezo wa mpira wa miguu umeshatushinda, hatuwezi kufanikiwa, figisu zilizopo *TFF* ni nyingi. Tazama sasa hivi kuna mbinu za makusudi zinazofanywa na *TFF* kuhakikisha kwamba Simba inapata nafasi ya kushiriki kwenye mashindano ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani limetengenezwa zengwe kwa sababu *TFF* inaelekea kwenye uchaguzi wake, wameambiwa kwamba kwa sababu kwa miaka minne Simba haijashiriki mashindano ya Kimataifa, mtakosa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi *TFF* na wenyewe wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha eti Simba iwakilishe Taifa kwenye mashindano ya Kimataifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea, kidogo tu, maana toka ulivyoanza... *(Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, dakika zangu.

**SPIKA:** Kaa kidogo, muda wako tutautunza.

Napata taabu kidogo, vitu vyako unavyovisema ushahidi wake sijui unaotoa wapi? Eeh! Tuhuma hizo ni nzito! Unajua Simba ni *club* kubwa sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mtolea malizia hotuba yako. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, naamini dakika zangu utakuwa umezilinda vizuri.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yana ushahidi usiofichika. Duniani kote matokeo ya uwanjani yanaheshimika, hata kama kuna matatizo yametokea, wanaadhibiwa waliosababisha matatizo hayo, lakini siyo kuhamisha *point* kutoka timu moja kuzipeleka kwenye timu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuchezea haya matokeo ya mezani, yanaonekana tu hapa Tanzania, lakini huko kwingine kote mpira wa miguu watu wanaheshimu matokeo ya uwanjani.

**MBUNGE FULANI:** Serengeti imeenda kwa nini?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, *referee* akiyakubali...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea unapewa taarifa, ngoja upokee. Mheshimiwa Ester Bulaya, kuna nini?

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa taarifa ndugu yangu Mtolea kwamba hayo matokeo ya mezani ni kwa Simba; kwa *club* kama Yanga ambayo inatarajia kuchukua ubingwa, haipo kabisa. *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Kuna Mheshimiwa mmoja ameniandikia hapa kwamba kwa kuwa kanuni zinaruhusu *point* tatu kuhamia Simba, tatizo ni nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipokea kabisa taarifa aliyotoa Mheshimiwa Bulaya, naipokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo hapo tu. Siyo kwenye *point* tatu za *KageraSugar*, hawa Simba wameonyeshwa kubebwa kwenye maeneo mengi. Mechi ya kwanza Simba imecheza na Mbao, zikaongezwa dakika nne na refa akazidisha dakika mbili tena. Mechi ya pili, Simba imecha za na Mbao, refa akaongeza dakika saba, lakini kwenye kucheza zikaongezeka dakika kumi zaidi. Leo hii *Mbao FC* imeingia fainali na Simba kwenye Kombe la *FA* tayari viwanja vimebadilishwa mara mbili zaidi.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Taarifa!

**SPIKA:** Taarifa iko wapi hiyo? Mheshimiwa Mtolea, taarifa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, sisi kama *Mbao FC...*

**SPIKA:** Kuna taarifa kule. Mheshimiwa Mtolea hebu kaa chini kwanza. Taarifa tafadhali.

## TAARIFA

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba tu kumtaarifu Mheshimiwa mchangiaji kwamba mchezo wa soka ni mchezo unaoongozwa na kanuni na sheria. Kwa kuzingatia kwamba watu humu tumegawanyika Usimba na Uyanga, ili yaweze kwenda vizuri, naomba huko asielekee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tunachotaka kumtaarifu ni kwamba ukimpa mtu kadi tatu mfululizo anatakiwa a-*miss* mechi moja mwishoni. Kingine, pilipili usiyoila wewe yakuwashia nini? Kwa sababu Kagera siyo Yanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mtolea apokee taarifa. Ahsante sana.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE**: Mheshimiwa Spika, kuna taarifa hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, taarifa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpe mchangiaji taarifa kwamba akitaka ushahidi wanao *TFF*, kwamba ma–*referee* sita waliochezesha Yanga wamefungiwa mwaka huu kuonyesha kwamba Yanga niwatoa rushwa, Yanga ni wababaishaji kwenye michezo, *TFF* imewafungia. Yanga katika mechi zote alizocheza na Simba, wamepewa kadi nyekundu Simba na Yanga kafungwa naye anajua. Sasa Yanga ana uwezo gani? Nampa taarifa kwamba Yanga ndiyo wanaobebwa kuliko timu yoyote kwenye ligi. Wana tawi linaitwa Toto, linafungwa kila mechi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona sasa Mheshimiwa Nchemba amesimama na Waheshimiwa wengine wamesimama. Naona mjadala wa Mheshimiwa

Waziri unataka kuharibika sasa. Kwa hiyo, meza naamua sasa mambo ya Simba na Yanga basi yaishe, tutayamaliza uwanjani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mtolea kama una mengine endelea kumalizia dakika zako. Kwa hiyo, hayo ya Simba na Yanga naomba sana hebu yaishie hapo. Malizia dakika zako. *(Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba pamoja na madaraka makubwa uliyopewa na Kanuni ya tano, lakini pia unaitumia hiyo Kanuni ya tano kwa kuheshimu pia Kanuni ambazo zinanilinda mimi katika uchangiaji na unafahamu tunapochangia hapa tunakuwa tumejipanga, tumejiandaa kwa muda mrefu ili tufikishe kilio cha Watanzania na Serikali iweze kukifanyia kazi. *(Makofi)*

Pili, zimetoka taarifa hapa sasa sijui unanipa nafasi na zenyewe kwanza nizipokee au nizikatae japo kwa dakika moja au unanisaidiaje katika hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Bahati mbaya sana muda wako umeisha Mheshimiwa Abdallah Mtolea. Mheshimiwa John Kadutu. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya yangu kuendelea kuimarika. Nitumie fursa hii kuwatoa wasiwasi wapiga kura wa Ulyankulu, nina imani Mwenyezi Mungu atanilinda mpaka 2020 tukamalizana salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake Kwa hotuba iliyoletwa mbele yetu na kwa sababu Mheshimiwa Mwakyembe hana muda mrefu pale, pamoja na kwamba yeye ni mtu wa habari, lakini tumkaribishe na tuna imani naye, kazi itakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza mtangulizi, Mheshimiwa Nape. Sisi wanamichezo tulifarijika

sana naye na niseme tu alifanya kazi nzuri, haya mengine ni ajali za siasa. Nimtie moyo Mheshimiwa Nape, asikate tamaa na kwa sababu yeye ni msanii, basi aendelee kuwepo kwenye vuguvugu letu hili la michezo na usanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu sasa timu yetu ya *Serengeti Boys* kama siyo jana basi watakuwa wameshafika Gabon. Ni juu ya sisi sote kuonyesha mshikamano juu ya timu hii. Kuzijenga timu, hazijengwi kwa maneno. Kuzitengeneza timu zipate mafanikio, hazitengenezwi kwa maneno. Kwa sasa nchi nzima na familia ya wanamichezo tunachangia mafanikio na gharama mbalimbali za *Serengeti Boys.* Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tushiriki basi kwa dhati badala ya kushiriki kwa maneno tu na kuwalaumu wenzetu wa Wizara kana kwamba kila jambo wanafanya wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata huko Hispania, Madrid, Barcelona wapo watu wanahangaika nazo. Ukienda Uingereza, Liverpool, Manchester United au timu ya wenzangu wale ambao wanaishi kwa wasiwasi Arsenal, zote hizi zinatengenezwa na watu. Tusiishie tu kusema maneno na kulaumu, tujaribu kushiriki na sisi katika kuhakikisha maendeleo haya tunayoyasema yanafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo ambalo kila mwaka mimi nalisema, hata kabla sijaingia Bungeni nimekuwa nikilisema. Mimi kama mwanamichezo ni juu ya michezo mashuleni. Hiyo *Taifa Star* tunayoizungumza ya mwaka 1980 iliyocheza mpira kule Nigeria, sehemu kubwa ya waliocheza kule walitoka mashuleni, walitengenezwa.

Mheshimiwa Spika, michezo ya shule za msingi, michezo ya sekondari, michezo ya vyuo ilikuwa ni chachu ya kutengeneza wachezaji kwenye michezo yote. Iwe riadha, iwe mpira wa miguu, iwe *netball* ambayo sasa sijui inaelekea kufa, itabaki Bungeni tu sijui! Yote ilitengenezwa kutoka mashuleni. Sasa hatutaki kusema juu ya waliotangulia wakafuta michezo ile mashuleni adha yake tunaiona.

Mheshimiwa Spika, sasa michezo imebaki kwenye shule mbalimbali chache ambazo siyo za Serikali, wanatusaidia sana kuhakikisha michezo inakwenda vizuri. Je, Serikali, TAMISEMI, Wizara ya Habari na Wizara ya Elimu kwa nini sasa isishirikiane kuhakikisha michezo mashuleni inarudi kama zamani na iwe ndiyo jiko letu la kupika wachezaji na wanamichezo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hebu utakapokuwa unakuja kuhitimisha, hebu ingia kidogo pale utufafanulie mambo yalivyojipanga kwa ajili ya michezo mashuleni. Bahati mbaya simuoni Mheshimiwa Profesa Ndalichako, angekuwepo na yeye ni pamoja na Mheshimiwa Simbachawene, hizi Wizara zote tatu zishirikiane...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndalichako yuko Arusha, kutuwakilisha kwenye lile jambo la msiba ule mkubwa.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Spika, ahaa basi.

**SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu na mimi sikuwepo.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni kwamba Serikali iko hapa, ione umuhimu huo. Badala ya kuwa tunasubiri mafanikio tu kama alivyosema Mheshimiwa Mtolea, kwamba tunasubiri mtu ameshinda huko, tunamleta hapa Bungeni na kupiga naye picha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikizungumzia juu ya Watoto, mabingwa wa Dunia wa michezo ya Watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Timu yetu ya Mwanza na mwaka kesho tunakwenda Kombe la Dunia; je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuisaidia hiyo timu ikafanye vizuri? Hivi karibuni timu ya walemavu ilikuwa inashiriki mashindano pale Uingereza; je, inasaidia nini kutaka kwa watoto hawa?

Mheshimiwa Spika, suala nyingine ni juu ya viwanja. Bahati mbaya sana Serikali yetu haina viwanja vya kutosha. Tunavyo viwanja hivyo; Kiwanja cha Uhuru pamoja na Uwanja wa Taifa, lakini muda sasa umefika Serikali itengeneze viwanja vyake yenyewe, kuliko kutegemea viwanja ambavyo sasa ni mali ya taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, pia viwanja hivyo visitengenezwe Dar es Salaam tu. Dodoma hapa tunahitaji kiwanja, tunahitaji kiwanja Mwanza, tunahitaji Arusha, viwanja vya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni juu ya makato. Mimi nashiriki sana michezo hii, makato ni makubwa sana kwenye viwanja. Watu wanakusanya pesa lakini pesa hizi zinakusanywa na wachezaji. Wachezaji wanachapa kazi ndiyo maana pesa inapatikana, lakini makato ni makubwa kiasi kwamba yaani faida inayobaki iwe kwa *TFF*, iwe kwa Chama cha Mpira cha Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mpira Mkoa wa Tabora. Nafahamu, yaani kinachokuja kubaki ni kitu kidogo sana. Serikali basi iangalie; je, inajenga viwanja hivi kuwakomoa wanamichezo? Je, inajenga viwanja hivi ili shughuli ibaki ya matamasha au ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tuna michezo ya Afrika Mashariki ya Bunge. *BungeSports Club* imesajiliwa kwa kanuni zile zile kama za Simba, kama za Azam kama za Yanga. Tuna michezo hii lazima Wizara ioneshe kutuunga mkono kama *Bunge Sports Club*. Tumekuwa ni watu ambao kama vile sisi tunacheza michezo mingine tu ambayo haitambuliki. *Bunge Sports Club* na ninyi Mawaziri mko humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, *BungeSports Club* ni *club* ya Wabunge wote na wafanyakazi wote. Nawaomba Mawaziri kutumia jukwaa hili; Mawaziri fikeni basi mje mfanye

mazoezi na sisi. Pia mshiriki, muwepo kutuhamasisha kuona kwamba michezo ya Afrika Mashariki inayokuja tunaweza kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja ya Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kadutu kwa mchango wako, Mwenyekiti wa Chama cha *Football* Mkoa wa Tabora.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Taska Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Omar King.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii. Kwanza nianze kwa kutoa pole nyingi sana kwa wananchi Mkoa wa Arusha, kwa Watanzania wote, kwa walimu wote wa shule ya Lucky Vincent, mmiliki wa shule, wazazi waliopoteza watoto wetu wapendwa, nawaombea Mungu awape ujasiri wa kukabiliana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie Wizara hii kwa mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nilikuwa naomba kuelewa kwenye Halmashauri zetu kuna Afisa Michezo na Afisa Utamaduni. Sasa nilikuwa naomba kujua hawa watu huwa wanawajibika kwa nani? Mwajiri wao anakuwa ni Wizara ya Utamaduni au anakuwa ameajiriwa pale Halmashauri? Kazi zao zinakuwa ni zipi, kwa sababu ukiangalia kwenye michezo; michezo ndiyo hiyo imedorora mashuleni. Ukingalia pia kwenye utamaduni, utamaduni ni huo nao umedorora mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka miaka ya nyuma wakati sisi tunasoma, sisi tuliosoma zamani, kulikuwa na mashindano ya michezo. Unakuta zinakusanywa shule za

*primary* za Wilaya hiyo zinashindanishwa na shule moja inaibuka inakuwa mshindi, inapewa zawadi ya kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye suala la utamaduni, kulikuwa na mashindano; shule za *primary* zinashindana ngoma za utamaduni na shule moja inaibuka mshindi wa utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika kuimba kulikuwa na mashindano. Kwenye utamaduni walikuwa wanaweka mashindano ya nyimbo, ngoma, wanaimba ngoma za makabila tofauti na nyimbo zinatungwa zenye maudhui ya nchi hii ambazo zingekuwa na mafundisho. Wakati ule sisi ilikuwa ni mambo ya siasa za ujamaa, kwa hiyo, wanaimba nyimbo za ujamaa ambayo pia zilisaidia kuwajenga watoto mashuleni na kutujenga sisi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitu kama hivyo sasa hivi sivioni. Kwa hiyo, huwa inaniwia vigumu, halafu unapoenda kwenye Wilaya unashindwa kujua kazi za Afisa Utamaduni na Afisa Michezo aliyeko Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, wengi mtakumbuka, michezo imeibuliwa kule mashuleni, mimi ninao mfano wa watu ambao waliiwakilisha nchi hii nje ya Tanzania na wakaikletea medali. Mwinga Mwanjala ni mchezaji ambaye aliibuliwa toka *primary school* na akaenda akaiwakilisha nchi hii, akaleta medali. Nzaeli Kyomo aliibuliwa toka *secondary school,* akina Gania Mboma wote hao waliibuliwa toka mashuleni na wakaweza kuiletea medali nchi hii na wakailetea heshima nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba na niungane na wenzangu waliotangulia, michezo irudishwe mashuleni. Wizara ya Elimu irudishe mashuleni michezo iwe kama kipindi, kama ambavyo zamani tulikuwa tuna vipindi vile vya michezo. Pia viwanja vya michezo vijengwe vingi kwenye mashule. Shule inapoanzishwa wahakikishe kwamba ina kiwanja cha michezo; aidha iwe ni Shule ya *secondary,*

*primary* kwa Shule za binafsi au Serikali viwanja vya michezo viwepo pale; iwe ni *condition* moja ya kuanzisha hiyo shule ili kuibua hivyo vipaji. Kwa sababu naona wachangiaji mnasema kwamba hatuna wawakilishi, mnaongea mambo ya mpira ya miguu kwamba Tanzania inakosa kwenda kucheza michezo ya kuiwakilisha nchi labda kwenye Kombe la Dunia au Kombe la Afrika, lakini ni kwa sababu tumeshindwa kuibua vipaji vya watoto ambavyo vinapatikana kwenye shule zetu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye utamaduni. Naomba nizungumzie suala la utamaduni; katika kitu ambacho mtu unaweza ukapoteza heshima yako ni kukosa utamaduni wa nchi yako au kabila lako.

Mheshimjiwa Spika, naomba hizi nyumba za makumbusho ambazo zimejengwa kule Dar es Salaam na moja iko kule Arusha, labda na Mwanza wanayo, naomba Wizara hii izingatie, hizi nyumba za makumbusho zijengwe kila Mkoa. Ninaamini kwamba kila Mkoa una utamaduni wake na kila Mkoa una makabila ambayo yalikuwepo kwenye huo Mkoa tangu wakati huo, ambao wana mila zao na vitu vyao vya zamani ambavyo walivitumia. Hivyo vitu vingeweza kuhifadhiwa kwenye nyumba za makumbusho za kila Mkoa ili iwe faida kwa kizazi kilichopo na kizazi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kama sisi tutakuwa tumepotea, lakini pale mkoani watoto wataweza kwenda kutembelea kwenye zile nyumba za makumbusho na kuona vitu ambayo vilitumika zamani na wazazi wao. Kwa sababu mimi naamini kwamba mkataa kwao ni mtumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Uingereza wameweza ku-*maintain* vitu vyao vya asili na sehemu zao za asili ambazo zilikuwa zinatumika tangu enzi za *King George.* Unakuta yale maeneo yao ya asili yapo mpaka leo yanatumika kama makumbusho na wanakwenda ku-*visit.(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hayo maeneo, kila Mkoa utenge sehemu ambayo watajenga nyumba ya makumbusho ambayo watahifadhi vitu vya makabila ya Mkoa huo kwenye nyumba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la mchaka mchaka. Nilikuwa naomba Wizara ya Elimu ishirikiane na Wizara ya Michezo mchaka mchaka urudi mashuleni. Sisi wakati tunasoma, tulikuwa tunakimbia mchaka mchaka asubuhi. Ni kiasi kwamba watoto wanapofika pale shuleni kabla hawajaingia darasani, wakimbie mchaka mchaka, wazunguke hata eneo la shule ili wawe wakakamavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoona, Mheshimiwa Makamu wa Rais amesema kwamba watu wafanye mazoezi. Sasa kwa nini hayo mazoezi yasianzie kwenye shule zetu? Maana yake tunahimiza watu wazima wafanye mazoezi kama anavyosema Makamu wa Rais, basi na pia na mashuleni tuwahimize watoto wakimbie kabla hawajaingia madarasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nilikuwa naomba kuwe na paredi mashuleni, watoto wafundishwe kuimba Wimbo wa Taifa. Ni aibu unamkuta mtoto anamaliza Darasa la Saba hajui kuimba Wimbo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sisi zamani tulikuwa tunaimba Wimbo wa Taifa kabla hatujaingia darasani. Siku hizi sijui kama vitu hivyo vinatekelezwa. Ingewekwa tu kama *policy* kwamba watoto kabla hawajaingia darasani, waimbe Wimbo wa Taifa. Hii ni kwa faida yao, pia ni kwa faida ya nchi yetu. Sisi zamani mbona tulikuwa tunaimba Wimbo wa Taifa kabla hatujaingia darasani. Kuwe na paredi na mchaka mchaka, nilikuwa naomba nisisitizie hilo kwenye mashule. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Eeeh, watoto wanakuwa wazembe.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, hii itawapa ukakamavu na pia itawajenga kutokufikiria vitu vingine, kwa sababu mtu anakuwa amekimbia, mwili umechangamka, anapofika mle darasani ana-*concetrat*e na shule, Ndivyo sisi tulivyolelewa. Vitu ambavyo tulilelewa ambavyo vilitusaidia sisi tunapaswa tuvipeleke kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu wasanii hizi kazi za wasanii waweze kupata haki zao, lakini pia usajili wa kazi za wasanii nilikuwa naomba labda wangeweka mpaka mikoani. Kwa mfano, kule kwetu Katavi, mtu atatokaje Katavi aende mpaka Dar es Salaam kwenda kusajili hiyo kazi yake? Kwanza kuna nauli, halafu kuna hizo kodi ambazo atatumia, pesa zenyewe za usajili nimesikia hapa mnachangia, sio mtalaam sana kwenye mambo ya usanii, lakini mnasema sijui shilingi 300,000 kodi sijui ya nini.

Mheshimiwa Spika, kwa kijana ambaye anaanza maisha, hiyo inakuwa ni hela ngumu sana kupata ili aweze kusajili kazi yake. Kwa hiyo, naomba ili kuwawekea unafuu, hizo ofisi za usajili za kazi za wasanii ziweze kupelekwa mpaka mikoani ili na wananchi hata na wale wasanii wangu wa kule Katavi waweze kusajili kazi zao kwa wepesi zaidi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba vitu vya zamani virudishwe. Kwa mfano, kulikuwa na zile sikukuu ambapo ilikuwa zinaweza kukutana ngoma za Mkoa huo zikashindanishwa na zikapewa zawadi. Zawadi siyo lazima iwe kubwa, lakini hii inatufanya tusipoteze utamaduni. Ndiyo maana unakuta mara nyingi mnawalaumu vijana wa sasa hivi wakitunga miziki sijui wanaimba miziki ya *hip pop* na nini, ile miziki wanayoiga kule ilitumiwa zamani na Waafrika weusi ambao walikuwa wanadai uhuru, ndiyo ikaja hii mambo watoto wakiimba wana-*rap*. Sisi tunayo miziki yetu ya asili ambayo inatutambulisha sisi kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, napata utata sasa hivi ninapoona kwamba hivi Mtanzania anaweza akasimama hapa akasema muziki wake wa asili ni upi? Kwa sababu naona miziki yote imechanganywa na utamaduni... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska umalizie.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Utamaduni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Mbogo, umechangia vizuri sana kuhusu kuimarisha michezo mashuleni.

Mheshimiwa Ali Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali nitangulize shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na aliyetufanya tukaja leo hapa katika mazingira ambayo tuko salama.

Mheshimiwa Spika, pili, tutoe pole kwa familia ambazo zimepata msiba kutokana na tukio ambalo limetokea ingawa inajirejea, lakini kipekee nahisi sitaitendea haki nchi yangu bila kutoa pole kwa janga ambalo limetokea.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia suala hili, kwanza nianze na chombo muhimu sana ambacho ni *TBC. TBC* ukiangalia katika dira yake, kwa mujibu wa kitabu ambacho kimetolewa na Mheshimiwa Waziri hapa, ni kwamba kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri na katika

dhima wakaandika kwamba upatikanaji stahiki wa habari; halafu tukija katika *slogan* yao wanasema, "Ukweli na Uhakika."

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na dhima hii na dira ambayo imeelezwa ya *TBC,* moja kwa moja ni kwamba *TBC* inataka kutuhabarisha Watanzania habari za ukweli na uhakika na ndivyo walivyoji-*position.* Hapo hapo, habari hizo za ukweli na uhakika bila ya kuwa na miundombinu mizuri, bila hawa *TBC* kuwezeshwa hatutaweza kupata habari za ukweli na uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukisema habari za ukweli na uhakika, wakati mwingine inawezekana kikatangulia chombo kikatoa habari ambazo siyo za ukweli na siyo za uhakika. Sasa *TBC* baadaye ndiyo ije ikanushe. Sasa inaweza ikachelewa kutoa habari kutokana na miundombinu ambayo wanayo au mazingira ya kazi ambayo yapo. Sasa ili tuihabarishe vyema jamii yetu, basi hapa tunahitaji tuwekeze katika *TBC.* Tutakapowekeza katika *TBC* ina maana tunawekeza katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Serikali inafanya mambo mengi sana ambayo chombo cha kitaifa kipo cha *TBC,* kwa hiyo, kinao uwezo wa kuitangaza Serikali kupitia mambo yote ambayo wanayafanya. Kwa hiyo, tunaomba kwa Mheshimiwa Waziri kwamba tuangalie zaidi katika hii *televison* yetu au chombo hiki ili tuwekeze mtaji wa kutosha ambao naamini utatulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara hii ya Habari kwa kuifanya Zanzibar sasa ni mwanachama katika Shirikisho la Soka Afrika. Najua hizi jitihada zilifanywa na *TFF.* Kwa hiyo, napongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina pongezi nyingine lakini pamoja na ombi, tunajua kuna mchakato pengine kwamba Zanzibar pia iweze kutambuliwa na *FIFA.* Kwa hiyo, nalo hilo pia tunapongeza kama mchakato huo utakuwa unaendelea,

utakuwa unakwenda kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, hapo nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufanya kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nakumbuka hapa tumepisha sheria ambayo inahusiana na vyombo vya habari na wanahabari, ukatengwa mfuko wa taaluma kwa ajili ya waandishi wa habari. Kwa hiyo hili Mheshimiwa Waziri lisimamiwe vizuri, kwa sababu lengo la sheria ile moja ni kuwawezesha wanahabari. Kwa hiyo, tutenge fedha za kutosha na tulisimamie ili tuweze kuwa na wanahabari wazuri na waweze kutoa habari zao kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nije katika soka ambalo linazungumzwa; nazungumzia kuhusiana na habari za *academy.* Tunajua Wizara ndiyo mlezi wa michezo. Basi Wizara iweke sheria, utaratibu na vivutio ambavyo vitawawesha watu kuweka hizi *academy*, kwa sababu siyo rahisi *academy* zote zikawekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, yakiwekwa mazingira na vivutio, inaweza ikachangia kabisa kuwa na wanamichezo wazuri, siyo kwa soka peke yake katika *academy*, tunaweza tukawa na *academy* za mambo mengi kama kuogelea na mambo mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni muhimu, nilisikitika sana hapa kumsikia mtu mmoja anauliza katika kuchangia hotuba hii kwamba Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi yuko wapi, labda anaweza akawa ametekwa. Kwa taarifa tu, kwenda kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi hakuingizi kwenye chama. Katibu Mkuu siyo kazi yake kumwingiza au kupokea mwanachama. Katibu Mkuu kazi yake ni kuongoza chama. Kwa hiyo, nami namshauri Mheshimiwa Lema, kama anataka kuja CCM, apite katika shina lake kule Arusha, apite katika ngazi ya Tawi, atapatiwa kadi na atajiunga na chama chetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kwenda kumtembelea Katibu Mkuu siyo kuingia katika chama. Kwa hiyo, uje ufauate

taratibu hizi za chama na miongozo ambayo ipo. Kwa nini umshike Katibu Mkuu wetu? Ninyi mmechagua Katibu Mkuu siyo zamani sana, lakini hajulikani. Hilo ndiyo tatizo, kwamba hatambuliwi. Sasa unaanza kuingia kwa Katibu Wakuu wa wenzako. Pilipili iko shamba, inakuwashia nini? Eeh, pilipili iko shamba inakuwashia nini au ndiyo kiherehere? *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili walifahamu vizuri kwamba siyo jambo la kusema unazungumza hivyo.

Mheshimiwa Spika, lingine, nizungumze jambo ambalo limewahi kuzungumzwa na watu wengine katika sanaa. Tumeweka sanaa katika mazingira ambayo wasanii wanaweza wakajiajiri na wasanii wanaweza wakajiajiri kupitia njia mbili; wanapoweza kufanya sanaa zao wakazi-*record,* lakini pia huwa wanafanya maonesho ya *live;* tuchukulie mfano kama michezo hii ya kuigiza au muziki. Sasa kumetokea sintofahamu, kitu ambacho hakijulikani kimetokea vipi?

Mheshimiwa Spika, wasanii wameshajiandaa kufanya *show*, tayari wanavamiwa. Sasa ile ajira ambayo tunasema kwamba itatokana na sanaa, au itapatikana kutokana na sanaa, inakufa. Unapokwenda katika kumbi zile katika michezo hii au katika kumbi za sanaa unaweza ukakuta askari wanavamia. Sasa hili siyo jambo zuri, kwa sababu tunawavunja moyo, kwa sababu wao wanapata mapato yao kwa mujibu wa kuuza kazi zao na kufanya maonesho ya *live* ambayo watu wanaingia kwa vingiilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano, kwa sababu inawezakana ikawa Wizara yake imeruhusu, lakini pengine inawezekana kuna muingiliano. Kuna baadhi ya Mikoa mingine wasanii hawana raha; wanaingia kwenye *show* wanabebwa pamoja na watazamaji. Kwa hiyo, hili naomba lingeangaliwa likafanyiwa utaratibu mzuri ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine katika timu yetu hii ya *Serengeti Boys*, ni kweli timu yetu inafika mbali, lakini tunahitaji kuwekeza katika soka. Tusiwe na *Serengeti Boys* hii ambayo kwa mwaka huu imeonesha mfano; na tuliwahi kuwa na timu kama hiyo miaka ya nyuma ya akina Ngasa na wenzake waliokuwa katika timu ile ya *Serengeti Boys* iliyopita. Inapita miaka mitano halafu ndiyo inakuja kuibuka *Serengeti Boys* nyingine ambayo inaweza ikatupa matumaini Watanzania. Hili jambo tunaomba liwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kama tunakumbuka katika soka, wachezaji wengi sasa hivi ambao wanamalizia umri wao kucheza, walitoka kwenye *Serengeti Boys,* lakini toka timu ile ilipokuwa ikifanya vizuri, basi mpaka leo imekuja hii nyingine ndiyo inatufuta machozi.Kwa hiyo, tunakaa sana, miaka 10, 15, ndiyo inatokezea timu nyingine ya vijana, inaundwa inakuwa inafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, tuliangalie hili, timu zetu hizi ziwe endelevu. Tulishashika usukani katika kuingia mashindano ya Afrika, basi tuwe tunaonekana pale mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tujaribu kufanya kitu kama hicho kingine katika riadha, isiwe mwaka huu, tumeshinda kwenye riadha au tumepata nafasi ya tano kwenye riadha katika mwaka huu, wengine wameshinda China kule, wengine wameshinda India. Sasa isije ikaja ikapotea hii, hizi nguvu ambazo tumezitoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Maulid Mtulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima. Pili, nakushukuru nawe Spika wangu kwa kunipa fursa ya kuzungumza katika Wizara yetu hii muhimu sana kwangu nikiwa kama Mbunge wa Jimbo la Kinondoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwanachama wa *Simba Sport Club* na kadi yangu ni hai. Kuna maneno yamesemwa hapa lazima yawekwe sawa. Nashukuru uligundua kwamba yanayosemwa hayako sawasawa, ukaamua kusimamisha sasa mimi kwa sababu nakuja kusema sawa sasa, *record* tuna-*balance story*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza timu ya Simba ndiyo timu bora kabisa Tanzania. Vile vile ndiyo timu ambayo imecheza vizuri na imeshinda mechi zake na hasa mechi zote ngumu. Wanaodai kwamba tunapendelewa, *record* zinaonesha tumewafunga Zanzibar, tumewafunga juzi pale na wanamkumbuka sana Kichuya na kona zake. Kwa hiyo, suala la upendeleo kwa Simba halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hiyo mbao iliyowatoa machozi, ikawafanya wasicheze fainali, sisi tuliwafunga Mwanza na wao wakafungwa Mwanza. Kwa hiyo, ukitafuta timu ambayo ina kiwango kidogo na ambayo siku ukienda kwenye mechi za Kimataifa wanatutia aibu sana hawa wanaobebwa halafu... *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia!

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Naam naam!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wala tusizozane sana kuhusu Simba. Nawaunga mkono watumie hizo mbinu zote wanazotumia kwa sababu gani? Watoto wa miaka 12 tangu wazaliwe hawajawahi kuishuhudia Simba ikichukua ubingwa. Sasa kwa mimi ninayeshughulikia usalama, itakuwa hatari sana. Yaani ikishindikana kwa kucheza, ikashindikana kwa *point* za mezani, jambo pekee litakalosalia itakuwa ni kuiba lile kombe ambacho kitakuwa ni kitu cha hatari sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiunga mkono kwa kweli! Nchi za jirani mpaka wanauliza, hivi Simba ilishashuka daraja ama vipi? Maana yake ni miaka mingi. Kwa kweli wekeni mipango sawa; na hivi ikizingatiwa mwaka kesho kombe linaenda Singida, yaani ni vyema mkapambana kwa muda huu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia taarifa hii; unaipokea Mheshimiwa! *(Kicheko)*

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii siipokei, kwa sababu *record* zinaeleweka kwamba Simba siyo muda mrefu tu ilikuwa inashiriki na imeshiriki kwa ufanisi na ukizungumza timu ambayo inatambulika nchi hii, hakuna kama Simba. Tunawashinda kwa kuanza hata kuvaa viatu, sikwambii kuvaa jezi. Kwa hiyo, Simba ni timu ambayo haiwezi kusahaulika na timu ambayo watu hawawezi kuisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha msingi hapa ambacho nataka tukieleze ni kwamba mpira wa miguu una sheria na taratibu. Bahati nzuri msemaji kasema kabisa anataka Wizara iachane na soka, ifuate michezo mingine. Bila shaka yeye ana mchezo mwingine zaidi ya soka, japokuwa hajausema, naamini utakuwa labda kuogolea au kuvuta kamba. Kwa hiyo, hafahamu vizuri Sheria za Soka.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Soka imewekwa kabisa kwamba mchezaji akipata kadi tatu, haikupaswa hata Simba kukata rufaa, ni *automatic* kwamba mtu amevunja sheria, wasimamizi wa sheria wanatakiwa Simba wawape *points* zao. Kama hili halitoshi, sisi leo tunakwenda Gabon kule, kwa sababu wale ambao walipata ushindi kinyume na utaratibu walinyang'anywa zile *points.* Sasa nashangaa leo hao hao wanashangilia Gabon lakini utaratibu huo huo ukiwa kwa Simba inakuwa nongwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niweke hayo mambo sawa, Simba ni timu makini, itachukua ubingwa, makombe yote mawili, bila kubebwa na huyo Yanga tunamsubiri tutaonana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, naiomba Wizara isaidie sana timu zetu hizi kubwa Simba na Yanga. Nikiri kwamba Wizara hasa Mheshimiwa Waziri, tumekubaliana tupate muda tukae tujadiliane kuhusu michezo na mambo ya sanaa katika Jimbo langu la Kinondoni, lakini timu zetu hizi za Simba na Yanga ni timu ambazo zinaunganisha umoja wetu. Leo mimi na ndugu yangu Mheshimiwa Mtolea nahitilafiana naye, lakini naungana na Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa wengine wa CCM. Leo usishangae Mheshimiwa Mwigulu Nchemba akakaa pamoja na kiongozi wangu Mheshimiwa Mbowe katika soka. Sasa hizi timu zina umuhimu mkubwa sana, kwa sasa hizi timu zinalinda mpaka utaifa wetu, tunaweza tukahitilafiana kwenye vyama, lakini tukakutana kwenye mpira.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako hatuhami timu hizi. Unaweza kuhama vitu vingine vyote, lakini ni ngumu sana kuhama timu. Sasa kama timu hizi zimefika mahali zinalinda utaifa wetu, Wizara sasa izisaidie hizi timu. Msaada ambao nautaka kwa Wizara; hizi timu zimeanza miaka ya 1930, 1936 ni timu ambazo zimeanza siku nyingi, lakini inaonekana huko nyuma viongozi walifanya kazi kubwa. Wamejenga majengo. *Clubs* zote zina majengo makubwa. Wamejenga imani ya watu, *Clubs* zote zina wapenzi wengi,

lakini inaonekana sasa hivi viongozi wetu wameshindwa kututoa pale walipotufikisha wazee kutupeleka kule tunakotamani. Nahisi kuna tatizo la menejimenti, kuna tatizo la ufahamu wa uendeshaji hizi *clubs* zetu kama wanavyoendesha wengine.

Mheshimiwa Spika, timu ambazo zina wapenzi wa kutosha, lakini ndiyo timu ambazo zinaongoza kwa kuombaomba, ni timu ambazo zinaishi kwa kutegemea wafadhili. Wakati mwingine inashindwa hata kututumia sisi wanachama wake na wapenzi wake. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atafute namna ya kukaa nao na atumie wataalam wake wa Wizara kuzisaidia hizi timu ili ziweze kutumia rasilimali zake ilizokuwa nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye muziki. Mimi natoka Jimbo la Kinondoni, Jimbo la Ma-*star*, nina Wasanii wa kutosha kabisa. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Waziri ameniambia tutafanya vikao vyetu na vijana hawa. Naomba jambo la kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi ni mpenzi mkubwa wa wanamuziki wangu wa Kinondoni, nikianza na mtu mzima Diamond; na kwa sababu Diamond na Ali Kiba wanakuza muziki huu wa kizazi kipya, naye namtambua na nampenda sana.

Mheshimiwa Spika, pia mimi ni mpenzi wa muziki mpya unaitwa singeli. Huu huwezi kumsahau Msaga Sumu, kijana Manifongo, hata Profesa J, ametoa muziki wake mmoja anasema Kazi, Kazi. Anasema watu wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, hawa vijana wakati wanafanya hizi kazi zao, Wizara yetu inatakiwa iwalinde. Niliwahi kuzungumza na Diamond, yeye kama yeye muziki wake unatumika kwenye Makampuni ya Simu kama milio ya simu, lakini malipo anayoyapata hayaendani kabisa na thamani ya muziki wake. Wizara sasa iingilie, iwahoji, wanatumia vigezo gani kuwalipa hawa vijana wetu?

Mheshimiwa Spika, la pili amelisema Profesa J, nimeongea na Diamond *TRA* wanampelekea anadaiwa

milioni 400, hivi ukidaiwa milioni 400 maana yake yeye mwenyewe mapato yake basi ni karibu shilingi bilioni 1.2. Sasa haya mapato kama ndio hivyo TRA wanasema yeye alipe kodi shilingi milioni 400, mapato yake ni mabilioni hayo, yamekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, vile vile vijana hawa wanahitaji kusaidiwa kwenye menejimenti. Leo Diamond katoka alikotoka, kafika pale. Hivi tunamwacha pale pale adumae au tunamwendelezaje? Yeye ameshakua sasa hivi ni kama *model* kwa wasanii wa Tanzania, *East Africa* na hata Afrika kwa ujumla. Wizara lazima iangalie namna gani inaweza kumtoa pale; na wakati mwingine siyo kwa kutoa pesa, ni kukaa nao hawa vijana na kuwasaidia katika mambo ya utawala. Kwa sababu tuna viongozi wetu wa mambo haya ya sanaa, washiriki katika kuwasaidia wasanii wetu kwa mambo ya utawala.

Mheshimiwa Spika, pia niseme, pamoja na mapenzi yangu makubwa kabisa na wanamuziki hawa na wasanii wa maigizo, bado nahimiza wasanii wetu lazima wajikite kwenye nidhamu. Nidhamu ndiyo mafanikio ya kila jambo. Haina maana ukiwa msanii ukose nidhamu. Leo wasanii wamekuwa ndio katika watu wanaoandikwa andikwa kwenye magazeti na wengine wanaamini wakifanya utovu wa nidhamu ndio majina yao yatatajwa. Mimi Mbunge wao siamini katika hilo. Naamini kwamba wafanye kazi kwa juhudi, walinde vipaji vyao, wafanye kazi kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kwamba malipo wanayoyapata hayaendani na kazi wanayoifanya. Leo wasanii wa maigizo, wanatengeneza filamu wakati mwingine kwa shilingi milioni 15, shilingi milioni 12; anakwenda kuingia mkataba shilingi milioni 20, kazi ndio imeuzwa kabisa! Maana yake hawezi hata ku-*print* tena ile kazi. Kazi ndiyo imeuzwa, imeenda kwa *Step Entertainment* au nani au nani na huyo mtu anayenunua kazi ni kikampuni kimoja tu. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, iangalie hawa watu wanaonunua kazi za wasanii na kupora kabisa kazi na kuchukua hati miliki ya kazi, lazima waangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kubwa nawaunga mkono vijana wangu, nawaandaa, tutafanya kikao na Wizara, lakini kubwa waangalie nidhamu na maadili ya Kitanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia, ni kengele ya pili.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ila jana Mheshimiwa Mtulia kabla hujakaa, hivi Simba na *African Lion* ilitoka ngapi ngapi jana. *(Kicheko)*

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Tumewachapa mbili, moja kama kawaida. Kama kawaida. Nakushukuru sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**SPIKA:** Nilikuwa sijafahamu kidogo matokeo. *(Makofi)*

Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Ali Juma. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunijaalia uzima, kuweza kusimama tena ndani ya Bunge hili Tukufu. Pia napenda kupongeza na kushukuru kwa dhati Ofisi yako kwa kuweza kuokoa maisha yangu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano waliouonyesha na nitakuwa sio mtu mwema sana nisipowashukuru Wabunge wa Mkoa wa Rukwa na Katavi kwa upendo waliouonyesha bila kujali itikadi za vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, pia naungana na wazazi, Walimu, ndugu na jamaa katika kuomboleza msiba uliotukuta juu ya

wanafunzi ambao walituacha. Tunasema kazi ya Mungu hatuwezi kuhoji, lakini tumepokea, ingawa mambo haya hayazoeleki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kuchangia mambo machache nikianza na upande wa habari. *TBC* ni *Television* ya Taifa wote tunajua, lakini inachangiwa na walipa kodi wa nchi hii wakiwepo wa Mkoa wangu wa Rukwa, leo tunapokuwa tunajadili bajeti, wanashindwa kujua wawakilishi wao wamezungumza nini? Je, wamezungumza yale waliyowaambia? Kwa sababu hawawezi kuona tena Bunge *live.*

Mheshimiwa Spika, yawezekana hata nia njema ya Serikali hasa anapokuwa anazungumza Mheshimiwa Rais kwamba watu wafanye kazi, lakini tunafahamu fika kwamba Rais anapokuwa anafanya jambo lolote anaonekana *live*. Rais huyu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichaguliwa kwa kura za Watanzania, Wabunge wamechaguliwa kwa kura za Watanzania. Sijajua utofauti mkubwa uliojitokeza hapo katikati.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri pamoja na sisi Wabunge, mimi bado linanichanganya kwenye kichwa changu. Tofauti ni nini? Ni nafasi au ni kazi kama alivyozungumza? Kwa sababu ule muda anapoonekana yeye, wananchi wanaacha kazi wanamsikiliza, basi angalau hata kipindi hiki cha bajeti sasa ili wananchi waweze kuwaona Wawakilishi wao wanafanya nini? Je, wanazungumza yale waliyowaambia wazungumze au inakuwaje? Sidhani kama itakuwa busara au uzalendo anaousema yeye aonekane, Waheshimiwa Wabunge wasionekane, wakati wote walikwenda kuomba kura na wananchi ni wale wale ambao wanatakiwa waone nini kinazungumzwa na nini kinatendeka. Sidhani kama uzalendo uko mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri labda aje atuambie kwamba pesa zinakuwa nyingi sana kuonyesha Bunge, lakini upande wa Rais na vitu vingine

pesa zinakuwa siyo nyingi. Wakati huo huo *TBC* inaweza kuonyesha mambo mengine. Napenda tupate taarifa Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* kwamba kwa mara ya mwisho ni lini taarifa za Upinzani zilionyeshwa *TBC?* Nimekuwa mfuatiliaji sana wa *TBC.* Sasa kama *TBC* imekuwa na ubaguzi, ni vyema Mheshimiwa Waziri aje kutuambia tujue. Ni lini kwa mara ya mwisho *TBC* ilionyesha habari za Upinzani, wakati wote ni Wabunge na wote ni Wawakilishi wa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili kwa upande wa habari, ni juu ya Waandishi wa habari. Pamoja na Bunge kutoonyeshwa *live,* Watanzania hawa wanategemea kupata habari kwenye vyombo mbalimbali. Leo waandishi wa habari wanakuwa na hofu ya kutoa habari. Hatujasikia tamko kutoka kwa Mheshimiwa Waziri linaloonesha moja kwa moja uzito juu ya ulinzi wa Waandishi wa Habari. Tumeangalia matukio kadhaa, achana na hayo ya huko nyuma ya akina Mwangosi na watu gani, lakini bado hatujaona jitihada za Serikali juu ya ulinzi wa Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie mikakati yake aliyoipanga juu ya Waandishi wa Habari. Wananchi hawawezi kujua chochote bila kuwaona au kuwasikiliza Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wangu wa Rukwa kuna maeneo hakuna *TV,* wanategemea kusikiliza redio. Hizo redio zenyewe sasa hivi habari haziendi kama zilivyo; sijui mpaka zichujwe wapi, zifanywejwe! Sasa haya mambo inafikia mahali yanakuwa na ukakasi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie ni mikakati gani ameiweka juu ya ulinzi wa Waandishi wa Habari pamoja na wamiliki wa vyombo vya habari? Sambamba na hilo, ile ripoti ya Mheshimiwa Nape tunataka tuisikie, kwa sababu hapa ndiyo mahali pake, aje atuambie nini kinaendelea juu ya kile kitu? Kama kuna kiini macho tujue kwamba imeshindikana, lakini imeshindikana kwa nini?

Mheshimiwa Spika, upande wa michezo, hatuwezi kuboresha michezo tukiwa hatujaboresha viwanja vya michezo. Hapa tutapiga *story* siku zote na kutafuta mchawi. Kwa sababu huwezi kusema watu waje wacheze, unategemea kwamba waje wacheze Dodoma tu; kwa sababu hawa watu wanatoka kwenye Wilaya na Mikoa. Huko kwenye Wilaya na Mikoa hali za viwanja ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, katika viwanja hivyo kuna viwanja vinamilikiwa na Chama Tawala; siyo dhambi, basi viendelezeni. Viko kwenye hali mbaya! Shida ni nini? Yawezekana bado hakujawa na mikakati thabiti kwa sababu hatutegemei kuangalia *Serengeti boys* wale wale wakae miaka 20, tunataka mikakati ya wale ambao wanaandaliwa sasa kuja kuwa *Serengeti Boys* wa mwaka 2020. Hawa watu wanapatikana wapi? Wanapatikana kwenye Wilaya na Mikoa. Ni utaratibu gani umewekwa ambao utakuwa rafiki kwa hawa vijana wanaotoka kwenye mikoa na wilaya?

Mheshimiwa Spika, siamini kwamba Mkoa wangu hakuna wachezaji wazuri. Mkoa wa Rukwa wanakula samaki, kuna watu wanacheza vizuri sana. Ni lini utawajua? Utawajua kwa kufuata ule utaratibu uliokuwepo zamani. Kulikuwa na michujo inafanyika shule za msingi na sekondari. Nakumbuka kwa mara mwisho UMITASHUMTA pamoja na UMISETA wakiwa wanakwenda Geita nafikiri, ilitokea tamko hawarudi wale watoto. Tunaomba mtuambie sasa, hiki kitu ndiyo kimefutwa moja kwa moja au kuna mikakati gani inaandaliwa juu ya suala hili? Maana imeshakuwa sasa hatuelewi, tupo tu.

Mheshimiwa Spika, siamini kama wachezaji wengi wanatoka Dar es Salaam na Mwanza tu; na Mikoa mingine wachezaji wapo. Wekeni mikakati, wekeni mazingira rafiki ya kuwapata wachezaji wazuri na wapo, wanapatikana maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, vile vile tusiwekeze kwenye mpira peke yake. Kama tumeshindwa kwenye mpira, lazima tuwe

na *plan B.* Tutafute mchezo mwingine ambao hatutaitwa shamba la bibi Tanzania, haiwezekani! Naamini vipaji vipo vingi tu, lakini ni namna ya kupata hivyo vipaji na kuvifuata kule viliko. Kwa hiyo, kumekuwa na shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa limekuwa likizungumzwa sana. Siamini kwamba mpaka leo tumeshindwa kupata vazi la Taifa. Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho atuambie, maana nimeona huku pembeni nyuma ya hiki kitabu, lakini haijaonesha kwamba ndiyo hili, sijui! Nafikiri ndiyo utaratibu unaandaliwa. Muda umekuwa mrefu, mpaka lini kwa mwendo huu unaokwenda? Kama ndiyo hili limepitishwa, basi mtuambie lilivyopitishwa.

Mheshimiwa Spika, hiki kitu inatokea, hata ukiangalia kwenye muziki, watu wengi hasa wanawake unakuta mavazi wanayovaa pale ni tofauti na wanaume, wao watavaa suti nzuri na tai safi kabisa, lakini wanawake wanavaa vibaya! Leo mtawaambia nini wakati hakuna vazi lililoteuliwa? Tunaomba mtakapokuja, tena Mheshimiwa Naibu Waziri,yeye ni mwanamke, kwa sababu inapotokea kudhalilishwa, hawadhalilishwi wale walioko pale na wanawake wengine wote wanaozunguka kwenye jamii hizi tunapata aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, lilizungumzwa sana siku ya Ijumaa suala la Mwenge. Naomba Mheshimiwa Waziri aje anipe ufafanuzi kidogo. Kwenye Mkoa wangu wa Rukwa Wenyeviti wamekamatwa kwa kutochangisha pesa za Mwenge. Naomba kujua, ni sheria ipi ilitumika kuwakamata Wenyeviti hawa kwa kutochangisha pesa za Mwenge? Kwa sababu kitu kinachoitwa mchango kwa mimi ninavyoelewa, ni hiari siyo lazima. Sasa ni sheria ipi ilitumika kuwakamata Wenyeviti hao wa Serikali ambao hata mshahara hawalipwi; na kila siku tunajadili hapa, hakuna siku imepitishwa Wenyeviti wataanza kulipwa mshahara au posho. Sasa ni sheria gani ilitumika kuwakamata Wenyeviti hawa? Naomba kauli ya Serikali Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kichwa changu bado hakijakaa vizuri. Ahsante kwa nafasi uliyonipa kutoa mchango huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Aida Khenani. Mheshimiwa Juma Ali Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay. Mheshimiwa Juma, hayupo. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami niungane na wenzangu wote ambao wametoa pole kwa wafiwa wote na kweli Mungu azilaze roho za Marehemu watoto wetu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe pongezi zangu kubwa sana kwa Mheshimiwa George Huruma Mkuchika ambaye alikuwa *DC* katika Wilaya yangu ambayo mimi nilikuwa mdogo sana kwa kujenga uwanja wa michezo, ambao umefanya mimi kama Flatei Massay kuwa mwanamichezo kutokana na viwanja ambavyo huyu mzee wetu ambaye ni Mbunge humu ndani ameifanya kazi hiyo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini naamua kusema haya? Nasema haya kwa sababu kuna watu wanatakiwa kuenziwa katika Taifa letu. Kwanza, wamefanya kazi nzuri, uwanja wa Julius Nyerere ulioko Mbulu umejengwa kwa nguvu kazi ya kwake mwenyewe. Namkumbuka alikuja mimi nikiwa mtoto sana, nina miaka kama sikosei mitano. Nilikuwa naona jinsi akivaa magwanda yake ya kijeshi akiwa *Captain* na kuhamasisha wananchi wa Mbulu kujenga ule uwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa uwanja umekuwa mzuri na naamini wachezaji wengi wametokea pale na wana riadha wengi wametoka pale. Sasa niiombe Wizara iangalie namna gani ya kuweza kusaidia viwanja hivi vya michezo? Kwa sababu wanariadha wengi ambao kimsingi wameonekana katika Taifa letu kuleta zawadi ya ushindi katika medali za Kimataifa wametokea pale, mfano, Filbert Bayi, John Stephen

Akhwari, John Bayo, hawa watu wote wamefanya kazi na kulitangaza Taifa hili katika ulimwengu huu wa Michezo na wameweka rekodi ambayo mpaka sasa naamini haijavunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara iangalie sana uwanja ule, hata ikiwezekana basi waangalie namna ya kusaidia hata kwa kutumia maeneo ya ushauri tu nini kifanyike ili angalau michezo iweze kuendelea katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kusemea hawa wazee wetu waliotusaidia sana kuitangaza Tanzania. John Stephen Akhwari, kwanza namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, alifika akamtembelea mzee yule. Ana vikombe kama 15, Mheshimiwa Naibu Waziri aliona mwenyewe. Kwa sababu alifika, yule babu sasa anazeeka na hawezi kuishi miaka mingi kutokana na umri wake sasa. Naamini historia yake inaonekana na Mheshimiwa Waziri anayo. Hebu angalieni basi namna ya kuangalia malalamiko yake ambayo alimpa Mheshimiwa Waziri. Mimi ni Mbunge wake lazima nimwambie leo. Asingeweza kupata nafasi yoyote, nafasi ya kumsaidia ni wakati huu akiwa hai.

Mheshimiwa Spika, wakati ule walikuwa wanawasikiliza Taifa, ilikuwa ni ngumu sana kupata zile hela ambazo wanatunzwa wanaposhinda katika zile medali ambazo zimeisaidia nchi hii kusifika wakati huo. Kwa kweli walikuwa wanasaidia Tanzania na kuipatia heshima kama nchi. Hawakuwa wanapata jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, sasa basi waje wasaidie kwa sababu wamekuja wale watu wa *olympic* kutoka nchi ya Australia ikitaka kumjengea huyu baba au babu uwanja wa michezo, lakini kwa sharti moja tu, ni kwa jina lake. Kwa bahati mbaya sana Serikali wakati uliopita haikukubali kabisa jina la uwanja huo kuitwa kwa jina lake. Wale wafadhili wamekuwa kila siku wakijaribu kutafuta namna rahisi ya

kufanya muunganiko kati ya Serikali yao na sisi ili kumsaidia kumjengea mzee huyu ambaye ametangaza Tanzania katika ulimwengu huu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, basi naomba Serikali ione namna gani ya kusaidia. Nafiri Mheshimiwa Naibu Waziri siku ile mzee yule alimwambia masikitiko yake makubwa. Sasa kabla hajafika mahali Mungu akamchukua kwa sababu ni mzee, waje basi wamsaidie haraka ili angalau jina lile lisifutike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niliseme, Mbulu tumetoa wanamichezo wengi wa Kimataifa, siyo kwa sababu tu ni maarufu sana, hapana! Ni kwa sababu ya *nature* ya eneo lenyewe. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, sasa hivi wanamichezo wengi hasa wanariadha kutoka Mbulu wanachukuliwa maeneo mengi mengi na watu hufadhili mmoja mmoja. Sasa naomba Wizara ijaribu kufanya jambo moja tu, isiondoe sasa eneo la michezo ya mazoezi kutoka Mbulu kuipeleka Dar es Salaam. Kwa sababu sasa mnavyofanya namna hiyo saa hizi, historia inaweza kufutika kwa sababu moja tu.

Mheshimiwa Spika, ukimtoa mtu Mbulu kwenye kitu kinachoitwa uwanda wa juu, sisi kule bahati nzuri hali ya hewa inatu-*favour* na milima inawasaidia wachezaji. Sasa ukimtoa mchezaji toka Mbulu ukamfanyia kambi Dar es Salaam ili aende kushinda, anashindwa kushinda kwa sababu ya mvuto anaotumia, upepo ule au hewa ya Dar es Salaam iko *zero degree* wakati huku Mbulu kuna 1,500. Sasa ukimtoa pale akafanye mazoezi Dar es Salaam akienda Ulaya, hawezi kushinda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sababu hizo nafikiri ni za kitaalam sana; mimi sio Daktari lakini naziona na ninazijua. Kwa hiyo, wasaidie basi kuliko Chama kile cha riadha kiamue moja kwa moja kwa sababu wao ndio viongozi waamue kambi kufanyika Dar es Salaam, wanaweza kufanya hivyo kwa sababu wao ni viogozi, lakini waone, Filbert Bayi wakati

huo walikuwa wanafanya mazoezi na kufanyia pale Mbulu na wakashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii basi, walishinda kutoka na hali ya hewa iliyoko pale na *nature* ya mazingira ya kule ni milima na miinuko, ili akifika kule aweze kumaliza zile mbio akiwa na nguvu na kuisaidia nchi yetu tupate medali. Nimeona niseme hii moja kwa moja hapa kama mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nielezee sasa eneo la michezo. Michezo ni lazima uanzie ukiwa mdogo. Wenzetu ukiangalia historia ya michezo kwa sisi wanamichezo utaona watoto wetu wanafundishwa wakiwa watoto. Nami niungane na wenzangu kwa msingi huo ni vizuri kumfundisha mtoto akiwa mdogo akafahamu na kumjengea ile *behavior* akaweza akafanya michezo akiwa utotoni. Leo hii ukimfundisha punda mzee kulima, hawezi. Ni lazima basi hii michezo irudishwe shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, linguine, liko jambo ambalo nataka niseme kwenye sanaa na hasa Bodi ya Filamu. Bodi ya Filamu ina harufu ya rushwa. Naomba nirudie, ina harufu ya rushwa kwa sababu kwa sisi wasanii, nami nataka nikwambie, mimi ni msanii, lakini ukitaka kuomba chochote kwenye Bodi ya Filamu, wanaweka hali ambayo haimruhusu msanii kupata anachotaka. Kwa mfano, mpaka Bodi ikae unahitaji miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kufanya *inter-connection* wewe msanii wa Tanzania na Msanii aliyeko Ulaya, akija Tanzania inabidi aache kabisa kila kitu, anatakiwa asije na *camera.* Nashangaa sana, unamruhusu asije na *camera* wakati huo unamkubalia aingie na simu, sasa kama ni usalama wa nchi, sijui inawezekana. Simu nyingine zina *capacity* kubwa. Kama ukitaka asichukue hiyo picha, ataweza hata kutumia simu, si atachukua tu!

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, nimepeleka malalamiko katika Ofisi yake na nimeandika

mwenyewe. Walikuja Wabunge kutoka nchini Norway, ni wafadhili wa miradi mingi nchini, lakini Bodi ya Filamu ikawazuia wale Wabunge wasiingie na *camera* jambo ambalo nililishangaa sana, likanifanya nipate mshtuko kwa sababu wale Wabunge walipoingia, walikuja wakiwa watupu wakisema, kwa nini hatukupewa?

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri walifuata sheria za Tanzania, wamefuata sheria za mambo ya nchi za nje, wamefika Wizarani, wameandika, wametumia Ubalozi wa Norway, wametumia Ubalozi wetu ulioko Sweden, wameruhusiwa; wamekuja kwenye Wizara yako, wameomba kibali. Kilichowafanya wakatazwe wasipate kibali hicho ni Bodi ya Filamu. Wameomba, muda unatosha na bahati mbaya hawakupata majibu. Kwa nini hawakupata kibali cha kuingia na *camera?* Hiyo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye Bodi ya Filamu kuna shida pale; nami na-*declare* ninao ushahidi na nimempa kwa maandishi na nimesema kwa maandishi na Balozi pia amenipa barua yake kwa maandishi na nimempa *copy* yake. Naomba akachunguze Bodi ya Filamu, kuna shida pale. Bahati nzuri nimekwenda mwenyewe pale, ni mara tatu nimeshindwa kupata ninayotaka kuyafanya. Mara moja tu Mheshimiwa Nape alipokuwa Waziri alipiga simu ndiyo nikasaidiwa kwa sababu tu mimi ni Mbunge. Je, wasanii wangapi wana shida pale? Aangalie Bodi hii, kwa nini inatoa masharti magumu? Kama ni shida, tujue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nilisemee vizuri hili na nilisemee kwa uchungu mkubwa kwa sababu tunapoteza heshima. Anapokuja mtu anayefadhili nchi hii, lakini inafika mahali anakwamishwa kwa jambo dogo tu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Massay ni kengele ya pili.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja, lakini naomba kama hataleta majibu haya, nitashika shilingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Flatei. Niseme tu kwamba, Wabunge wanaotoka nchi nyingine, hata kama ni wageni wenu, ni wageni wangu pia. Sasa iweje Wabunge wa nchi nyingine wakwame Spika wala hana habari? Eti kubeba *camera* tu! Ina maana hawa Wabunge wamekuja kuchukua filamu hapa? *What happened*? Tunahitaji kujua zaidi kuhusu mambo ya namna hiyo ili tuyaweke sawa.

Sina hakika kama Mheshimiwa Leonidas Gama yuko humu ndani! Hayupo eeh! Naona ametoka kidogo. Mheshimiwa Norman Sigalla. Pia hatumwoni eeh!

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** *Ok*! Ooh, uko karibu hapa. Karibu sana Mheshimiwa Norman Sigalla atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuungana na wenzangu kutoa pole kwa ajili ya msiba mkubwa ambao Taifa letu limepata na bila shaka Mungu atawatunza watoto hawa maana ni wenye haki mbele zake.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwenye eneo la timu yetu ya Taifa. Mwaka 1985/1986 mimi ni mmoja wa wachezaji walioitwa kwenye Timu ya Taifa ya vijana. Wakati huo tulikuwa tunafundishwa na kaka yetu Joel Bendera, sifa ya kujiunga na timu hizo ilikuwa ni ubora wa wachezaji hao waliotafutwa Sekondari na kwingineko, maadam umri wao ulikuwa chini ya miaka 24.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watu wengi wanapoongelea timu ya Taifa, wanaongelea kana kwamba tatizo kubwa la Timu ya Taifa kufanya vibaya ni kwa sababu

hakuna timu za watoto wadogo. Ni tabia yetu kutokukumbuka historia ya mafanikio yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Waziri afahamu kwamba ili ufanye vizuri, cha kwanza ni wachezaji bora, lakini cha pili ni Mwalimu mwenye weledi. Nijikite hapo kidogo. Timu yetu ya Taifa kwa miaka nane mfululizo imekuwa ikifundishwa na kocha ambaye kwenye timu yake binafsi, yaani klabu yake hajawahi chukua ubingwa. Yaani kocha kwenye timu yake anakuwa katika tano za mwisho, lakini anapewa Timu ya Taifa ili ishinde, *it is impossible!* Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kocha mzawa afundishe Timu ya Taifa ni lazima uchukue *the best coach.* Unampataje? Aliyefanya vizuri kwenye ligi! Sasa kocha amepewa timu, ameshika nafasi ya mwisho au tano mwishoni kwa miaka karibu nane, tisa, kumi; bado kwa sababu ya vyeti vizuri tu, ndiye awe kocha wa Timu ya Taifa; haiwezekani kushinda.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu wa timu ya mpira wa miguu kama ni mzawa ni lazima achukuliwe katika makocha waliofanya vizuri na ndiyo maana ni maoni yangu kwamba kijana wetu Mecky Mexime pamoja na kwamba ni kijana mdogo, lakini *as of now,* ndiye kocha mzawa ambaye kwa miaka minne, mitano mfululizo timu alizoshika amefanya vizuri. Yanga au Simba akichukua ubingwa, anachukua ubingwa akiwa na *foreign coach,* lakini kocha mzawa anakuwa yeye. Hata akishika utatu, lakini *that is the best coach.*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba ni muhimu sana unapo-*dedicate team* kwa Mwalimu, ni lazima awe ni Mwalimu mwenye *good performance.* Bahati mbaya sana siyo wakati wote vyeti vinaashiria uwezo na hasa unapoongelea kupima mpira, siyo wakati wote.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu niongelee kidogo viwanja vya mpira. Wizara inayosimamia michezo ni vizuri sana ishirikiane na Wizara ya TAMISEMI ili kuona ni jinsi gani

wanaweza wakaboresha viwanja vyetu hasa vya shule za sekondari na msingi.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Majimbo yetu na Tanzania nzima ni viwanja vichache sana vya shule za sekondari au msingi ambavyo vina vipimo vizuri na ambavyo *level* yake unasema atapatikana hapa mchezaji mzuri. Viwanja vingi ni vibovu, kwa hiyo, havitoi tafsiri ya kwamba watoto wanaoandaliwa katika viwanja hivi, watakuwa ni wachezaji bora.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana viwanja vyetu angalau viwe na *level* ile inayoonesha kwamba watoto wetu watajifunza mpira; na vile vipimo pia vifanane na huko wanakokwenda. Hili likifanyika kwa ushirikiano wa TAMISEMI pamoja na Wizara inayosimamia michezo, itasaidia sana kupika wachezaji ambao ni wazuri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, unaweza ukakumbuka kwamba wakati amekuja kocha Maximo, yule wa Brazil, moja ya vitu ambavyo vilimsaidia yeye kufanya vizuri ni kwa sababu alipewa ushirikiano mkubwa na Serikali; malipo mazuri. Ndiyo wakati pekee ambapo wachezaji walijifunza hata kulala kwenye hoteli za kitalii au hoteli kubwa kama *Golden Tulip* kwa mwezi, miezi miwili au mitatu. Hamasa hiyo ilitosha timu hiyo kuipa nafasi ya kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, ombi langu; ni muhimu sana Wizara ikishakabidhi timu kwa kocha mzawa, vile vile *facilities* ikiwa ni pamoja na malipo kwa kocha huyo yafanane na makocha wa kigeni ambao tunawaenzi. Mbona inawezekana kuwalipa makocha wa kigeni fedha nyingi? Tunashindwa nini kufanya hivyo hivyo kwa makocha wanapokuwa sio wa kigeni? Hili likifanyika itakuwa muhimu kutia ubani na kutia nguvu kwa makocha wetu kuweza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa nichukue muda mrefu kwenye hili. Nisisitize tu kwamba Timu yetu ya Taifa na michezo kwa ujumla ndiyo heshima yetu. Bahati mbaya sana

mchezo unaopewa heshima kila wakati ni mpira wa miguu. Naomba sana, Wizara ipeleke nguvu pia kwenye michezo mingine. Iko michezo mingine kama michezo ya ngumi ambayo wengine tunaicheza, ni rahisi kufanikiwa kwa sababu michezo yote ambayo inajali uwezo wa mtu binafsi ndiyo michezo rahisi kushinda.

Mheshimiwa Spika, wewe ni mwanamichezo, unafahamu. Mpira wa miguu ndiyo mpira mgumu zaidi katika michezo kwa sababu akikosea mtu mmoja mnafungwa wote. Anakosea mtu mmoja, mnafungwa wote hata kama mmecheza vizuri, lakini mtu mmoja akizembea tu mnahesabika Tanzania mmefungwa; lakini ngumi, ukikosea wewe, unapigwa wewe. Ndiyo michezo mepesi kufundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michezo kama *table tennis,* kwa maana ya *singles,* ni rahisi! *Table tennis* ni rahisi, *long tennis* ni rahisi maana ukikosea wewe unafungwa wewe na ndiyo rahisi kufanikiwa na kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nisije nikaketi bila kukumbuka kuipongeza timu ya Taifa zima kwa jina la *Simba Sports Club* kwa kazi kubwa ambayo wanafanya ya kufanikiwa kucheza michezo ya Kimataifa kila wanapowakilisha nchi yetu, wamekuwa wakituwakilisha vizuri na hawajawahi kutuangusha. *(Makofi)*

Mungu ibariki *Simba Sports Club* na Mungu wabariki wanamichezo wote. Ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla. *(Kicheko)*

Nilikuwa nimemwahidi Mheshimiwa Saed Kubenea na atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Mwassa. Mheshimiwa Kubenea, tafadhali.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie mjadala huu.

Kwanza kwa niaba ya Waandishi wa Habari wenzangu, wamiliki wa vyombo vya habari, Wahariri na wadau wote wa habari, natoa pole kwa msiba mkubwa uliolikumba Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, napenda nizungumzie suala la uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam. Uwanja wa Taifa umekabidhiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano. Uwanja ule umejengwa kwa dola za Kimarekani milioni 50. Ni uwanja wa tatu kwa ukubwa katika Bara la Afrika, lakini uwanja wa Taifa umekabidhiwa ukiwa haujakamilika. Kwenye eneo la jukwaa kuu ambalo linaitwa *VIP,* ikinyesha mvua watu wote waliokuwepo pale wanaloa kana kwamba umesimama kwenye mnazi. Ushahidi ni mvua hii inayonyesha Dar es Salaam sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo ni kwamba mkandarasi alitakiwa ajenge ule uwanja kwa kuweka paa maalum ambalo litakuwa linafunga na kufungua ili wakati wa mvua lile paa liweze kutumika kuzuia mvua isinyeshee. Sasa uwanja umekabidhiwa, sherehe zimefanyika bila eneo hilo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo hilo, ulikuwepo mfumo wa ukusanyaji mapato na uwanja ulikabidhiwa bila mfumo huo kukamilika, lakini Serikali hii ya sasa hivi ikafuatilia utaratibu huo na ikaona kwamba ule mfumo unaweza ukawekwa na wajenzi na umewekwa na tumeokoa zaidi ya shilingi milioni 900 bila fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa nini usifanyike utaratibu mzuri, waliojenga uwanja ule wakaukamilisha tukaendelea na shughuli zetu bila mgogoro? Inawezekana kwamba ama waliopewa mamlaka ya kusimamia uwanja hawakuwa na uwezo wa kusimamia uwanja ule vizuri wakati wa ujenzi ama walihongwa ili uwanja ule usikamilike vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hatuna sababu ya kufukua makaburi, lakini ni muhimu Uwanja wa Taifa ukaangaliwa vizuri kwa sababu watazamaji au watu wanaofika uwanja

wa Taifa wanaloa mvua na ushahidi wa mechi ya juzi kati ya Simba na Azam watu wote waliokuwepo pale uwanjani waliloa kama vile wamesimama kwenye mnazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala hapa ambalo Mheshimiwa Waziri wakati anazungumza sikuwepo, lakini nimesoma vyombo vya habari. Gazeti la Habari Leo limesema Mheshimiwa Waziri amesema Waandishi wa Habari asilimia 90 hawana sifa. Sasa najiuliza, sijui utafiti gani ambao Mheshimiwa Waziri ameufanya kwamba asilimia 90 ya Waandishi wa Habari waliopo hawana sifa na sijui sifa ambayo Mheshimiwa Waziri anaizungumzia ni ipi? Kwa sababu wapo Waandishi wa Habari ambao wamepata mafunzo mazuri kwenye vyombo vya habari na wao leo wamekuwa Waandishi wa Habari, wanafanya kazi na wanaongoza vyombo vya habari.

Mheshimwa Spika, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe, Mwandishi wa Habari, anafahamu hili. Alipomaliza masomo yake ya Kidato cha Sita alikwenda kufanya kazi kwenye chombo cha habari. Wakati huo au mpaka sasa sina hakika, ila nahisi mpaka sasa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe hajawahi kusomea Uandishi wa Habari. Kama nakosea, Waziri wangu, kaka yangu atanikosoa, lakini ndivyo ninavyofahamu mimi.

Mheshimiwa Spika, elimu peke yake haitoshi kuwa na Waandishi wa Habari wazuri na mzungumzaji aliyepita hapa alizungumzia mambo ya ukocha kwamba kuwa na vyeti tu hakumfanyi mtu awe kocha mzuri. Kwa hiyo, ni vizuri kauli kama hizi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, sikukatishi lakini nia yangu ni kukupongeza tu. Hii habari ya vyeti tu halafu mkija hapa, ooh Bashite, Bashite!

Mheshimiwa Kubenea endelea tu. *(Makofi)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninachotaka kusema ni kwamba tunaweza

tukazungumzia vyeti na hatukatai vyeti, lakini tunachozungumzia, misingi, uadilifu, uaminifu mzuri wa mtu, elimu peke yake haitoshi. Ni lazima tujenge Waandishi wa Habari. Sasa kauli hizi zinaweza zikachukuliwa na Waandishi wa Habari na zimetolewa na Waziri mwenye dhamana ya tasnia ya habari ambaye anapaswa kwa vyovyote vile kulinda Waandishi wa Habari kwa gharama yoyote ile, sio kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hapa la Waandishi wa Habari kufanya kazi katika mazingira magumu sana. Waandishi wa Habari wanatishwa, hawako huru, wanaminywa na sheria nyingi mbaya ambazo zinaminya uhuru na haki ya Waandishi wa Habari kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano hai ni huo ambao wewe umeuchukulia wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye aliingia kwenye chumba cha habari akalazimisha habari itoke. Ripoti imeandaliwa na Mheshimiwa Nape, Kamati ya Mheshimiwa Nape iliyoundwa na Mheshimiwa Nape inaongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari, Maelezo, ni *Doctor,* ni Mwanasheria, ni Mhariri, amefanya kazi Mashirika ya Kimataifa. Haiwezekani mtu wa namna hii akafanya kazi bila weledi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeongozwa na Jesse Kwayu, Mhariri wa magazeti mengi nchi hii amepitia. Amekuwa kwenye *media* zaidi ya miaka 20; kizazi kingi hapa cha Uandishi wa Habari amekifundisha. Haiwezekani Jesse Kwayu akafanya kazi chafu isiyo na weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa aliitwa kwenye Kamati; akakataa, Kamati ilitaka kutoa ripoti kesho yake, ikasitisha ili imhoji Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa akakimbia Kamati. Uandishi wa Habari unaelekeza, tafuta *source,* akikosekana unasema. Huwezi kuua *story* kwa sababu mtu amekosekana. Makonda ameikimbia mwenyewe Kamati. Mheshimiwa Waziri anasema hawezi kutumia Ripoti ya Kamati ambayo haina weledi.

Mheshimiwa Spika, mimi sina ugomvi na Dkt. Mwakyembe, akikataa kutumia ripoti, huo ni utashi wake, lakini nina ugomvi naye anapochanachana na kuikosoa hii ripoti. Akatae kutumia, aseme sitaki, basi! Asibeze kazi ya kitume iliyofanywa na Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imefanya kazi ya kitume. Serikali hii ambayo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anaongoza, haikuhoji watu ambao walikuwa na vyeti feki. Wanalalamika, lakini ripoti ya vyeti feki imetolewa hadharani. Magazeti yameagizwa yaandike hiyo ripoti na magazeti hayo yamechapisha hadharani. Waziri wa Habari anayekataa ripoti ambayo haikusikiliza watu, ameruhusu magazeti anayoyaongoza yachapishe ripoti ambayo upande wa pili haukusikilizwa. Hii ni *double standard.* Kama tunataka kuongoza Taifa hili, ni vizuri tukafanya kazi bila kuonea watu.

Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, kidogo tu, kwani hiyo ripoti imeshakuwa *published?*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, ipi?

**SPIKA:** Hiyo ripoti unayoiongelea, imeshatangazwa kwa umma au bado haijatoka?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, majina yote elfu tisa mia tisa na ngapi...

**SPIKA:** Nina maana ya ripoti ile ya habari uliyokuwa unaizungumzia.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, haijatangazwa.

**SPIKA:** Aaah, nilikuwa nashangaa tu sasa unajuaje weledi wa hiyo ripoti...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Tume imetangazwa.

**SPIKA:** Nilidhani Mhshimiwa Waziri ndio anaweza akajua *content* ya hiyo ripoti na kui-*measure.* Kwa sisi ambao hatujapata tayari, lakini endelea tu kuchangia.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nime-*note* ulichoongea. Nasisitiza kwamba nchi inaendeshwa kwa misingi ya haki. Hatuwezi kuwa upande huu, jambo tunalikubali tunalifuata, upande huu...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko upande gani?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hapa, Mlinga!

**SPIKA:** Aaah, Mheshimiwa Mlinga Goodluck.

**T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Kubenea na Bunge zima kuwa gazeti linalomilikiwa na mwongeaji mwenyewe limechapa majina feki ya wenye vyeti feki ambayo yeye analalamika hawajasikilizwa. Limechapa na limeweka hadharani.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa hiyo na kwamba gazeti kwa mujibu wa

mhariri alifuata kuchapisha kwa sababu Rais aliagiza majina yale yachapishwe kwenye magazeti. Kwa hiyo, asingeonekana mzalendo kama angekataa kufanya kazi hiyo, naye amekuwa mzalendo amechapa, lakini haituzuii sisi kukosoa utaratibu uliotumika. Nami sio Mhariri wa hilo gazeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Mkataba wa *TBC* na Kampuni ya Kichina. Jambo hili limezungumzwa hapa Bungeni mara kadhaa, tumeliandika kwenye vyombo vya habari kwamba mkataba kati ya *TBC* na Kampuni ya Kichina ni wa kinyonyaji. Mheshimiwa Waziri wa habari aliyetangulia kabla ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, aliahidi mbele ya Bunge hili kwenye mkutano uliopita kwamba ripoti ile itakuwa hadharani na Serikali itaiangalia upya suala zima la mkataba wa *TBC* na Kampuni ile ya Kichina. Nataka Mheshimiwa Waziri wakati anajibu atueleze mkataba kati ya *TBC* na Kampuni ya Kichina umefikia wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea ni kengele ya pili.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, muda wangu uliuchukua, naomba nimalizie. Uliniingilia sana na Mheshimiwa Goodluck. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, Makatibu wananiambia kabisa kwa uhakika kwamba wamelinda sana muda wako.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mambo haya kidogo tabu! Cheti upeleke mwenyewe kwa mkono wako, kionekane feki, halafu utake tena ushirikishwe. Sasa sijui ushirikishwe nini pale.

Mheshimiwa Salma Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa masikitiko makubwa sana niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa msiba huu tulioupata wa kupoteza watoto wetu hawa ambao walikuwa na ndoto kubwa za kulipeleka Taifa letu mbele. Wanafunzi 32 ni msiba mkubwa mno, hilo darasa sijui watakuwa wamebaki wanafunzi wangapi na mtihani wao wa kitaifa utakuwaje. Kwa hiyo, nahuzunika sana kwa msiba huu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kuchangia Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa nichangie kuhusu kulinda utamaduni wa Taifa letu. Katika kulinda utamaduni wa Taifa letu kuna mambo mengi ya kuangalia kama uvaaji wetu na mengine mengi. Kuna tabia ya uvaaji wa nusu uchi hasa kwa jinsia ya kike, wanawake wengi wanavaa uchi yaani nusu uchi kabisa. Ukiangalia maigizo unakuta wanaume wamevaa vizuri kabisa lakini wanawake wapo nusu uchi. Sijui Serikali ina mpango gani katika suala hili au hamlioni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mashindano ya *Miss Tanzania*, hivi ni lazima uwe uchi ndiyo ushinde *Miss Tanzania*? Kwa kiwango kikubwa ukiwaangalia Ma-*miss* wanavaa nusu uchi kabisa na hiyo nafikiri ndiyo imeleta ugumu hata kumchangia yule *Miss Tanzania* aliyekuja hapa watu wanaona kwamba hii tasnia ni kama ya kuaibisha fulani yaani siyo utamaduni wetu kama Waafrika au Watanzania, mwanamke uvae uchi. Unakuta kabisa nguo zao asilimia 80 ya mwili wake uko uchi amevaa sehemu ndogo tu. Mimi niulize ni nini hasa kinachofanya iwe hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi mtu huwezi kuwa *covered* kabisa kwenye vazi lako la kibantu ukawa *Miss Tanzania*? Hata ukienda huko kwenye mashindano ya *Miss World* ukivaa *full* itajulikana kabisa hivi ndivyo Watanzania wanavyovaa, lakini ukiangalia *modern culture* unavaa nusu uchi unaenda huko *worldwide* unavaa *totally* uchi, Watanzania huwa

hatuvai uchi na hatuna kabila lolote ambalo linalovaa vazi lake uchi, sasa sielewi utamaduni huu wa kuvaa uchi umetoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye maigizo wanaume wamevaa lakini wanawake wako uchi, nusu uchi. Hata kwenye sanaa mbalimbali iko hivyo yaani mwanamke kuwa uchi imeonekana kama ni kivutio, hilo silikubali kabisa. Mheshimiwa Waziri anavyokuja kihitimisha hapa atueleze ana mpango gani na huu uvaaji wa nusu uchi kwa wanawake? Maana inaonekana mwanamke kuvaa uchi ni kivutio, akiwa *covered* ...

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma ukae chini kidogo upokee taarifa kwa makini.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, sijui ni Kiswahili kigumu au laa mimi ni Mngoni sijui Kiswahili naomba anifafanulie kidogo. Amelitaja sana neno kuvaa uchi, kuvaa uchi, sasa sijui anamaanisha nini au kuvaa nusu uchi au anamaanisha nini anasema tu kuvaa uchi, kuvaa uchi. Ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa Jacqueline hata mimi nimepata tabu sana hapa, maana umevaa halafu tena uchi sasa, Mheshimiwa Mwassa hebu tuwekee vizuri Kiswahili wewe unatoka Pwani bwana. *(Kicheko)*

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri huyo mtani wangu Mngoni naye haelewi Kiswahili vilevile, kwanza hawa siyo Watanzania. Wangoni toka lini wakawa Watanzania hawa wametoka South Africa tumewapokea tu, kwanza hapa wakae kwa *passport* na muwe na *permit* kabisa Wangoni toka lini mkawa Watanzania nyie. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Unaipokea Taarifa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa hiyo. Namaanisha kuvaa nguo nusu uchi, simaanishi uchi, kwa maana baadhi ya sehemu *sensitive* za mwili wa mwanamke zinakuwa uchi, ndiyo ninachomaanisha siyo kwamba ni kuvaa nusu uchi, asilimia 80 watu wanakuwa uchi.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Jamani namlinda msemaji, endelea Mheshimiwa Mwassa. *(Makofi)*

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika, pia napenda kuongelea suala la waandishi kuwekewa mazingira magumu au kuvamiwa wanapofanya kazi zao. Waandishi wa habari mara nyingi wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao hasa kwenye mikutano ya vyama vya upinzani wanakuwa wakivamiwa, wanakuwa hawana uhuru kabisa wa kuandika zile habari au vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tukio lililotokea *Vina Hotel Dar es Salaam,* waandishi wamevamiwa, wamepigwa mpaka sasa hivi hatujui ripoti imekaaje, lakini mimi nasema kwamba Serikali iwalinde waandishi wanapotekeleza majukumu yao. Waandishi ni kioo cha jamii, wanatakiwa waandike habari zote kutuhabarisha umma aidha habari za vyama vya upinzani au chama tawala wawe huru kote. Sasa hivi inavyoonekana wanapata hofu sana kuja hata kwenye mikutano ya vyama vya upinzani kwa sababu mara nyingi wanavamiwa lakini haionekani kama suala hili linachukuliwa *in a sensitive way.* Kwa hiyo, niombe Serikali iwalinde waandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, vilevile niende kwenye Vazi la Taifa, ukiangalia tuna Wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa lakini hatuna Vazi la Taifa, kwa nini? Lazima tuwe na Vazi la Taifa, tujivunie utaifa wetu kama Tanzania, lakini miaka kama

mitano iliyopita Vazi la Taifa linaongelewa, sasa Waziri atuambie kabisa hapa taratibu za utafutaji wa Vazi la Taifa imeishia wapi au kikwazo ni nini. Naomba Waziri atueleze wazi Vazi la Taifa tunalipata lini hapa Tanzania ili na sisi tuwe na Vazi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile niongelee suala la uchakavu wa mitambo *TBC*. Kwenye hotuba ya Waziri ameeleza kabisa kwamba amewatengea bajeti ya maendeleo ya shilingi bilioni moja kuhusu usikivu wa *TBC,* lakini nimtaarifa Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti hiyo haifai kitu kabisa kwani *TBC* ina mitambo chakavu hamna mfano. *TBC* ni mtoto wa Serikali na kama ni mtoto wako usimfanye wa kufikia, mbona hana *competition* na vyombo vingine vya habari. Mitambo yote ni chakavu, haisikiki sehemu nyingi kwa mfano ukiangalia wilaya za vijijini huko kwa mtani wangu Mngoni huko Ruvuma kote haisikiki, aseme hapa kama inasikika, hakuna, Ruvuma na sehemu nyingine kote haisikiki kutokana na uchakavu wa mitambo.

Mheshimiwa Spika, ninachomshauri Waziri aendelee kutafuta pesa, hiyo bajeti ya shilingi bilioni moja ni ndogo hawawezi kufanya kitu chochote pale kwa sababu mitambo yao ni chakavu kabisa. Nashauri muwatengenezee mitambo ile ili kionekane kweli ni chombo cha Taifa. Hata wafanyakazi maana sasa hivi wafanyakazi wenyewe wa *TBC* wanaona aibu hata kujitambulisha wao ni wafanyakazi wa *TBC* kutokana na watu wasivyoipenda kwa sababu ya kutosikika vizuri. Kwa hiyo, kama huyu ni mtoto wa Serikali inabidi aendelezwe vizuri, Waziri atafute pesa kwani hii shilingi bilioni moja haitoshi kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia niongelee kuwaandaa vijana wetu kimichezo. Katika shule zetu za msingi kuna wanafunzi wenye taaluma mbalimbali naona sasa wakati umefika kuibua vipaji vya wanafunzi hawa tusisitize michezo ifundishwe kabisa mashuleni kama ilivyokuwa mwanzo. Mwanzo kulikuwa na UMISETA na michezo mbalimbali sasa hivi naona kabisa imefifia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika *English Medium* hizi shule za *private* michezo hawana kabisa, nashauri Waziri afuatilie ili nao wao wawe na mashindano kama ilivyo katika shule za Serikali. Ukiangalia *English Medium* zote watoto hawana michezo yoyote wapowapo tu, hamna mchakamchaka yaani hawaeleweki. Naomba Waziri wa Elimu aangalie hizi shule binafsi wawe na mazingira ya watoto kucheza, wanakuwa *dormant,* hawajielewi na wakati tuna watoto wengi kule ambao wangeweza kuwa ile timu yetu ya *Serengeti Boys*. Ile timu yetu *Taifa Stars* wale wanaendelea kuzeeka, kwa hiyo tunatakiwa tuendelee kuandaa vijana wengine huku toka kwenye shule zetu. Kwa hiyo, nashauri tuendelee kuandaa vijana katika mtiririko unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Maryam Msabaha, atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia tena kusimama katika Bunge lako hili Tukufu nikiwa na kauli thabiti na pumzi. Nitoe pole kwa walimu na wanafunzi wa Mkoa wa Arusha waliopatwa na maafa. Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi na wafiwa wote awape faraja, kila nafsi itaionja mauti kwa wakati na wasaa wake.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri aangalie pia hotuba ambayo imewasilishwa na Kambi ya Upinzani, siyo yote aliyowasilisha ni mabaya yapo mazuri ambayo anaweza kuyachukua akaboresha Wizara yake. Siyo useme Upinzani kila kitu ni kubeza, sisi tupo hapa kushauri na yale mazuri tuliyowashauri kwenye hotuba ya Upinzani muyachukue ili mboreshe Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la Kiswahili lugha ya Taifa. Zanzibar kuna wataalam wazuri sana wa Kiswahili lakini tumejipanga vipi katika ajira za Afrika Mashariki

kuhusu lugha hii? Tunaona wenzetu Kenya hata nafasi zile za kwetu wanajitangaza. Leo hii ukiwa Marekani unakuta wenzetu wao ndiyo wanajitangaza kwenye hii fani ya Kiswahili wanakaa kule mpaka wanakuwa wakalimani, wanasomesha lakini bado Watanzania wako nyuma katika hili suala la kutangaza Kiswahili au kuchangamkia hizi ajira za soko la Walimu wa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, nimuulize Mheshimiwa Waziri, ana mkakati gani kuhakikisha Maprofesa wa Chuo Kikuu ambao wako kwenye masuala ya lugha yetu ya Taifa ajira zinazotoka kwenye hizi nchi za Afrika Mashariki wanapata fursa? Tumemwona Mheshimiwa Rais yuko katika masuala haya ya kukuza Kiswahili na kauweka utaifa mbele hata anavyokwenda kwenye mikutano mara nyingi amekuwa akiongea Kiswahili. Hata hivyo, tuangalie hawa wakalimani ambao wanafuatana na Mheshimiwa Rais ni namna gani wanaweza kujipanga Rais akiwa anahutubia angalau waende hatua kwa hatua yale maneno ya tafsiri yafahamike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri hata wanaopata nafasi ya kuwakilisha nchi yetu ya Tanzania kwenye mikutano mbalimbali na wao watangaze Kiswahili kama lugha ya Taifa. Nasema hivi kwa nini? Hakuna nchi yoyote ambayo imeendelea duniani kwa kuiga lugha za wengine. Ukienda dukani kwa wenzetu Korea huwezi kuuziwa kitu kama hujui Kikorea, lugha yao wameiweka mbele hata Japan na China ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasi tuangalie ni namna gani tutakuza lugha yetu ya Kiswahili siyo mtu unafika mahali unakwenda kwenye mkutano wa kimataifa unaongea Kiswahili lakini hakieleweki kama unaongea Kiswahili au Kiingereza. Tusimame tusimamie lugha yetu ya Taifa ili nasi tujitangaze na tukuze uchumi kwa kupitia lugha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la vyombo vya habari. Vyombo vya habari ni suala mtambuka. Vyombo vya habari vinatoa taarifa ya matukio mbalimbali kwa jamii.

Tumeona ni namna gani jamii imetumia vyombo hivi vya habari na wakapata msaada. Mfano kuna Watanzania hasa wa vijijini ambao walikuwa wanaugua au wako katika hali mbaya kiafya au wana maradhi sugu tumeona kalamu za waandishi wa habari zilivyotumika na Watanzania hawa wakapata msaada.

Mheshimiwa Spika, hapa tuna Wabunge wa Majimbo, Viti Maalum (Mikoa) au wa Kuteuliwa na Rais na tuna Mawaziri ambao wamepitia kwenye Majimbo wakapata uwaziri lakini utaona ni namna gani sisi wanasiasa tumeminywa katika vyombo vya habari. Napenda kujua ni kitu gani Serikali mnachoogopa katika suala hili la vyombo vya habari kwa suala la kutangaza *Bunge live*? Kwa sababu unavyotangaza *Bunge live* mimi kama mimi nimetoka Zanzibar, kuna wananchi wangu wanataka wajue leo Msabaha kaongea nini kuhusu Zanzibar lakini hawapati. Hamuoni mnajijengea mazingira ambayo ni magumu itakavyofika 2020 kwenda kuomba kura kwa sababu Watanzania wanataka wasikie wawakilishi wao waliowatuma wanasema nini Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanakatwa kodi zao kwa ajili ya *TBC,* kwa hiyo wanategemea iwapatie mijadala ya Bunge la Bajeti waone Mbunge wao kasema nini Bungeni. Hata wengine tukiongea humu huwa taarifa nyingine kama hazijapendeza watu haziwezi kutoka, kila mtu ana haki katika Bunge hili na kila mtu kaletwa hapa na wananchi kuwakilisha sehemu alipotoka.

Mheshimiwa Spika, tuangalie tena suala lingine, hapa kuna wawakilishi kutoka upande wa Zanzibar, kuna Wabunge ambao wametoka kule na kuna Wawakilishi ambao wamekuja hapa kutoka Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo ni muhimu tuangalie pia sekta ya Muungano kuhusu vyombo vya habari. Katika sekta hii ya habari wale wanaokuja kuchukua habari zetu kwa upande wa pili nao wamo au habari za Zanzibar zitaishia kubaki Zanzibar na za Bara zitaishia kubaki Bara? Kwa hiyo, tuangalie namna ya kudumisha Muungano kwenye suala la habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende tena kwenye suala la michezo. Michezo ni afya lakini hata michezo ndani ya Bunge, sisi tumekuwa tukienda kuwakilisha Tanzania Afrika Mashariki. Tumeshuhudia wenzetu waliokwenda Kenya (Mombasa) kwenye mashindano ya Afrika Mashariki utajiuliza kweli Serikali ina mikakati ya kukuza michezo kwani Wabunge waliokwenda kule walitia aibu. Tuangalie tumejipanga vipi hata tunavyoshiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki kama Wabunge na sisi tupate hadhi zetu kama Wabunge.

Mheshimiwa Spika, leo michezo haipewi kipaumbele. Tuangalie Brazil, Brazil imeendelea kutokana na michezo, kwa nini sisi Tanzania hatutaki kuipa michezo kipaumbele? Tumefanya michezo ni kama kiburudisho au kuondosha kisukari na presha kwenye mwili, hapana, michezo inaingiza pato la Taifa. Naomba tuangalie namna gani ya kukuza michezo na kutafuta vipaji, tuanze na sisi Wabunge ni mara ngapi tumekuwa tukileta makombe ndani ya Bunge hili, lakini kila tunavyokwenda mbele michezo inasahaulika.

Mheshimiwa Spika, zamani wakati tupo shuleni michezo ilikuwa inaanza kule shuleni, unaanza kuangalia vipaji kule shule, unaanza kumkuza yule mtoto akiwa mdogo mpaka anafika kiwango cha kuwa mwanamichezo bora lakini sisi michezo tumefanya kama sehemu ya kutoa presha na kisukari kwenye miili yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itenge bajeti ya kutosha kuhusu michezo na hasa suala la Wabunge wanavyoshiriki kwenye mashindano ya Afrika Mashariki pia watengewe bajeti ya kutosha. Mheshimiwa Spika utalichukua kama wewe ndiyo kiongozi wetu wa Bunge na siyo kama tunashiriki michezo ya Afrika Mashariki tunakwenda kudhalilika mbele ya Wabunge wenzetu. Hilo naomba ulipe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yameongelewa sana mambo ya sanaa. Kwenye sanaa wanawake...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunakushukuru kwa mchango wako. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri pamoja na mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, nianze na hili la *TBC*, naona wenzangu wengi wameliongelea suala hili. Bahati nzuri Spika wewe ni shahidi, nilipokuwa Mbunge kipindi cha mwanzo miaka 20 nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Katiba, Sheria na Utawala na Utawala ilikuwa ni pamoja na Waziri Mkuu na *TBC* ilikuwa kwenye Kamati yangu, nimetembelea mitambo yote ya *TBC* karibu nchi nzima. Hiki ni chombo cha Serikali, kwa nini vyombo vya watu binafsi vifanye kazi nzuri, matangazo yasikike vizuri kuliko *TBC*?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha lakini hatuwezi kumlaumu Dkt. Rioba - Mkurugenzi wa *TBC* ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa nini Serikali isitenge fedha za kutosha kununua mitambo ya kisasa ili *TBC* isikike kama redio zingine za watu binafsi? Kwa hiyo, huo ndio ushauri wangu. Wafanyakazi wa *TBC* wanafanya kazi usiku na mchana, waboreshewe maslahi yao na ndio maana wanahama kwenda vyombo binafsi kwa sababu ya maslahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nizungumzie habari, habari haziko mjini tu, ziko vijijini. Ukienda Wilaya ya Mpwapwa Vijijini utapata habari, kuna watu wanafanya kazi za kujitolea vijijini. Ukienda Wilaya ya Kongwa, Zoisa, Mlali, Kibakwe, Mpwapwa kule sehemu za Mima, Matomondo watu wanafanya kazi nzuri sana ya kujitolea lakini hawatangazwi, hawa waandishi wa habari wanazunguka mjini tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri kila wilaya iwe na mwandishi wa habari. Mheshimiwa Waziri ananisikiliza au anaongea na Naibu Waziri? Kila wilaya iwe na mwandishi wa habari wa Serikali ili aweze kupeleka taarifa hizi za maendeleo katika wilaya zetu lakini siyo kuandika taarifa za mjini tu, kila siku mjini, hapana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uandishi wa habari ni taaluma na ina mipaka. Huwezi kuandika jambo lolote unalotaka wewe haiwezekani, lazima kuna mipaka yake, uandike kwa kuzingatia maslahi ya nchi yetu. Siyo unaandika kwa kujifurahisha upate fedha kama biashara, *no,* lazima uandike taarifa kwa kuzingatia maslahi ya nchi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni michezo. Mimi ni mpenzi wa Simba *Sports Club.* Kila siku timu ya Simba ikicheza lazima utasikia Lubeleje anaipongeza Simba, anaitakia ushindi. Sasa tumenyang'anywa *point* tatu, Bwana Malinzi sitaki kuzisema sana hizo, lakini mimi ni Hakimu, kwenye *court of law* ukishakiri jambo, umekiri. *TFF* walikiri kwamba kweli yule mchezaji wa *Kagera Sugar* alikuwa na kadi za njano tatu, *that is plea of guilty*. Huwezi kusema kwa sababu umesemasema sana, mmekosea halafu mkamnyang'anya *point* zake, hilo naiachia *TFF. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpwapwa nilikuwa na Timu ya Mji Mpwapwa, imecheza ligi kuu miaka tisa na ilikuwa inaogopwa na timu za Yanga na Simba. Nikubaliane na mwenzangu aliyesema Timu ya Taifa siyo lazima wachezaji watoke Simba na Yanga tu, hapana, tunaweza kupata wachezaji wazuri hata wilayani huku. Kongwa kuna Timu ya Hengo ni nzuri sana. Kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri

arudishe michezo shule za msingi na sekondari, UMISHUMTA na UMISETA, huko ndiko tunakopata wachezaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuomba dakika tano na dakika tano nimemaliza, lakini nashukuru sana Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri, waendelee hivyo hivyo ila ombi langu kila wilaya ipate mwandishi wa habari, tuache kuweka waandishi wa habari wote mjini, hapana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa George Malima Lubeleje. Mheshimiwa Waziri wa Nchi nilikuona umesimama.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, taarifa kabla hajakaa.

**SPIKA:** Hajakaa bado endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nataka tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi kadiri siku zinavyozidi kwenda Timu ya Majimaji inaonekana kuwa tishio la timu zote katika nchi hii ya Tanzania. Sasa sijui taarifa hiyo anayo, kwa hiyo, nilikuwa nataka tu nimpe hiyo taarifa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje unapokea taarifa kwamba Timu ya Majimaji ndiyo tishio na sio Timu ya Mji Mpwapwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, sipokei taarifa hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, mpambe mwingine wa Majimaji huyo. *(Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Nikupongeze sana kwa namna unavyofanya kazi ya kuliongoza Bunge hili, kwa umahiri mkubwa ikiwa ni pamoja na timu yako. Hongereni sana, chombo kinakwenda barabara, tumeridhika na utendaji wako wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na nitakwenda moja kwa moja kwenye haki za wasanii. Naomba niongelee tu kwenye eneo hili la wasanii. Wasanii wetu wa Tanzania wanafanya kazi nzuri. Moja kati ya kazi kubwa ambayo wanaifanya ni pamoja na kuitangaza nchi yetu. Wako wasanii wazuri ambao wanafanya vizuri kwenye michezo kwa maana ya mpira wa miguu lakini pia kwenye kuimba na mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, napenda niwatambue baadhi ya wasanii hapa ambao wanafanya vizuri kwa mfano, Mzee Jongo, Ray, Diamond, Khadija Kopa, Ali Kiba, Profesa Jay na kijana mmoja machachari sana ambaye anawakilisha Mkoa wa Ruvuma yuko katika Bendi ya *TOT* anaitwa Neka, kijana huyo anatoka katika Wilaya ya Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wasanii wetu ni vizuri kabisa tukahakikisha kwamba wanapata haki zao za msingi ili kuweza kufanya usanii wenye tija. Inaonesha kwamba hawa wasanii kumekuwa na sheria ambayo inawabana. Wakati mwingine wanapenda kurekodi *video* zao ili watengeneze kanda lakini wanakuwa wanabanwabanwa, kwa mfano, labda anahitaji kwenda kurekodi kwenye eneo la daraja lile la Kigamboni, visheria vinawabanabana wanashindwa kufanya hivyo. Wakati mwingine wanatamani hata watumie labda gari la polisi kwa ajili ya kurekodi lakini wanashindwa

kufanya hivyo, lakini wakitoka hapa wakaenda nchi za wenzetu wanapewa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kama kuna sheria inawabana kutumia vitu hivyo basi tuweze kuileta hapa tuirekebishe ili wapate haki za msingi za kuweza kufanya *recording* ambayo itawasaidia na watakuwa wanafanya uwekezaji wenye tija kwenye usanii huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende pia kwenye suala la usikivu wa *TBC.* Kule kwetu Nyasa bado *TBC* haisikiki vizuri. Namwomba Mheshimiwa Waziri afanye kazi ya ziada, kwa sababu mpaka sasa hivi tunasikiliza habari za Malawi. Kuna ka-*station* fulani ya ka-Malawi kanachezacheza pale, sisi hatutaki, sisi sio wa Malawi, sisi ni Watanzania, weka *TBC,* acha maneno, weka muziki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi alisimama Mbunge mmoja hapa, nadhani matatizo ya kwenye jimbo lake yamekwisha kabisa hata wananchi wake wamekuwa wana hali nzuri kiasi ambacho hawana changamoto yoyote amejikuta anaacha kushughulikia mambo ya jimbo lake anaenda kushughulikia mambo kama ya shilawadu. Amesimama hapa akiongelea suala la Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kufichwa, mimi nashangaa sana Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi amefichwa wapi au kutekwa kwa namna moja au nyingine wakati huyu Katibu Mkuu yuko Arusha. Naomba niseme haya hayamhusu, ashughulike na ya kwake yanayomhusu. Pia huyu Kinana ni Katibu sio wa lelemama huwezi kumlinganisha Katibu huyu wa Chama kikubwa Chama cha Mapinduzi ukamlinganisha na Makatibu wa vyama ambavyo vinafanana na *SACCOS* fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kanali Mstaafu Kinana ni kiongozi mzuri, ni mwamba wa vita, ni mpiganaji hasa hasa kwenye Chama chetu cha Mapinduzi. Pia ni mkweli, ni mchapakazi na hana uwoga kwenye kusemea Chama chake cha Mapinduzi. Sasa nashangaa ukamchukua Kinana unamlinganisha na chama chake na wala nisimfiche ni Mheshimiwa Lema, anamlinganisha Kinana gwiji la siasa,

mwanaume kabambe ambaye anaweza kusimamia Chama cha Mapinduzi ipasavyo na Katibu wake ambaye haeleweki kama yuko duniani au yuko akhera mpaka sasa hivi, hii inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshauri tu kaka yangu Lema na mimi niseme toka nimefika hapa nimeanza Bunge hili la Kumi na Moja sijawahi hata siku moja kusikia akiongelea masuala yanayohusu jimbo lake amejikita kwenye mambo ya diplomasia ya kitaifa na kama nasema uongo rejeeni *Hansard* zake zote mtaona. Niseme hivi kwamba kama anahitaji aje tu CCM wala hatuna hiyana tutampokea lakini hii kutafuta chokochoko sio njema.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Jimbo hilo la Arusha, naomba nimshauri kaka yangu Lema ajikite huko, watu wa Arusha bado wana changamoto kubwa sana wanahitaji wasemewe na Mbunge wao, badala yake yeye amejikita kwenye mambo ya ushilawadu na kwenye mambo ya unabii...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mimi niseme kazi ya unabii siyo yake kwa sababu ni nabii wa uongo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, alitabiri hapa Dkt. John Pombe Magufuli atakufa na hajafa, ndio kwanza anaendelea kutekeleza majukumu yake, kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ipasavyo na maendeleo yanaonekana. Kazi anazozifanya Dkt. John Pombe Magufuli...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Ni kazi nzuri na wanachi wote wanazikubali.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unabii wake ni wa uwongo na mimi leo nataka nimbatize jina…

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Jina ninalombatiza leo hii ni nabii Israel mtoa roho za watu.

**SPIKA:** Mwalimu nimekuona. Mheshimiwa Jacqueline naona mwalimu amesimama.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mbunge kwa Kanuni ya 64(1)(b) Mbunge kutozungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mimi ndiyo nimepewa nafasi ya kuzungumza. Bajeti iliyoko mbele yetu haihusiani na shilawadu na haihusiani na Mheshimiwa Kinana. Suala la Mheshimiwa Kinana lilishatolewa taarifa humu Bungeni na likaeleweka kwamba yupo hajapotea. Sasa anapoliendeleza anazidi kuonesha kama vile amepotea kweli au yupo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba kusema kwamba Mheshimiwa Jacqueline yuko sahihi tu kwa sababu anaongelea habari na habari zenyewe zilizotolewa hapa Bungeni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jacqueline endelea kujadili hotuba ya Wizara ya Habari. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ndiyo maana nimesema uko vizuri na unachapa kazi ipasavyo na tunakubaliana na utendaji wako wa kazi. Kwa sababu wako watu sasa wanashindwa kujitambua nini aseme hata ulivyokuwa unajaribu

kumfundisha, tunakushukuru umekuwa mwalimu kwetu, umemfundisha hapa msemaji mmoja alikuwa anaongelea vyeti, mara ooh siyo lazima uwe na vyeti, mara nini, haeleweki, Mbunge wa Ubungo umemfundisha hapa vizuri lakini unaendelea kutoa hiyo elimu hata Mwalimu na yeye umemfundisha vizuri. Tunakushukuru sana na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu endelea kuchapa kazi tuko nyuma yako tunakuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa siipokei kimsingi amenipotezea muda na naomba unilindie dakika zangu, nina mambo ya msingi sana ya kuchangia hapa. *(Makofi/ Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Changia hoja basi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa utulivu sana kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana ya habari. Sina mashaka na utendaji wake wa habari, sina mashaka na utendaji wake wa kazi, ni Waziri mahiri, ni Waziri ambaye ameshafanya kazi Wizara mbalimbali na kila eneo alilopewa kufanya kazi amefanya vizuri. Kwa hiyo, ni matumaini yangu atawatendea haki wasanii wa nchi hii na ataitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwatie moyo Mheshimiwa Waziri, Naibu pamoja na timu yako yote fanyeni kazi. Hizi kelele za chura hazimzuii mwenye nyumba kulala, wala kelele za chura hazimzuii chura kunywa maji, kwa hiyo endeleeni kuchapa kazi, tuko nyuma yenu tunawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Jacqueline pamoja na uliyoyaongea, nashukuru sana kututaarifu kwamba Mheshimiwa Kinana yupo na hajambo kabisa. Pia ukanifanya kidogo nianze kuwaza kuhusu hawa Makatibu Wakuu, nikawaza huku Katibu Mkuu sijui nani sijui, huku

upande huu, kule kwingine sijui nani Katibu Mkuu, kwa watani zangu kule. Siku nyingine jamani humu ndani mtutajie Makatibu Wakuu wenu akina nani. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Wapo.

**SPIKA:** Wapo eeh?

**WABUNGE FULANI:** Wapo.

**SPIKA:** Nashukuru nasikia wapo*. (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari na Michezo ni Wizara muhimu zaidi ikilenga kuinua michezo, burudani na kuelimisha jamii kupitia nyimbo na michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nahitaji kujua ni lini Serikali itakamilisha kuweka ofisi za usajili kila wilaya ofisi za *COSOTA* na BASATA ili kuondoa usumbufu kwa wasanii wakitaka kusajili kazi zao mpaka waje Dar es Salaam; huoni kama huo ni usumbufu kwa wadau wa sanaa. Je, hamuoni kama huu ni upotevu wa kodi kwa sababu msanii mchanga hawezi kujigharamia mpaka afike Dar es Salaam na pia kuna urasimu mkubwa katika ushuru wa *stamp?* Je, ni lini Serikali itaondoa kero hizi; itapunguza urasimu kupitia usajili *COSOTA*, BASATA na *TRA,* wasanii kuibiwa kazi zao, kujenga ofisi kila Wilaya, kuzingatia maadili katika kazi za sanaa za maigizo, michezo, nyimbo, vichekesho vinavyokiuka maadili ya Kitanzania? Ni lini Serikali kupitia *COSOTA*/BASATA itaacha ubaguzi kwa kuwafungia nyimbo/maigizo kazi za sanaa kwa baadhi ya watu na wengine hawachukuliwi hatua wanapotengeneza video zinazochefua jamii. Itawatafutia masoko wasanii. Kazi za sanaa zinalala ukizingatia nchi kama Kenya wako vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge kuonesha *live.* Ni lini Serikali italiachia Bunge kuoneshwa *live*. Je, hamuoni kwamba kuzima Bunge mnajichimbia kaburi nyie wenyewe. Mmeondoa uhuru wa Watanzania kuongea kwa uhuru, kuonya, kuelimisha na kuikumbusha Serikali kupitia Bunge *live* na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, Sheria kandamizi za mitandao. Hamuoni kwamba Watanzania pamoja na Sheria hii mpya ya habari hawajajifunza na kutambua vizuri matokeo yake. Mnawafungulia mashtaka Wapinzani tu CHADEMA, *CUF* wao CCM hawavunji Sheria? Acheni tabia ya kunyanyasa watu. Roma Mkatoliki mlimteka kwa sababu tu kaongea ukweli kaisema Serikali, Je, uhuru wa habari uko wapi?

Mheshimiwa Spika, habari Bunge; leo hata waandishi wa habari wanaoingia Bungeni hawapati taarifa kamili ili ziruke kwa Watanzania mpaka ziwe zimekuwa *edited (filter)* kitu ambacho kinapunguza ukweli wa habari. Wizara iangalie hili ili kuweka uhuru wa waandishi wa habari kupata taarifa kutoka Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuchunga hotuba za Kambi Rasmi ya Upinzani. Hii ni kero na hailisaidii Taifa. Kambi ya Upinzani ni mbadala wa Serikali tawala katika kuisaidia Serikali kibajeti katika vipaumbele ili Wizara zisonge mbele. Sasa hotuba zinapofanyiwa *editing,* je, hamuoni kama mnapoteza lengo la Upinzani kuisaidia Serikali. Tunajenga nyumba moja na Taifa moja, ubaguzi usifanyike kwa Upinzani tu bali angalieni haki.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Nianze na utamaduni. Palikuwepo na mchakato wa kuanzisha vazi la Taifa na fedha zilitumika katika mchakato wa kupata vazi hili ilifikia mpaka kutolewa mifano ya vazi la Taifa. Je, mchakato ule umefikia wapi na mpaka sasa fedha kiasi gani zimetumika?

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi vijana wetu maadili yameporomoka sana, kuanzia mavazi hata baadhi ya lugha wanazotumia, heshima kwa wakubwa hakuna na kupoteza

kabisa mila na desturi ya Watanzania ya kuheshimu hata wakubwa zao. Je, Serikali imejipangaje kurudisha maadili na utamaduni wetu wa Kitanzania wa kuheshimiana? Tukiimarisha utamaduni wetu, wa kucheza ngoma za kienyeji, mapishi ya kienyeji na kadhalika inaweza kuwa ni moja ya vivutio vya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, michezo. Kutokana na magonjwa kuongezeka duniani magonjwa yasiyoambukiza kama sukari ya kupanda, shinikizo la damu la kupanda juu na magonjwa ya moyo, mazoezi ya mara kwa mara yanaweza kupunguza magonjwa haya. Je, Serikali wamejiandaa kwa kiasi gani kuhakikisha wanajenga viwanja vya michezo kwa Wilaya kwa kuanzia lakini ziteremke chini kila Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha *King Memorial* kilichopo Manispaa ya Moshi. Uwanja huu ni mkubwa kabisa na michezo zaidi ya saba. Hakuna uwanja Moshi na uwanja huu ni wa Mkoa. Tumekuwa tukitumia uwanja wa ushirika ambao ni mdogo, tulishuhudia sherehe za Mei Mosi 2017 pale uwanja wa Ushirika walishindwa kufanya maonesho ya magari kwa sababu ya udogo wa uwanja. Hata mashindano yajulikanayo kama Kilimanjaro *marathon* huwa yanafanyika uwanja wa Ushirika, lakini michezo hii imekuwa sana inaleta wageni duniani pote kwa sasa ni padogo na suluhisho ni kuutengeneza uwanja wa *King Memorial.* Hivi inaingia akilini *King Memorial* penye heka zaidi ya 10 patumike tu kama soko la kuuzia mitumba ambayo hawatumii hata eneo lisilozidi heka mbili? Kwa nini wasipatiwe sehemu nyingine kama kule Pasua, Manyema na kadhalika, sehemu zipo nyingi.

Mheshimiwa Spika, habari. Ni haki ya Watanzania kupata habari. Hii ikiwa ni pamoja na wananchi hawa kupata habari zinazoendelea Bungeni ili wajue Wabunge wao kama wanawasilisha matatizo yao. Kwa kuwanyima haki hii ni uvunjifu wa Katiba. Je, ni lini shughuli zote za Bunge zitarudishwa na kuanza kurushwa *live* ili wananchi waweze kupata habari kuhusu nini kinaendelea Bungeni? Kwa nini Serikali inaogopa?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, *TBC*. Televisheni ya Taifa haifanyi matangazo kwa usawa hasa inapochukua matangazo ya kisiasa kwa uwiano sawa na vyama vingine. Pia *TBC* ijikite kutoa elimu ya uraia na mendeleo zaidi katika vipindi vyake badala ya kuweka vipindi vya muziki kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee viwanja vya michezo mikoani. Katika Mkoa wetu wa Mbeya hatuna viwanja vya kutosha vya michezo vinavyoweza kusaidia watoto wetu kujifunza michezo na kukuza vipaji kama mjuavyo Mbeya na viunga vyake bado vinatoa wachezaji bora wa michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niongelee viwanja vya wazi. Viwanja vingi vimetaifishwa na watu wachache bila kuchukuliwa hatua za kisheria na kurudisha viwanja hivyo kwa wahusika ikiwemo Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa. Ni lini vazi la Taifa litakuwa tayari katika utekelezaji wa utumiaji huo. Kama Taifa tunahitaji utambulisho wa vazi letu.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu timu ya mpira wa miguu. Tumekuwa jamii na Taifa la kushindwa kila wakati kwa Wizara kutowekeza zaidi katika timu hii, lakini Wizara kutosimamia miundombinu/aina ya namna ya kupata wachezaji bora toka sehemu mbalimbali ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho niongelee suala la ufungiaji wa wanamuziki. Siku za hivi karibuni Serikali imekuwa inawafungia waimbaji wa nyimbo za bongo fleva kwa kile kinachodhaniwa hakiwafurahishi watawala. Hii inaondoa ubunifu na hali ya wasanii kuimba hisia zao kwa usahihi. Serikali itumie ofizi zake kama BASATA kuwasimamia wasanii hawa kufuata kanuni na haki za wasanii bila kubagua na kupendelea kwa kutumia hisia za kisiasa tu.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa

kuboresha mfumo wa habari Tanzania, pamoja na mambo mazuri yanayofanyika lakini nipende kutoa ushauri kwa yafuatayo:-

(1) Kuboresha zaidi televisheni ya *TBC* kwa mfano mitambo ya radio;

*(2)* *TBC* kusikika Tanzania nzima

(3) Maslahi ya wafanyakazi; na

(4) Mafunzo kwa wafanyakazi yawepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo nashauri:-

(1) Kuboresha viwanja vya michezo katika Wilaya na Mikoa;

(2) Kukuza michezo kwa vyuo, sekondari na shule za msingi;

(3) Vijijini kuna vijana wanaoweza kucheza mipira, riadha na michezo mbalimbali, lakini wanakosa msaada wa vifaa na viwanja vya michezo; na

(4) Viongozi ni tatizo kubwa wapo kwa ajili ya maslahi siyo kukuza vipaji vya michezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba mchezo wa ngumi na riadha itiliwe mkazo ili waliletee Taifa sifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri na pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)* ni chombo cha Serikali na *TBC* inafanya kazi nzuri sana ya kuwatangazia wananchi habari mbalimbali za maendeleo na uchumi wa nchi yetu *TBC* Taifa, *TBC1, TBC FM* na *TBC International* wote wanafanya kazi nzuri sana. *TBC* Taifa inasikika vizuri katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto, wafanyakazi wa *TBC* waboreshewe maslahi yao kwa kuwa wanafanya kazi usiku na mchana kuwatangazia wananchi habari mbalimbali, mitambo ya *TBC* iboreshwe Makao Makuu Dar es Salaam na Kanda zote ikiwemo *TBC* Kanda ya Kati Dodoma kwa kuwa hivi karibuni matangazo ya *TBC* Taifa yalikuwa yanakatikakatika kila wakati na kufanya wasikilizaji kukosa habari au matangazo muhimu. *TBC1* pia wakati mwingine matangazo hukatika na kutokuonyesha taarifa za habari vizuri na rangi nyeupe.

Mheshimiwa Spika, Jengo la *TBC1* lililopo Mikocheni likamilishwe kwa kuwa ujenzi ulianza zamani. Je, Mheshimiwa Waziri kwa nini jengo hilo halikamiliki miaka mingi? Zitengwe fedha za kutosha kukamilisha jengo hili.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari kwa ujumla, kwa kuwa sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo na uchumi wa nchi hii na sekta ya habari ni taaluma hivyo, nashauri waandishi wa habari wawe wamesomea taaluma hiyo na waandishi wa habari ambao hawana taaluma hiyo waondolewe.

Mheshimiwa Spika, Televisheni zinazoonyesha picha chafu ambazo ni kinyume na maadili ya Watanzania, zifungiwe au wapewe onyo ili wasioneshe picha chafu kwenye Televisheni na kama wataendelea kukiuka wachukuliwe hatua za kisheria. Vile vile kila Wilaya kuwe na Afisa Habari ili kuandika na kutangaza habari za maendeleo ya Wilaya ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa viwanja vya michezo; kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma

tunampongeza sana na kumshukuru Mheshimwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kukubali uwanja mkubwa wa michezo ujengwe mjini Dodoma Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ligi kuu ya *Vodacom;*, kwa kuwa ligi kuu ya *Vodacom* inaendelea na katika mechi ya timu ya Simba na Kagera *Sugar* iliyochezwa uwanja wa Kaitaba Mjini Bukoba, ilithibitika kwamba Kagera *Sugar* ilimchezesha mchezaji aliyekuwa na kadi tatu za njano kinyume kabisa na kanuni za ligi kuu. *TFF* ilikiri kwamba mchezaji huyo alikuwa na kadi tatu za njano lakini hata hivyo Simba walinyang'anywa *points* tatu kwa maelezo kwamba walikosea taratibu za rufaa. Mheshimiwa Waziri naomba maelezo kwa nini Simba walipokonywa *points* tatu, Serikali isimamie suala hili ili timu ya Simba wepewe haki yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote kwa kazi na kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu na Serikali tumekuwa na kasumba ya kutokuwekeza kikamilifu fedha ya kutosha kwenye michezo na hilo suala la kuwezesha michezo mbalimbali kuachwa kwa wahisani, mashabiki na wapenda michezo.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunashuhudia tunapeleka *team* kambini kwa maandalizi ya mashindano ya Kimataifa lakini wachezaji wanalalamika hata chakula wakiwa kambini hawapewi inavyostahili, hii ni aibu kwa Taifa huwezi kuvuna bila kupanda.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma michezo mashuleni ilipewa uzito na kipaumbele kwa maana tangu *primary school* tulijengewa misingi mizuri ya kuifahamu vizuri mchezo, lakini pia kusaidia wanafunzi kwa sasa shule nyingi hasa shule za umma hakuna jitihada zozote za kuendeleza michezo na hakuna walimu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha tunajenga vipaji vya watoto bado mapema, Serikali ieleze Bunge mikakati ya kuhakikisha kwenye mashule yote kuna Walimu wa michezo wenye ujuzi wa michezo. Serikali ieleze mikakati ya kupeleka vifaa vya michezo kwenye shule za umma ili watoto wapate fursa ya kushiriki michezo na kujenga afya na akili zao.

Mheshimiwa Spika, viwanja vingi vilivyotengwa kwa michezo maeneo mbalimbali vimevamiwa na kujengewa makazi na Serikali inalijua hili, Serikali ieleze Bunge viwanja vyote vya michezo nchini vinalindwaje, visivamiwe lakini pia ni mikakati gani ya Serikali kurejesha viwanja vilivyovamiwa.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunashuhudia watoto wakitumika kwenye michezo ya maigizo na hivyo kuwapotezea ndoto zao lakini pia kuwajengea taswira hasi kwa michezo inayotisha. Serikali itoe maelezo ya kutosheleza ni kwa nini watoto wanatumika kwenye maigizo?

Mheshimiwa Spika, katika Taifa letu maeneo mengi ya pembezoni mwa nchi, usikivu wa redio ni hafifu sana na maeneo mengine hakuna kabisa, mawasiliano ya redio. Je, kuna mpango gani wa Serikali kuhakikisha mawasiliano ya redio yanafika pande zote za Taifa hili ili kila Mtanzania apate haki ya kusikia na kujua yanayojiri ndani ya nchi yake.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kaliua yapo maeneo ya Kata nyingi ambayo usikivu ni hafifu sana na pengine hakuna kabisa. Kata hizo ni Kata ya Igwisi-Kijiji cha Igwisi, Kijiji cha Mpanda mlohoka; Kata ya Usimba-Vijiji vya Usimba; Kata ya Ushokola-Kijiji cha Ukikubi; Kata ya Zugimlole-Vijiji vya Igombe na Luyombe; Kata ya Ukumbi Siganga-Vijiji vya Usinga na Ukumbi kakonko; Kata ya Usingi, Kijiji cha Kombo na Luganjo; Kata ya Usonye, Vijiji vya Luganjo, Mtoni, Shela na Maboha; na Kata ya Uganga-Vijiji vya Mkuyuni, mpilipili na limbula. Serikali ieleze kuna mipango gani mahsusi kuhakikisha mawasiliano na usikivu katika maeneo haya unapatikana.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma mchakato wa kumpata *Miss* Tanzania ulikuwa unavutia na waliochaguliwa walituwakilisha vizuri Kimataifa. Kwa kuwa kwa sasa suala hili limepoteza mvuto na kuendeshwa kwa rushwa kubwa na udhalilishaji. Serikali ifute uwepo wa zoezi hili kwa heshima ya Taifa.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuinua Sekta ya Sanaa, Michezo pamoja na kusimamia mambo yote yanayohusu Wizara hii. Naomba kuchangia katika hotuba hii maeneo yafuatayo:-

Kuimarisha huduma na mitambo ya *TBC*; niungane na hotuba ya Kamati husika juu ya ushauri wao wa kuwekeza kiasi cha kutosha kwa Shirika letu la *TBC* kama ambavyo Kituo cha AZAM walivyofanya, naamini pamoja na majukumu mengi ya Serikali, lakini kuimarisha *TBC* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, *TBC* ndio ambayo imetapakaa nchi nzima na Shirika la Taifa haiwezekani tuliache shirika letu litoe huduma dhaifu. Watu wengi sasa hawaangalii vipindi vingi vya *TBC* kutokana na ubora hafifu unaotolewa na *TBC* na hatimaye watazamaji kupendelea huduma za vituo vingine kama vile AZAM, *ITV* na kadhalika. Nashauri Serikali ichukue maoni ya Kamati na sisi Wabunge na yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Mpira Tanzania *(TFF);* Shirikisho letu la Mpira Tanzania *(TFF)* kwa kiasi kikubwa wanajitahidi kutekeleza wajibu wao wa kila siku mfano ni jinsi walivyosimamia timu yetu ya mpira iliyopo Gabon kwenye mashindano ya vijana chini ya miaka 17 .

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ningependa nishauri juu ya Shirikisho letu la Mpira Tanzania *(TFF),* hivi kwa nini inajitokeza mara kwa mara Shirikisho letu limeingia katika mgogoro na vilabu vyote vya mpira? Mfano ni suala la klabu ya Kagera kunyang'anywa pointi tatu walipocheza na Simba, suala hili linalichafua sana Shirikisho letu la mpira. Hivi

*TFF* haina wataalam wa kutosha ambao wangeweza kushauri hili kumalizika kwa haraka na kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atoe majibu yenye kuridhisha kwa sababu *TFF* wapo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Mpira; viwanja vya mpira ni chachu ya maendeleo ya mpira nchini, tunavyo viwanja vichache vyenye hadhi, nishauri Serikali isimamie viwanja vilivyopo mikoani vifanyiwe ukarabati hususani maeneo ya kuchezea mpira. Inasikitisha kuona kwa takribani miaka 50 sasa tuna viwanja visivyozidi 10 vyenye hadhi ya Kimataifa. Nishauri Wizara hii kwa kushirikiana na TAMISEMI ihakikishe kila Wilaya inakuwa na kiwanja cha mpira ili kuleta maendeleo ya mpira nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri asilimia 90 ya watangazaji na waandishi kukosa sifa stahiki ya taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji. Jambo hili linasikitisha sana niombe sasa *TCRA* wahakikishe kuwa vituo vyote vya utangazaji vinazingatia sifa na vigezo ili huduma zitolewe na watu wenye sifa. Hivi inakuwaje vituo kuajiri watu wasiokuwa na sifa? Je ni hatua zipi zimechukuliwa kwa vituo vya utangazaji vilivyo na waandishi na watangazaji wasio na sifa?

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI kwa utaratibu wa kuandaa vijana na *TFF* kuandaa vituo vya Ufundi kila mkoa kwa madhumuni ya kulea vijana. Jambo hili ni zuri sana na kama litasimamiwa vema litaleta maendeleo ya dhati na ya kweli ya mpira nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linahitaji kuwa na rasilimali fedha, sijaona wapi Wizara imetenga fedha katika kutekeleza mpango huu. Vile vile napongeza ushauri wa sisi Waheshimiwa Wabunge kuanzisha vituo vya mfano huu katika maeneo yote ya Majimbo.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari na Utamaduni kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Napongeza Utendaji mzuri wa Wizara na kwa kweli wanafanya kazi nzuri kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika Utamaduni wa Mtanzania. Utamaduni wa Mtanzania unapotea kwa kuwa kizazi chetu kinafurahia sana tamaduni za kizungu kuliko zetu. Vifaa vyetu vya asili kama mundu, kinu, mchi, kisagio, mtungi, kata, vibuyu na kadhalika vyote vinapotea na hakuna wa kuvirudisha. Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda utamaduni wetu wa asili kwa kuvilinda vifaa vyetu vya asili.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa mazao yetu pia, kwa kuwa shule nyingi ziko maeneo ya mijini utakuta wanafunzi wanashindwa kujua hata mmea wa mahindi ukoje? Naomba Serikali waweke mpango mahsusi wa kuandaa maeneo maalum ya kitamaduni kama vile Kijitonyama kuweka sehemu ya vitalu vya kuonyesha utamaduni wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hiyo itasaidia katika kukuza na kuendeleza utamaduni wetu. Sambamba na hiyo ni mavazi yetu ya asili kama kaniki, kanzu, migolole, shanga, vibwaya na kadhalika. Vifaa hivyo vitunzwe kwa kumbukumbu kwa kuwa vinatoweka sasa.

Mheshimiwa Spika, Sanaa; wachezaji muziki walio wengi wanaume wanavaa nguo vizuri sana lakini wanawake wanavaa nusu uchi. Hali hiyo inatudhalilisha sana wanawake na inatuharibia kizazi chetu kipya kwa kuiga mavazi ya utamaduni ambao si sahihi sana. Serikali itoe kauli kwa wanawake wanaocheza muziki wavae mavazi yao ya heshima pasipo kuwadhalilisha wanawake wenzao.

Mheshimiwa Spika, Mapambo; utamaduni wa kusuka nywele, tumeona watoto wanakua kwa kukazwa nywele

na kumfanya mtoto ashindwe kupumua na kupoteza maisha. Serikali itoe angalizo kwa akinamama wenye watoto waangalie watoto wao na wawasuke nywele za kawaida za utamaduni za mikono kwa kuwasaidia watoto mpaka watimie umri wa miaka 12 kwenda juu umri huo mtoto anaelewa baya na zuri.

Mheshimiwa Spika, *TBC*; ijengewe uwezo iweze kuwa na mitambo mizuri na shughuli za Kiserikali ikiwemo shughuli za Wabunge Majimboni watumie *TBC Radio* na *TV* itasaidia hata kuongeza kipato. *TBC* wajitahidi wawe na mawasiliano katika mikoa yetu ya Tanzania Bara na Zanzibar ili wananchi wetu wafaidi matunda ya *Television* yetu na *Radio* yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika kwa ufanisi hotuba ya Wizara yao. Nawaombea kila la kheri katika majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC);* Shirika la habari ni chombo muhimu katika nchi kwa kuelimisha na kupasha habari wananchi wake. Bado kuna matatizo makubwa kwa wananchi wa vijijini ya usikivu usioridhisha. Wananchi wanashindwa kupata matokeo muhimu ambayo ni haki yao. Ushauri wangu katika hili ni kwamba, Serikali kuboresha miundombinu ya *TBC* kwa kununua vifaa vya kisasa vitakavyoondoa kabisa tatizo hili. Aidha, Serikali iongeze kasi ya kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya maendeleo ya michezo; michezo ni jambo lenye manufaa makubwa katika nchi. Michezo inajenga afya pia inaleta uhusiano mwema kati ya Mataifa duniani. Taifa letu limekuwa likidorora sana kwenye sekta ya michezo yote hasa ya mpira wa miguu, hii ni kutokana na matayarisho mabovu katika kuwapata wachezaji wa mpira. Ushauri wangu katika hili ni kuwa, ni vyema Serikali ikaweka sera maalum na endelevu ya kuwapata wachezaji. Ni vyema kuwa na timu ya kudumu ya na siyo kuendelea na utaratibu wa sasa ambao wachezaji hukusanywa pale tu wanapohitajika na kuruhusiwa kuondoka baada ya kumaliza mchezo husika, hali hii siyo ya tija hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili katika kuwapata wachezaji walio bora ni Serikali ingekuwa na utaratibu maalum wa kuweka somo la michezo katika shule maalum ya michezo. Hii ingerahisisha kuwapata wachezaji wenye viwango ambao watakuwa wameandaliwa kuanzia udogoni (watoto wenye umri mdogo).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iwe na mikakati kabambe ya kuimarisha michezo ili kuibua vipaji vya wanasoka nchini. *Academics* za mpira zianzishwe katika maeneo mbalimbali nchini kwa ushirikiano wa Serikali na wadau mbalimbali wa soka. Vijana wakijifunza mpira katika *academy* zitakazoanzishwa watajifunza soka na michezo mingine wakiwa bado wadogo. Kujifunza soka ukiwa mdogo unapata uzoefu wa kutosha na hivyo kuna uwezekano wa kucheza soka la kulipwa baadaye. Hivi ndivyo nchi nyingi zenye mafanikio makubwa ya soka duniani zinavyofanya.

Mheshimiwa Spika, pia Shirika la Utangazaji la *TBC* lizingatie weledi katika ufanyaji kazi. Mfano, kuna muda Shirika hili linajisahau na kutangaza habari za Serikali na Chama cha Mapinduzi na kupuuza habari za Vyama vya

Upinzani. Kwa kuwa Shirika hili linaendeshwa kwa kodi za Watanzania wote hivyo ni jambo jema Shirika hili likaacha ubaguzi katika kutoa na kutangaza habari.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vya habari Tanzania umeendelea kupotea siku hadi siku. Yapo baadhi ya matukio ya hivi karibuni yamethibitisha kupotea kwa uhuru wa vyombo vya habari mfano; kuvamiwa kwa *studio* za *clouds TV* na *Radio* siku za hivi karibuni na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Tukio hilo limeishusha sana nchi yetu katika utekelezaji wa uhuru wa vyombo vya habari, pia limeichafua sana nchi yetu duniani kote. Serikali ichukue hatua thabiti katika kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri pamoja na timu yake yote kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake nzuri iliyojaa matumaini ya kuinua Wizara hii katika Habari, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali yangu tukufu kuwekeza katika suala zima la michezo wala isichukulie mzaha kwani sekta hii ikisimamiwa vizuri itakuwa inaingiza mapato mengi katika Taifa letu pamoja na kutangaza utalii katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Lushoto, *Radio* ya Taifa haipatikani kabisa zaidi ya wananchi kusikiliza *Radio* za Kenya. Hivyo, naishauri Serikali yangu tukufu ijenge minara ya redio katika Wilaya ya Lushoto kwani wananchi wanakosa taarifa muhimu pamoja na mawasiliano muhimu ya kuhusu nchi yao pamoja na nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Lushoto kuna vijana wengi wana vipaji vya sanaa na michezo lakini vijana hawa wameachwa huko vijijini na kupoteza vipaji vyao. Kwa

hiyo, naiomba Serikali hasa Wizara ya Michezo itoe timu kwa ajili ya kwenda vijijini ili kwenda kuibua na kuwanusuru vijana ambao wana vipaji na kuwajengea uwezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Lushoto ni Wilaya kubwa ambayo ina vijana zaidi ya 250,000, lakini ndani ya Wilaya hakuna uwanja hata mmoja wa michezo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijenge uwanja wa michezo Lushoto Mjini. Pamoja na hayo, kujengwe Chuo cha sanaa katika Jimbo la Lushoto ili kuendeleza vipaji hivi vya vijana wetu hawa wa Kitanzania. Niishauri Serikali ifundishe michezo mashuleni pamoja na kupewa vifaa vya michezo katika shule zote.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali yangu tukufu kwa wale wote ambao wapo vijijini, wanamichezo pamoja na wasanii Serikali iwasaidie ili waweze kukuza vipaji vyao sambamba na kuwa na ajira kupitia kazi yao hiyo kwani wasanii wa vijijini wanapata tabu sana mwisho wa siku wanakata tamaa na kuiona Serikali yao haiwajali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanazozifanya. Mheshimiwa Waziri mna kazi kubwa ya kusimamia Taifa letu kuhakikisha mnajitahidi sana ili mila na desturi za nchi yetu na utamaduni wetu uendelee kubaki. Nasema hivi kwa kuona vijana wetu wanajiajiri kwa kuanzisha sanaa ya muziki huu wa kizazi kipya ambao baadhi yao hasa vijana wa kike huwa wanacheza wakiwa wana nguo ya ndani tu.

Mheshimiwa Spika, hivi Baraza la Sanaa la Taifa linaangalia maudhui ya nyimbo tu kama maneno yaliyotumika siyo au linawangalia kundi lote hata wachezaji? Kwani vijana wa kike baadhi yao wanatutia aibu sana. Mheshimiwa Waziri Wanawake tunadhalilika sana wakati mwingine unashindwa kuangalia TV ukiwa na watoto wako

wa kiume kuogopa itatokea hiyo nyimbo yenye vijana waliovaa vibaya, Watanzania sio Wazungu hata kama tunataka muziki ukue siyo hivi. Namwomba Waziri akemee vikali kwani mila na desturi za Watanzania ni hazina kubwa aliyotupa Mwenyezi Mungu, tusiwaachie watu watuharibie.

Mheshimiwa Spika, michezo ni jambo ambalo linalitangaza Taifa letu na Tanzania, kwa kweli tunajitahidi ila viwanja vya michezo Tanzania Bara ni kidogo. Ni muhimu kila vinapopimwa viwanja tukumbuke viwanja vya mpira kwani vipaji vya michezo vinaanzia vijijini Wizara ikishirikiana na Wizara ya Ardhi jambo la kutengwa viwanja vya michezo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja, hata hivyo yapo mambo machache yanahitaji maboresho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchezo wa mpira wa miguu ndiyo mchezo unaopendwa sana duniani kote, uongozi wa *TFF* unasababisha matatizo makubwa kwa makundi mbalimbali ya wapenzi wa mpira wa miguu hususan pale wanaposhindwa kusimamia haki za vilabu vya mpira na wanachama wake kwa kupotosha maamuzi yanayolenga kufanya upendeleo, kunyima haki na kuonesha kuegemea upande fulani. Jambo hili ni aibu, tunahitaji viongozi walio juu ya ubinafsi na upendeleo wowote kwenye maamuzi yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni viwanja vya mpira wa miguu. Upo utaratibu wa *TFF* kutumia msaada wa *FIFA* unaotolewa kwa wanachama wake kuweka nyasi za bandia kwenye viwanja vinayoteuliwa. Ni busara kuweka utaratibu mzuri wa viwanja gani tunadhani vianze kuwekewa nyasi hizi kabla ya kufikiria labda viongozi wetu *TFF* wanapeleka nyasi bandia katika mikoa wanayotoka. Viwanja vya mpira vya Jamhuri Dodoma, Jamhuri Morogoro, Majimaji Songea vingestahili kuwekewa nyasi za bandia kwanza kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunahitaji viongozi wa *TFF* wasio na upendeleo wa ovyo ovyo. Nchi hii yetu wote, wote tunayo haki sawa, ni vema viongozi wawe watenda haki kwa wanaowaongoza. Kwenye mpira wa miguu *TFF* ni tatizo, wajirekebishe.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali na Wizara kwa ujumla katika juhudi zake za kuendeleza michezo, sanaa na utamaduni nchini. Serikali iweke mkazo zaidi katika kuipa nguvu lugha ya Kiswahili kwa kutumia lugha hii katika shughuli na hafla mbalimbali za kitaifa na kimataifa ili lugha yetu hii iweze kuongeza idadi ya watumiaji na pia kuongeza soko la ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, utamaduni; Serikali iendelee na juhudi za kutoa elimu kwa wananchi juu ya mila potofu zinazoathiri afya za wananchi. Serikali iendelee na juhudi za kutoa elimu kwa wananchi juu ya tamaduni zinazokandamiza wanawake, watoto na jamii kwa ujumla. Wasanii wapewe elimu ili wasiitumie sanaa kudhalilisha wanawake kwa mavazi yasiyoendana na maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, *TBC* iongezewe nguvu ya vitendea kazi, rasilimali fedha, watumishi wa kutosha ili redio na *TV* ziweze kusikika na kuonekana nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ina wajibu mkubwa wa kujenga Taifa linalohabarishwa, lililoshamiri kiutamaduni, lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri wa michezo. Hata hivyo, wajibu huu haujaweza kutekelezwa mpaka sasa na bajeti ya mwaka 2017/2018 haielekei kujenga msingi mzuri wa kuwezesha azma hiyo kutekelezwa ifikapo 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya Sekta ya Habari, Taifa linarudi nyuma kwenye kuwezesha

uhuru na haki kwa mujibu wa ibara ya 18 na 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na ibara ya 19 ya mkataba wa kimataifa wa haki za kiraia na kisiasa wa mwaka 1966 ambao Serikali imeridhia. Hivyo, Serikali ifanye marekebisho ya Sheria zote zilizotungwa katika Bunge la Kumi na Bunge la Kumi na Moja zenye kukwaza uhuru na haki wa/ya habari. Aidha, Waziri katika majumuisho aeleze hatua ambazo Serikali imechukua kwa viongozi na watendaji wa Serikali walioingilia uhuru wa habari ikiwemo juu ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuvamia *Clouds Media* akiwa na watu wenye silaha.

Maendeleo ya utamaduni wa nchi yetu yanategemea sana ukuaji wa lugha ya Kiswahili na matumizi yake. Katika majumuisho Wizara ieleze Serikali imefikia hatua gani katika kuwezesha lugha ya Kiswahili kutumika katika ngazi zote za mahakama nchini. Aidha, Serikali inapoleta Miswada ya Sheria Bungeni inaleta Miswada hiyo kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili ambayo inafanya kisheria lugha rasmi ya sheria hizo kuwa Kiingereza, Wizara ishawishi katika Baraza la Mawaziri na ngazi zote za Serikali ili Miswada yote iletwe ikiwa katika lugha ya Kiswahili pekee.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika aya ya 45 ya Hotuba ya Waziri ukurasa wa 25 imetajwa Kamusi kuu mpya ya Kiswahili. Ni vyema Wabunge tukapatiwa nakala ya kamusi husika.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa *TFF* kuandaa vituo vya ufundi vitakavyokuwa na vifaa stahiki kila mkoa kwa madhumuni ya kulea vipaji ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya michezo. Hata hivyo, kwa Mkoa wa kiserikali wa Dar es Salaam idadi ya vijana wenye vipaji ni kubwa kwa mkakati kuweza kutekelezwa kwenye ngazi ya mkoa. Hivyo ni vyema mkakati huo ukatekelezwa kwenye ngazi ya Wilaya na nawasilisha rasmi ombi kwa *TFF* kwa kituo kuwekwa katika wilaya mpya ya Ubungo katika Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa maendeleo ya soka la wanawake, *TFF* itoe majibu kwa Wizara ni kwa kiwango gani imeifaidia timu ya Mburahati *Queens* ambayo inatoa wachezaji wengi kwenye timu ya Taifa ya wanawake kama ilivyoahidi kwa nyakati mbalimbali.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Dkt. Harrison Mwakyembe na timu nzima waliofanikisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, niipongeze timu yetu ya vijana chini ya umri wa miaka 17 kwa mafanikio na heshima kubwa inayoiletea Tanzania. Niiombe Serikali bila kujali matokeo ya mashindano yatakayofanyika Gabon baada ya mwezi huu, Serikali isiwatupe vijana hawa, kwani wameonesha uwezo na vipaji vya hali ya juu, kutokana na umri wao kuwa mdogo tuwekeze zaidi kwao na naona akina Samatta wengi kutoka kwa vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie shirikisho la mpira wa miguu Tanzania *(TFF)*; ni ukweli usio na shaka hali katika shirikisho hili sio nzuri, migogoro na malalamiko ambayo kwa kiasi kikubwa tulishaanza kuisahau wakati wa uongozi uliopita chini ya Rais Leodgar Chills Tenga kwa sasa imerudi kwa kasi sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri asimamie vizuri shirikisho hili na kwa kuwa watafanya uchaguzi mwaka huu wapate viongozi wazuri ambao wataipeleka Tanzania mbali kupitia mchezo huu wa soka.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*. Natambua Wizara hii inawajibika kwenye Wizara hii kupitia maudhui na usajili wa vyombo vya habari. Tumeshuhudia magazeti na vipindi vya runinga vinavyoenda nje ya maadili, tumeshuhudia magazeti yakiandika habari za uongo na uzushi dhidi ya viongozi, Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni muathirika wa jambo hili. Ushauri wangu, Serikali ichukue hatua kali ikiwa ni pamoja na kufungia maisha magazeti au Televisheni zinazothibitika kufanya vitendo hivi vya kuchafua majina ya watu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC);* usikivu wa *TBC* Redio upo chini ya asilimia 25 kwa nchi nzima, niiombe Serikali iongeze bajeti ya *TBC* ili iweze kuwekeza katika mitambo na kuongeza usikivu hadi vijijini ambapo ndipo wananchi walipo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nachangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo chetu cha *TBC* naomba kiimarishwe, hususan maeneo ya vijijini. Aidha, Redio ya Taifa na *TV – TBC* hazisikiki kabisa na *TV* za *TBC* muono wake sio mzuri. Kwa mfano, maeneo ya Tarafa ya Amani, Muheza yenye Kata za Mbomole, Misanai, Zirai, Kwezitu, Kweningoji na kadhalika Redio ya Taifa, *TBC,* haisikiki kabisa. Naomba mipango ifanyike kuimarisha sehemu hizo ili vyombo hivyo visikike na kuonekana.

Mheshimiwa Spika, wasanii wanafanya kazi kubwa lakini inaonekana haki zao *(copyright)* hawazipati kama inavyostahili; ni vizuri kuweka mikakati madhubuti ya kuwasaidia kupata haki zao. Aidha, wote wanaofanya uhalifu huu wakamatwe na kufikishwa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutungwa Sheria hivi karibuni ya Vyombo vya Habari, lakini maslahi ya waandishi wa habari hawapewi. Wapo waandishi wengi hawalipwi mishahara na wanaendelea kuwa vibarua. Suala hili liangaliwe kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Timu yetu ya *Serengeti Boys,* ni vizuri timu hii ikaangaliwa vizuri na isipoteze wachezaji hao ili baadaye wawe *Taifa Stars. Taifa Stars* imeshindwa kabisa kutuletea sifa katika nchi kwa sababu mbalimbali ikiwemo kutokuwa na kocha bora na wacheaji wengi wa Taifa wana umri mkubwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pia naomba kuchangia hoja katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari; kwa kuwa waandishi wa habari ni watu muhimu sana katika jamii kwa kuwa ndio wanaofanya kazi kuielimisha jamii katika Taifa letu, naiomba Serikali iweze kuwalinda na kuwapatia haki zao wanazowajibika kuzipata kama kuongezewa posho zao katika kazi wanazozifanya, kuwapatia vifaa vya kisasa na heshima yao ilindwe na wasidharauliwe. Kwa upande wa makazi na kadhalika, Serikali inatakiwa wawaongezee waandishi hao hasa wale wanaoonekana katika televisheni mbalimbali, waandishi wanatakiwa wapatiwe posho ya mavazi ili waweze kuonekana katika muonekano mzuri. Hili liangaliwe hasa kwa watangazaji wa *TV* ya Taifa *TBC.*

Mheshimiwa Spika, wasanii wa filamu waweze kupata haki zao ipasavyo kwa sababu wasanii wa Tanzania wanadharaulika sana na jamii inapendelea kuangalia au kununua kanda za filamu za nje. Naishauri Serikali kufuatilia ulipaji wa kodi kwa wafanyabiashara wanaoingiza kanda za filamu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, nidhamu katika kazi za muziki; ni mara nyingi tunaona wasanii wakiimba nyimbo zisizo na maadili na kuvaa mavazi yasiyo na maadili na hasa kwa wasanii wa kike. Naishauri Serikali isimamie vema maadili ya wasanii, hasa wa muziki katika nchi hii, vinginevyo tutafika pabaya. Nashauri wasanii wetu wasiige tabia za nje bali waangalie mila na desturi za Kitanzania.

Meshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Nitaanza na suala la utamaduni katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili inapewa kipaumbele cha juu katika nchi yetu, ni jambo jema. Ila napenda kuonesha hisia zangu katika Wizara hii kwa mustakabali wa Taifa hili kwa kuwa lugha ya Kiingereza imekuwa ikitumika maeneo mengi katika Serikali yetu, mfano *interviews* za kuomba kazi hufanywa kwa lugha ya Kiingereza, hotuba na mawasiliano mengi hufanywa kwa lugha ya Kiingereza, ukienda kwenye suala la biashara za kimataifa kati ya nchi na nchi kwa wafanyabiashara wetu na wa nje hufanywa kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wangu ningeomba pamoja na kutumia Kiswahili, bado nchi yetu haijaweza kujitegemea kama nchi za Kichina wanavyoweza kutumia lugha yao ya ndani. Hivyo basi, kwa kuwa bado tunategemeana na nchi nyingine kiuchumi, bado tunahitaji kufundisha lugha za Kiswahili na Kiingereza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, michezo; kwa kutambua umuhimu wa michezo katika Taifa letu, kuwa michezo ni afya, ajira, mahusiano na pia kutangaza Taifa letu kitalii, bado tuko nyuma sana kwa kutumia michezo yetu kwa manufaa ya Taifa hili. Nashauri Wizara kuwa na *Sports Academy* kila kanda kwa nchi yetu ili kuweza kuinua vipaji vya vijana wetu mpaka kwenye ngazi za chini.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wadau mbalimbali kwa kutumia michezo kupeleka ujumbe wa jamii, lakini kama Wizara, tunaomba michezo itumike vizuri katika kuitangaza nchi yetu lakini pia kupinga vitendo mbalimbali vya kurudisha nyuma maendeleo ya nchi, mfano, kupinga ujangili wa tembo kupitia michezo, kupinga utumiaji wa dawa za kulevya na kupinga ndoa za utotoni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, michezo kupitia utalii. Michezo ni kiunganishi kikubwa cha nchi na nchi kupitia vivutio vya utalii wetu. Nasema hivyo kwa sababu leo ukitaja Timu ya *Arsenal* unataja nchi ya Uingereza. Kwa Taifa letu bado hatujafika kuwa na Timu ya Taifa ambayo inaweza kuitangaza nchi yetu

kiutalii. Hata *Serengeti Boys* ambayo inabeba jina kubwa la Hifadhi ya Serengeti, haijaweza kutangaza hifadhi yetu hata kwa hadhi ya nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri Wizara kuwasaidia vijana wenye vipaji vya michezo ili kuitangaza nchi yetu. Limekuwa ni jambo la kawaida kuona mchezaji amejitahidi na kufika kiwango kikubwa ndiyo Wizara inamtambua. Nashauri vipaji vya vijana wetu vianzie shule za msingi ili waweze kusaidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nimehudhuria *Kilimanjaro Marathon,* Mkoa wa Kilimanjaro na nilikimbia mbio za kilometa tano, kilichoniumiza ni kuona washindi waliopatikana ni kutoka nchi ya jirani ya Kenya. Hii inanipa tabu sana hata kutangaza Mlima Kilimanjaro kupitia mashindano hayo muhimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kupitia Wizara ijifunze kuanzisha mashindano kama haya ambayo kwa sasa yanafanywa na wadau ili kuweza kuandaa vijana wetu mapema, hasa kutumia Jeshi letu ambalo pia lina nidhamu na vijana wengi. Vilevile, kama tunavyojua michezo ni ajira, tunaweza kuajiri vijana wengi kupitia michezo. Hii itarudisha nidhamu ya michezo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, taasisi nyingi za Serikali ziliajiri wanamichezo wengi kuwa watumishi, mfano mzuri ni *TANAPA,* iliajiri watumishi wengi wanamichezo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Dkt. Harrison Mwakyembe Waziri, Naibu Waziri Anastazia Wambura, Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba hapa Bungeni ili tuijadili. Yapo mambo ambayo nahitaji kuyachangia ambayo ni:

Moja, ufinyu wa Bajeti; siku zote Wizara hii imekuwa ikipatiwa bajeti finyu sana na kusababisha Wizara hii kufanya kazi zake katika wakati mgumu sana na mbaya zaidi pamoja na kupatiwa bajeti kidogo lakini hata bajeti iliyopangwa haipelekwi kwa wakati hivyo kusababisha Miradi mingi

iliyopangwa kutokamilika kwa wakati. Ni vema Wizara hii ingepewa kipaumbele kwa sababu pia imekuwa ikifanya kazi ya vijana wetu inayohusiana na sanaa.

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa viwanja vya michezo katika Halmashauri, vijana wetu wanakosa haki yao ya msingi kutokana na uvamizi uliofanywa katika viwanja vilivyoachwa wazi kwa ajili ya michezo kuvamiwa na kugawiwa kwa watu kujenga. Nakumbuka Serikali ilitoa tamko kuwa waliovamia viwanja vya wazi waondolewe lakini mpaka leo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Serikali kwa ajili ya jambo hilo. Hivyo, ningependa kupatiwa ufafanuzi wa agizo hilo la Serikali sababu vijana wengi hawana maeneo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, Vazi la Taifa; ningependa kujua mpango wa Serikali kuhusiana na vazi la Taifa, nakumbuka Serikali ya Awamu ya Nne ilishawahi kutuletea taarifa kuhusiana na mchakato wa kupata vazi hilo lakini mwisho wake mpaka leo hatujui limefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, *(TBC)* Shirika la Utangazaji la Taifa; naomba Serikali ifanye jitihada za kutosha kuhakikisha *TBC* inapatiwa pesa ya kutosha ili iweze kusikika nchi nzima. Tunasikia vibaya kuona maeneo ya mipakani wanapata mawasiliano toka nchi jirani. Pia vitendea kazi viboreshwe viendane na hadhi ya chombo cha Serikali.

Mheshimiwa Spika, watu wenye ulemavu; naomba Serikali iwatendee haki watu wenye ulemavu kwa kuweka Sheria ya kuhakikisha wamiliki wote wenye *Television* wanaweka watafsiri wa lugha katika *Television* ili watu wenye ulemavu wa kusikia nao waweze kuona. Pia itawasaidia kupata ajira kwa watu waliosomea kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, michezo ya UMISETA; naiomba Serikali yetu iweke kipaumbele kikubwa sana katika kutenga pesa kwa ajili ya michezo hiyo ili tuweze kuibua vipaji vya watoto wetu ili tuviendeleze kwa ajili ya kusaidia nchi hii kwa upande wa maendeleo ya michezo. Michezo ni ajira, michezo ni afya na michezo inajenga mahusiano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, habari; *TBC* mitambo iboreshwe, kuwa na uwezo wa kusikika nchi nzima hasa redio ambayo ni ya Taifa lakini haisikiki nchi nzima hasa wilaya na mikoa ya pembezoni kama Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Spika, *TBC (TV*) mitambo yake ni chakavu iboreshwe. Vyombo vya habari kutokuwa huru; uwepo uhuru wa vyombo vya habari kama redio *TV,* Magazeti na kadhalika. Kuna fununu kuwa Serikali ina mpango wa kuzuia *TV* na redio kusoma magazeti asubuhi kwa Watanzania (yaani tuongee magazeti). Hii itazuia Watanzania wengi sana kukosa hata ile haki ya kujua nini kiko kwenye magazeti hasa kule ambako magazeti hayafiki kama Kakonko.

Mheshimiwa Spika, mitambo ya redio Kakonko/ Kibondo kutojengwa wakati bajeti ya 2016/2017 ilipitisha bajeti ya kujenga *TBC* redio *boster*. Mitambo hiyo haijajengwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, michezo; tuandae michezo kuanzia shule za msingi/awali, sekondari, vyuo, na kadhalika. Hii itatengeneza *"Pool"* ya wachezaji watakaounda timu za kitaifa. Serikali itenge bajeti ya michezo hasa mpira wa miguu ili timu za kitaifa kama Serengeti *boys* zinapofanya vizuri ziweze kupewa fedha.

Mheshimiwa Spika, sanaa; chuo cha sanaa Bagamoyo kipewe fedha za kutosha ili kujiendesha na kiboreshe miundombinu yake kama *studio* ya kisasa. Serikali ilinde haki za wasanii pamoja na kupewa haki miliki lakini kazi zao bado zinaibiwa.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, michezo mashuleni; napenda kuishauri Serikali kuhakikisha inafufua michezo na utamaduni

mashuleni kama ilivyokuwa ikifanyika huko nyuma. Kwani awali kulikuwa na michezo mashuleni kama mpira, kukimbia, kurusha tufe, kuruka kamba na mambo kama hayo. Pia kulikuwa na ngoma za makabila mbalimbali na hizo zilikuwa zina mafunzo mazuri kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, *TBC*. Naomba kuishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuinusuru *TBC,* kwani *TBC* iko katika hali mbaya sana. Naomba maslahi ya wafanyakazi wa *TBC* yaangaliwe .

Mheshimiwa Spika, wasanii; naomba kuishauri Serikali kuheshimu kazi za wasanii na kuwasaidia katika kupitisha kazi zao bila kuchukua hatua ndefu za uandaaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA); Taasisi hiyo ndio inayoandaa wakuzaji wa sanaa, wasanii, waendeshaji na wasimamizi wa shughuli za sanaa, lakini bajeti inayotengewa ni ndogo na haiendi kwa wakati. Naomba Serikali ipeleke bajeti inayoidhinishwa na Bunge na ipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, usalama wa waandishi wa habari. Waandishi wa habari wanaishi katika hali ya wasiwasi, naiomba Serikali ione namna ya kuwalinda waandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa maandishi Wizara hii. Kwanza nianze kwa kutoa pole kwa familia ya watoto na Walimu pamoja na dereva wa basi lililopata ajali Wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha. Nitoe pole za dhati ya moyo wangu kwa kweli inasikitisha sana tena sana na kutia uchungu, kikubwa kazi ya Mungu haina makosa. Tuombe roho za marehemu ziwekwe mahala pema peponi amina.

Mheshimiwa Spika, pili nimpe pongezi mzee wangu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa kuendelea kuaminiwa

na Mheshimiwa Rais kupewa Wizara hii ya Michezo, Habari na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, wilaya nyingi nchini hazina viwanja vya michezo ya *football, netball, basketball* na kadhalika, lakini kuna mikoa hapa nchini ina historia ya kutoa wachezaji bora na wasanii bora kama Mkoa wa Kigoma ninaotokea mimi.

Mheshimiwa Spika, cha kunishangaza ni kuona *TFF* wanajenga viwanja Mwanza na kuacha kuboresha viwanja vya Lake Tanganyika na Wilaya ya Kigoma ili kuwaenzi wachezaji wa zamani kama kina Sande Manara, Katwila, kina Mambo sasa, Kitwana Manara na wengine na hata kina Mizani Khalfan kina Juma Kaseja na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu suala la wasanii wa muziki wa kizazi kipya kama kina Diamond, Ali Kiba, Omari Dimpozi, Banana Zoro, Maunda Zoro, Juma Nature na kadhalika wote hawa wanatoka Kigoma.

Mheshimiwa Spika, inaashiria kuwa Mkoa wa Kigoma ni mkoa unaotoa vipaji vya kila aina. Tunachoomba Serikali ni kuona namna ya kuwasaidia wasanii hawa kuwa na hati miliki ili waweze kunufaika na vipaji vyao vya asili kuliko kama ilivyo sasa msanii anatunga yeye, anaimba yeye, anayenufaika ni mwingine.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nizungumzie suala la utamaduni; tuombe Serikali kupitia Wizara hii kurudisha ngoma za asili mashuleni ili basi tuweze kuenzi ngoma zetu za asili. Kupitia mashuleni sherehe mbalimbali za kitaifa, sherehe za mikoani na wilayani kuwa na utaratibu wa kualika ngoma za asili ili kutunza tamaduni zetu za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kukuza michezo mashuleni kwa kurejesha kwa nguvu kubwa michezo ya UMISETA ili kuanza kuibua michezo mashuleni na hatimaye watoto wakue na vipaji vyao.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la *TBC;* hali ya huko vijijini *TBC* haisikiki kabisa tuombe Serikali kupitia Wizara hii ione namna gani ya kuboresha vitendea kazi ili waweze kufanya kazi yao ya kutoa huduma kwa watanzania wote hususan kwa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, niongelee pia suala la mchezo wa kuogelea kuna tatizo la mchezo wa kuogelea pale ambapo tunaacha kwenda kuibua vipaji kwenye wilaya zenye maziwa kama vile Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria, hebu tushauri Serikali kuibua vipaji kwenye maeneo hayo kwani watoto wengi hujua kuogelea vizuri. Tukiwapa mafunzo ya kuogelea kwenye *swimming pool* wanaweza kufanya vizuri na kuiletea ushindi nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie lugha ya Kiswahili; kuna tatizo kubwa la nchi za nje kama *USA*, *Holland*, *UK*, na kadhalika watu wa *DRC* na Kenya ndio wanaofundisha Kiswahili kwenye vyuo vikuu vya nchi mbalimbali, kwa nini Serikali isiwaandae Walimu wa Kitanzania wanaochukua somo la Kiswahili na Kiingereza ili wawe na *degree* ya lugha tu na waweze kuthubutu kwenda nje kufundisha lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia Wizara hii kwa kumpongeza kwa kuteuliwa kushika wadhifa wa Uwaziri katika Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo, natambua kuwa majukumu yaliyopo katika Wizara hii ni makubwa mno kutokana na ukweli kwamba Wizara hii inagusa furaha za Watanzania wengi kupitia michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishauri kufanya marekebisho katika kanuni za ligi kuu ya *Vodacom* kwa kuondosha kanuni inayoipa timu iliyoshindwa uwanjani ushindi eti kwa kigezo cha timu shindani kumchezesha mchezaji mwenye kadi za njano tatu. Kanuni hii imepitwa

na wakati na nchi nyingi duniani wameiboresha kwa kubakisha *point* kwa timu iliyoshinda na ile timu ilivyotumia mchezaji mwenye kadi tatu za njano huadhibiwa kwa kutozwa faini na mchezaji husika kupigwa faini pia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri jambo lingine ni lugha ya Kiswahili; lugha hii ni miongoni mwa urithi ambao tuliopo leo tumerithi na hatuna budi na sisi kurithisha kizazi kijacho. Lugha ya Kiswahili ni alama muhimu isiyo na shaka kabisa kuwa inalitangaza Taifa letu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kuandaa mipango madhubuti ya kukilinda na kukienzi Kiswahili kwani Serikali haijengi chuo maalum cha kufundisha Kiswahili pekee. Chuo hiki kitafanya kazi kubwa ya kukienzi Kiswahili kwa kufundisha masomo mahususi yanayohusu Kiswahili tu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Kiswahili kisitumike kama lugha ya kufundishia na kujifunzia kwa elimu ya sekondari na vyuo hapa nchini. Kitendo cha kuendelea kukitumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika masomo ya elimu ya juu ni kuendelea kuwa watumwa wa kikoloni. Nashauri lugha ya Kiswahili iwe ndio lugha rasmi ya kufundishia na kujifunzia katika masomo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu uozo uliopo *TFF* na Vyama vya Mpira vya Mikoa na Wilaya. *TFF* imetawaliwa na watu wanaosimamia maslahi yao binafsi badala ya mpira wa miguu. Kwa nini kila kukicha utasikia stori za magari ya Timu ya Taifa kuzuiwa hotelini au *TRA*. Hizi habari za *TFF* kudaiwa na *TRA* pamoja na hoteli ambazo timu zetu zinaweka kambi ni dalili za wazi kuwa *TFF* wana upungufu katika utendaji kazi wao. Mfumo wa usimba na uyanga uliokithiri pale *TFF* ni adui kwa maendeleo ya soka nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kutorushwa mubashara kwa matangazo ya Bunge. Jambo hili ni kinyume kabisa na katiba ya nchi yetu inayotoa haki ya Watanzania kupata taarifa na habari hususan za Bunge ambapo wawakilishi wao wanawasemea wao lakini kwa bahati

mbaya wananchi hawaoni jinsi wawakilishi wao wanavyofanya kazi walizowatuma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri jambo lingine ni kuhusu *Ciber Crime Act.* Sheria hii imekuwa ikitekelezwa kwa wananchi ambao wana mlengo mmoja tu wa kisiasa (Wapinzani). Katika wingi wa vijana waliowahi kushtakiwa na kuhukumiwa wote ni aidha CHADEMA au *CUF*, kwa nini vijana wa CCM ambao kila kukicha wanaendelea kutoa maneno ya kejeli na matusi kwa viongozi wa upinzani lakini hakuna hata mtu mmoja aliyewahi kukamatwa na kufikishwa mahakamani. Tunaomba Serikali iache kutekeleza usimamizi wa sheria ya mtandao kwa ubaguzi wa itikadi za kisiasa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya maana Wizara hii ina mambo mengi mno.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee wakalimani wa lugha ya alama kwa viziwi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aseme kitu kuhusiana na hili maana Watanzania hawa wako njia panda na hawaelewi kinachondelea. Namwomba sana Mheshimiwa aseme kitu Watanzania viziwi wapone maana wako gizani, wanakosa habari nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee katazo la uchambuzi wa magazeti kwenye redio na televisheni. Nampongeza Waziri kwa katazo hili naelewa kuwa ameangalia maslahi ya wafanyabiashara ila amepitiwa kuangalia makundi mengine hasa wasioona wote Tanzania. Ikumbukwe kuwa uwezo wa kuchapisha nukta nundu kwenye magazeti haupo na ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri; kuliko kuendelea kuwaweka gizani Watanzania hawa wasioona kwa kukataza uchambuzi wa magazeti. Naomba Serikali ije na njia ya jinsi gani Watanzania hawa watapata hizi habari ndipo hili katazo liendelee.

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa; mchakato ulishaanza umefikia wapi? Naomba ufafanuzi wa hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa afya njema aliyonijalia. Nitumie fursa hii kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri yenye mipango yenye kuleta matumaini kwa wasanii, wanahabari na wanamichezo.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nianze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kumekuwa na changamoto kubwa ya watoto wa Kitanzania kutokua na ushiriki mkubwa katika michezo. Hivvyo, basi tumekuwa tukijenga Taifa lisilo na hamasa ya michezo. Hivyo basi, nipende kuishauri Serikali kufanya jitihada za kurudisha michezo mashuleni ambayo itaweka wanafunzi katika hali ya kuepuka hata vishawishi. Sambamba na hili, Serikali pia irudishe ushiriki wa wanafunzi katika sanaa na utamaduni kama hapo zamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukosefu wa timu za kushiriki katika michezo kama *volleyball, handball, badminton, table tennis* na kadhalika ambayo Tanzania kama Taifa tumekua tukijisahau na kuelekeza nguvu nyingi katika baadhi ya michezo kama mpira wa miguu. Naiomba Serikali iwezeshe ukuaji wa michezo ya aina yote kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha makumbusho cha Bujora. Hiki ni kituo cha makumbusho ya kabila la Kisukuma kilichopo Mwanza, Wilaya ya Magu. Kituo hiki kimepoteza umaarufu wa hadhi yake hata kupelekea upungufu wa watalii wa nje na ndani kulingana na miaka ya nyuma. Bujora Sukuma *Museum* inahitaji fedha ili kuweza kuimarishwa na kukarabatiwa kurudi katika ubora wake.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, naiomba Serikali kulisimamia suala hili kwa ukaribu ili kituo hicho kiimarike na

kwa kufanya hivyo tutaongoza utalii ndani ya Mkoa wa Mwanza na kwa ujumla Serikali itapata kuongoza ukusanyaji kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu mfupi, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia machache katika Wizara hii. Nianze kwa kutoa pole kwa msiba mkubwa tulioupata katika nchi yetu kwa ajali iliyotokea katika Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, utamaduni; nchi yetu imebarikiwa kuwa na makabila 126 na kila kabila lina mila na desturi zake na kwa pamoja ndiyo zinatengeneza utamaduni wetu. Ila bado vipo baadhi ya vitu katika tamaduni hizo ambavyo vinadhalilisha wanawake. Kwa mfano, ukeketaji, kutokutoa umiliki kwa wanawake na kurithi wanawake wanaofiwa na waume zao hata kama wanawake hao hawataki. Katika jambo hili la ukeketaji ngariba wameanza kutumia mbinu mpya ya kukeketa watoto wachanga, hili jambo ni baya sana. Mambo haya bado yanaendelea pamoja na kuwa na jitihada za kupiga vita mambo haya.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua katika bajeti hii Serikali ioneshe wazi itafanya nini kukomesha tamaduni na desturi hizi mbovu zinazomdhalilisha mwanamke na mtoto wa kike. Ufike wakati wa kuzirasimisha baadhi ya tamaduni katika mfumo rasmi ili kuziondoa zisizofaa.

Mheshimiwa Spika, michezo; kumekuwa na jitihada za kuhamasisha mpira wa miguu kwa vijana walio chini ya umri wa miaka 17, *Serengeti Boys,* lakini hakuna nguvu ya kutosha kuhamasisha uwekezaji kwenye mpira wa miguu na michezo mingine. Pamoja na timu hizi za *Serengeti Boys* na *Kilimanjaro Queens* kufanya vizuri, bado hazipewi kipaumbele cha kutosha wakati vipo vipaji na wana uwezo wa kufanya vizuri kimataifa na kwa sasa timu hizo zimeweza kufanya

vizuri katika michezo yao. Kwa mfano *Kilimanjaro Queens,* hawa ni wanawake, walichukua Kombe la Afrika Mashariki na Kati mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, ili timu zetu zifanye vizuri ni lazima tuwekeze tuwe na chanzo cha kuaminika cha kuwekeza pesa kwenye michezo na lazima kuwekeza na kuupa mwamko wa kutosha mpira wa miguu kwa akinamama. Umefika wakati sasa kuwe na chanzo cha kuaminika cha kuwekeza pesa kwenye michezo na njia rahisi wanayofanya duniani kote ni kupitia Bahati Nasibu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu Serikali haitengi pesa kwenye bajeti na hakuna njia ya kuupa pesa mchezo na mchezo wa bahati nasibu unasimamiwa na Wizara ya Fedha badala ya Wizara inayohusika na michezo. Nashauri bahati Nasibu ya Taifa iwe chini ya Wizara hii ili kiwe chanzo cha upatikanaji wa fedha katika michezo na kuwezesha timu zetu kushiriki katika mashindano.

Mheshimiwa Spika, habari, uhuru wa vyombo vya habari; sheria tuliyopitisha hapa Bungeni ina vipengele vinavyolalamika na ni vizuri Serikali ione haya na kuvipitia na ikaangalia namna ya kuvibadilisha ili kuweka uhuru wa vyombo vya habari wa kweli. Tumeona hivi karibuni vyombo vya habari vikivamiwa na viongozi wakiwa kwenye maeneo yao ya kazi, tumeona kwenye vyombo vya habari wanahabari wamepigwa wakiwa wanatekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maadili na utamaduni wa Mtanzania; maadili na utamaduni wa Mtanzania yameendelea kuporomoka siku hadi siku kutokana na

mambo mengi ikiwemo ukuaji wa teknolojia. Watu walio wengi, hasa vijana, wamekuwa wakikosa maadili mema kwa kuangalia au kuiga mila na tamaduni za nje ya nchi. Baadhi ya watoto wamekosa heshima kwa wakubwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutunza mila nzuri na tamaduni zetu kwa kuchukua hatua pale panapotokea ukiukwaji wa mila na desturi, wazazi pia wanapaswa kuangalia maadili ya watoto wao. Elimu kuhusu utunzaji wa mila na desturi itolewe katika jamii. Tunahitaji Tanzania yenye Watanzania walio na maadili mema.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa viwanja vya michezo; viwanja vingi katika mikoa mbalimbali havikidhi vigezo vya kuwa viwanja vya michezo, hasa vile vinavyomilikiwa na CCM. Katika Mkoa wa Iringa, Uwanja wa Samora Machel umejengwa maghala ndani yake na kusababisha uharibifu pamoja na kuharibu lengo la kuwa na uwanja huo. Napendekeza kuwa Serikali, kupitia Wizara, iwashirikishe Sekta Binafsi ili kuendeleza viwanja hivyo hasa Uwanja wa Samora Machel Mjini Iringa ili kuweza kuinua kiwango cha michezo. Serikali pia ijenge viwanja vipya vya michezo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Sanaa Bagamoyo; wananchi walio wengi, hasa vijana, wamekuwa wakijishughulisha na sanaa. TASUBA ni chuo kinachotoa mafunzo ya sanaa lakini miundombinu yake haikidhi mahitaji. Katika fedha waliyotengewa Bajeti 2016/2017, milioni 300, wamepata milioni 100 tu, sawa na 5.6%. Nashauri Serikali iweze kuwamalizia kiasi cha fedha kilichobakia kwani chuo hiki ni tegemeo la vijana wengi kupata ujuzi ili wajitegemee kimaisha.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa kupata habari; kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasisitiza kuwa wananchi wanao uhuru wa kupata habari, Serikali imezuia wananchi kupata habari za Bunge *Live.* Naishauri Serikali isiwe na woga wa kukosolewa kwani ni afya kwa Taifa na watajipanga kuweza kutekeleza majukumu

yao. Niiombe Serikali iruhusu uhuru wa vyombo vya habari ili wananchi wapate haki yao.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kuweka mikakati mizuri na endelevu ya kuinua vipaji katika michezo kuanzia vijana wa miaka 13. Hii itatuhakikishia kupata wanamichezo mahiri wa kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, rai yangu; michezo hii iwe ya aina mbalimbali sio soka na *netball* peke yake bali izingatie riadha na michezo mingine. Timu hizi zizingatie jinsia ili kupata vijana wa kike na wa kiume katika michezo. Timu zizingatie watu wanaoishi na ulemavu na kuwawezesha. Suala la michezo ya wanawake halijapata kushughulikiwa ipasavyo na Serikali.

Mheshimiwa Spika, michezo mingi ni ile ya *netball* lakini wanawake wana uwezo wa kushiriki katika kila mchezo lakini hawawezeshwi. Kwa mfano, sasa hivi Timu ya Mpira ya Wanawake ya Chalinze ndio mabingwa wa Taifa lakini hawana uwezeshwaji na wamekwama kuendelea na mazoezi na hivyo kuhujumu fursa zilizopo mbele yao. Tunaiomba Serikali iwahudumie hawa wachezaji wa Timu hii ya Wanawake ya Chalinze badala ya kumuachia Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete peke yake. Serikali iweke mkakati wa kujumuisha wanawake katika maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, utamaduni; Serikali izingatie tamaduni zilizopo Tanzania na kuzifanyia kazi zile ambazo zinajenga heshima na maadili mema na kuzidumisha kwa kuzifundisha shuleni na kwenye sherehe mbalimbali, wakati huo huo wakiwaasa wananchi dhidi ya mila na tamaduni zinazodhalilisha watu kijinsia, kidini na kikabila.

Mheshimiwa Spika, ngoma zetu zidumishwe lakini wachezaji wavae nguo za heshima wakati wa kucheza, sio lazima watu wawe nusu uchi. Wizara ifanye kazi na Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Spika, kuunganisha juhudi za Wabunge na Serikali; Wabunge wengi wamekuwa wakitoa jezi na vifaa vingine vya kuwezesha michezo majimboni lakini wamekuwa wakifanya hivyo katika mazingira magumu maana majimbo yetu hayana viwanja vizuri vya michezo na hata baada ya kupata timu nzuri au wachezaji wazuri, hakuna mwendelezo maana hatuna Maafisa Michezo kwa hiyo usimamizi ni mgumu. Tunaomba Wizara itupatie utaratibu mzuri wa kuibua vipaji kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, majimbo yaliyopo kwenye maeneo ya milima yana uwezekano mkubwa ya kuzalisha wanariadha. Tunaomba maafisa michezo na vifaa vya kusaidia hilo.

Mheshimiwa Spika, kushirikisha Sekta Binafsi; michezo ni biashara kwa hiyo Serikali ifanye tathmini ya namna ya kushirikisha Sekta Binafsi, sio kufadhili timu ili kujitangaza bali kuwa na timu kikamilifu, kuajiri makocha, kufadhili viwanja vya michezo na kuziendesha ili Serikali ibaki kuweka mazingira mazuri kisheria na kisera. Serikali iwezeshe kutafuta wenye vipaji watakaochukuliwa na Sekta Binafsi kwenye timu za michezo mbalimbali, kwa mfano, Serikali itenge fedha ya kusomesha Maafisa Michezo vyuo vikuu, Makocha, Walimu wa Michezo, Waongoza Filamu, wataalam wa sanaa na utamaduni na filamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia maliasili zetu katika uwekezaji katika filamu, watengenezwe maeneo ya mbuga zetu, miji yetu, vijiji vyetu, milima yetu, maziwa yetu, mito na bahari na kutoa leseni/ vibali, hatimiliki kwa ajili ya kuja kutengenezea filamu. Hii itauza nchi yetu na kuviweka kwenye ramani ya medani za filamu nchini, vilevile inawezesha Watanzania kuajiriwa kwenye filamu na *documentary* hizi, wakati huo huo wakilipatia Taifa kipato kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuona jinsi hili litakavyofanywa. Nchi

yetu ilishawahi kutumika kutengeneza filamu lakini ilikuwa kabla ya uhuru lakini sasa mazingira ni mazuri zaidi, kwa hiyo Wizara itumie fursa hii kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, magazeti na *TV;* Tanzania ina uhuru uliopitiliza wa habari kwa maoni yangu na kwa kweli kuwa na magazeti mengi sio tu kueleza lakini ni chanzo cha matatizo mengi yanayotokana na tasnia hii ya uandishi maana uandishi wa vyombo vyetu vingi hauridhishi hata kidogo. Kwanza ni lugha inayotumika, utafiti mdogo ungefanywa kwenye mambo mengi ya kiuchumi, kisayansi, kiteknolojia na kijamii. Wote wanaandika taarifa za kuambiwa, hakuna anayefanya utafiti na kutoa ripoti inayofundisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, waandishi wetu wengi hawana ujuzi wa kutosha kwenye uandishi wa taaluma kiasi kwamba wawe wamebobea katika fani maalum. Suala la kuandika makala yasiyofanyiwa utafiti linaleta usumbufu, udhalilishaji na maumivu kwa wananchi wengi na hii haikubaliki. Tunaitaka Serikali ichukue hatua kali za kisheria kukomesha hili huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Sanaa za Ufundi ndio yenye ushiriki mkubwa wa Wasanii kuliko sanaa nyingine nchini Tanzania. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na BASATA 2006, idadi ya wasanii nchini ni milioni sita; zaidi ya milioni nne kati ya hao ni wale wanaojishughulisha na sanaa za ufundi wakiwemo, wachongaji, wachoraji, wachoraji katuni, tingatinga, wasusi, wabunifu wa mitindo, walimbwende na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali ikiwemo ya *(WIPO) Word Intellectual Property Organization* 2012), pia zinaonesha ni kiasi gani tasnia hii inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye ajira na pato la Taifa kuliko hata madini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango huo kwa Taifa, sanaa hii haipewi kipaumbele na Serikali, hivyo kudumaza maendeleo yake. Changamoto zifuatazo ni baadhi ya vikwazo vya maendeleo katika tasnia hasa sanaa ya uchoraji. Sheria kandamizi hasa kuporwa kwa maeneo mfano, kama ilivyokuwa katika maeneo mengine ikiwemo Nyumba ya Sanaa, sasa kumetokea watu wanaotaka kupora eneo la wachongaji Mwenge, eneo ambalo lilikabidhiwa Chama cha Wasanii Wachongaji Tanzania (CHAWASATA) na Serikali ya Awamu ya Kwanza mwaka 1984. Kufuatia kuhamishwa kutoka barabara ya Ali Hassan Mwinyi *Road* (Zamani Bagamoyo *Road*) ili kupisha upanuzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mshangao mkubwa wamejitokeza waporaji wenye nguvu za kifedha wanaoshirikiana na Kamishna wa Ardhi ili eneo lile lipewe watu wengine. Jitihada mbalimbali zimefanywa na chama cha CHAWATA ili kunusuru eneo hili lisiingie mikononi mwa wanyang'anyi ikiwemo kuomba msaada kwa vyombo vya umma ikiwemo BASATA ambao kwa barua yao ya hivi karibuni walisema jambo hilo haliwahusu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ituambie, nani anayehusika kufuatia hali hii tete ya sintofahamu. Hali ya amani katika Kijiji cha Mwenge Vinyago ni tete na wachongaji wasingependa kulazimishwa kuingia katika uvunjifu wa amani. Jamani, naomba suala hili lipatiwe majibu ili hali ya utulivu iendelee. Naomba sana Wizara hii ambayo iko chini ya Mwanasheria Dkt. Mwakyembe aliyebobea alisimamie hili kwa nguvu zote ili haki ya wachongaji hawa isipotee na wanamtegemea sana na wana imani na Waziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine kubwa inayokabili fani ya uchongaji ni watu wa Maliasili na Utalii ambao wamekuwa wakizuia vinyago visipite *Airport* hata kama vina stakabadhi halali za *TRA*. Hali hii imedumaza soko la vinyago toka asilimia 59 hadi asilimia 15 kitu ambacho ni hatari na hii ni fursa kwa majirani zetu hususan Kenya. Kupitia

Idara ya Sanaa, watu wa maliasili wameambiwa wakae nao ili kwa pamoja wajue na kufikia muafaka, lakini bila mafanikio. Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, pia kama ukifuatilia utendaji wa Mamlaka zingine hususan Tume ya Ushindani, bidhaa zote feki huwa zinachomwa zile zinazokamatwa tena hadharani, je vinyago vinavyokamatwa vinapelekwa wapi? Hatujawahi kuona vinateketezwa au kupigwa mnada ili kusaidia wenye mahitaji mbalimbali na kadhalika. Kuna tetesi kuwa, vinyago hivyo vinavyokamatwa pale *airport* hurudishwa Mwenge kwa mlango wa uwani. Naomba ukweli wa jambo hili na maelezo.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA**: Mheshimiwa Spika, michezo na hasa mpira wa miguu ni mchezo unaotoa ajira ya pesa nyingi kwa wiki au mwezi. Wapo wachezaji wengi duniani kutoka Afrika ambao wanalipwa mabilioni ya fedha kwa wiki mfano Samweli Eto wa Cameron na Didie Drogba wa *Ivory Coast.* Wizara ihakikishe inainua michezo kwa kuanzisha timu za vijana kila wilaya ili kutengeneza vipaji ambavyo vitaweza kupata ajira ya kucheza mpira wa kitaaluma ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Viwanja wa Michezo; ili michezo ikue lazima kuwe na viwanja vizuri vyenye ubora.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Michezo vya Kikanda; viwanja hivi ni muhimu kujengwa ili kuwe na uwiano katika nchi. Kanda ya Kusini ikiwa na uwanja pale Mtwara itachochea wananchi kupenda michezo na kuinua uchumi wa vijana na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, michezo mashuleni ndio chachu ya kuinua vipaji vya Watanzania. UMISETA na UMITASHUMTA iwekezwe ipasavyo. Wizara itenge pesa zipelekwe mashuleni badala ya kuwabebesha mzigo huu TAMISEMI peke yake na hata TAMISEMI hawapati pesa mashuleni kwa ajili ya michezo badala yake wanabebeshwa mizigo Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu mzigo ambao hawajatengewa bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, ili timu ya shule iende katika kituo cha tarafa au cha wilaya kilichotengwa kwa ajili ya michezo kuna gharama kubwa mfano chakula na gharama za wasimamizi. Wizara itenge pesa za UMISETA na UMITASHUMTA ili iweze kufanyika *effectively* maana kinachofanyika hivi sasa ni kuondoa lawama tu na sio *effective* kwa sababu haifanyiki kwa siku zinazotakiwa kwa kukwepa gharama.

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke siku maalum ya maonyesho ya ngoma za asili ambayo itafanyika kikata, wilaya, mkoa na kitaifa hii itasaidia kufufua utamaduni wetu nchini na pia kujitangaza kwa mataifa na baadaye kuingiza pato la Taifa kupitia utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, Mtwara na Lindi hakuna *frequency* za *TBC (television)* na zinapatikana kwa taabu sana. Naomba Wizara iweke mawimbi ya *Television* hizi Mtwara *(TBC1* na *TBC2)*. Mimi tangu *TBC2* imewekwa binafsi sijawahi kuiona na wala sijui inafananaje. Katika maeneo yote imefungwa isipokuwa Mtwara na Lindi tu.

Mheshimiwa Spika, si kweli, kwamba waandishi wanavamiwa nchini, isipokuwa waandishi wa habari wanapokuwa kazini wanaweza kupata ajali kama mfanyakazi yeyote yule na sio kama inavyodaiwa na baadhi ya Wabunge kwamba waandishi wanavamiwa.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi nzuri ya kuendeleza michezo na sanaa. Pia napenda kuwapongeza kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi uliotukuka na hasa kuhakikisha maendeleo mazuri ya Sekta ya Habari,

kuendeleza utamaduni, mila na desturi za Mtanzania, kuimarisha tija na kulinda kazi za sanaa na pia kuendeleza michezo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri za kusimamia shughuli za Serikali na kuhakikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama ilivyo kwa nchi zingine ina jukumu kubwa la utambulisho wa Taifa, kupitia Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Nchi yetu imesheheni vipaji mbalimbali na kinachohitajika ni kuibua hivi vipaji na kuviendeleza.

Mheshimiwa Spika, vipaji vingi vya michezo vipo vijijini na juhudi za makusudi zinahitajika kuibua vipaji vya michezo na sanaa huko vijijini ili viendelezwe. Michezo na sanaa ni ajira nzuri sana kwa dunia ya leo na pia ni utambulisho mzuri wa Taifa letu (*National brand*) na michezo pamoja na sanaa vinaleta heshima kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbeya Vijijini na hata Mkoa mzima wa Mbeya kuna vipaji vingi katika michezo hasa mpira wa miguu na riadha. Serikali ichukue hatua za makusudi za kimkakati wa kuibua hivi vipaji ikiwa ni pamoja na kuhimiza michezo mashuleni na kujenga viwanja vya michezo vijijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kipekee wa Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)* ambalo ni tegemeo la Watanzania walio wengi vijijini kupata habari mbalimbali kwa muda mrefu *TBC* haisikiki katika maeneo mengi vijijini na wananchi wanakosa fursa ya kupata habari. Pamoja na kutengewa bajeti ya shilingi bilioni moja katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, lakini ripoti ya Kamati inaonesha bado utekelezaji na pia kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na

mahitaji halisi ya uwekaji wa vyombo vya aina yake. Naungana na maoni ya Kamati ya kushauri Serikali kuwekeza vya kutosha katika Shirika la Utangazaji *(TBC)*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la wizi wa kazi za Wasanii wakiwemo waimbaji wa Injili, nashauri Serikali iweke mkakati wa kulinda kazi za wasanii ili waongeze kipato kwa kazi zao na pia mapato ya Serikali yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara husika kwa mwaka 2017/2018. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa katika Wizara hii. Pia nimpongeze Waziri pamoja na wataalam wake kwa kuandaa bajeti nzuri yenye mwelekeo chanya, bajeti hii ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze timu yetu ya *Serengeti Boys* kwa kuonesha mfano wa kufanya vizuri katika mechi zake zote, hii ni alama tosha na kuikumbusha Serikali kuwa mchezo wowote unahitaji uwekezaji kuanzia chini kwa maana ya kuanzisha vituo vya michezo na kukuza vipaji. Utaratibu huu umekuwa ukifanywa na nchi mbalimbali kama Ulaya, Amerika, Asia na Afrika ingawa sisi hatukuliona jambo hili kwa miaka ya hivi karibuni ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, michezo hivi sasa ni ajira ambapo imeajiri vijana wengi sana na wamekuwa wakinufaika kama akina Mbwana Samata ambaye anaiwakilisha nchi vizuri sana huko Ulaya. Hivyo, niishauri Serikali bado hatujachelewa tuwekeze katika michezo kwani kuna faida nyingi sana ambazo zitakwenda kutatua changamoto kwa mfano za ajira.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vyombo vya habari vimekuwa havifuati taratibu na sheria zilizowekwa. Hata Mheshimiwa Rais aliwahi kulisema hili kuwa baadhi ya vyombo vya habari vimekuwa vikivuka mipaka. Habari au uandishi kwa kuzungumzia hapa tunaweza kuona ni vitu vya kawaida tu lakini uandishi wa habari wa aina hasi unaweza kuliingiza Taifa katika machafuko makubwa sana. Mifano iko mingi sana ambayo vyanzo vya machafuko ni vyombo vya habari. Habari zinaenea kwa urahisi sana kuliko kitu chochote na sumu yake ni kali sana.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tunahitaji kuwa makini sana na vyombo vyetu vya habari ambavyo habari zake ziko katika malengo hasi, habari zake si za kujenga nchi, wala za kimaendeleo, tuviangalie vyombo ambavyo vinatoa kipaumbele kwa habari binafsi ambazo hazina tija kwa Taifa. Serikali sasa kupitia Wizara ni wakati wa kuchukua hatua kali bila woga wala aibu kwa chombo chochote cha habari ama iwe redio, magazeti au televisheni ambacho kinakiuka taratibu na sheria zilizowekwa. Vinginevyo tukivionea haya na nchi ikaingia katika machafuko kutokana na vyombo vya habari basi ni sisi viongozi ndiyo tutakuwa wa kulaumiwa kwa sababu tulipewa dhamana ya kuvisimamia lakini kwa utashi wetu tukashindwa.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia utamaduni huwa tunazungumzia tamaduni ya nchi au mahali husika. Sisi kama Taifa tuna tamaduni mbalimbali lakini tamaduni hizi tumekuwa tukiziona tu katika maadhimisho mbalimbali vikundi vikikaribishwa kucheza ngoma na kadhalika lakini hakuna mkakati madhubuti uliowekwa wa kuhakikisha tamaduni zetu zinadumishwa kwa namna yoyote na kuzitangaza. Tamaduni zetu ni fursa kama tukizitumia vizuri kwa sababu wageni watakuja kuziangalia na sisi tumejaliwa kuwa na makabila zaidi ya 100, hivyo tamaduni tunazo nyingi sana. Naishauri Serikali sasa kuchukua hatua katika sekta hii pia ili kuiwezesha kukua na kuleta manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, juzi Jijini Dar es Salaam wasanii wetu wa *Bongo Movie* waliandamana na dhumuni lao ni

kuzuia filamu za nje kutokuuzwa nchini na kuzipa kipaumbele filamu za kwao. Nina ushauri mzuri kupitia Wizara hii naamini utawafikia. Kuzuia filamu za nje sio utatuzi bali wasanii wetu wanatakiwa kuangalia ni wapi walipokosea mpaka soko lao likashuka. Bila kujua walipokosea na kujirekebisha haitakuwa suluhisho kwao kwani hata wakizuia hizo filamu za nje na zikabaki za kwao tu pia soko halitakuwa zuri.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamekuwa wakilalamika sana kuhusu ubora wa filamu za ndani kuanzia kwa waigizaji, vifaa wanavyotumia na matukio katika filamu zao. Ninavyofahamu, filamu haiwezi kutengenezwa kwa miezi miwili halafu ikawa tayari sokoni, ni ngumu kuingia katika ushindani wa soko la filamu hata tu la Afrika Mashariki. Hatuwezi ndugu zangu ni lazima tuishi kwa kujifunza, asiyetaka kujifunza lazima atakuwa na mawazo mgando.

Mheshimiwa Spika, hivyo tuwape elimu vijana wetu wa *Bongo Movie* kuacha kuharakisha filamu kwa miezi miwili au mitatu kuitoa sokoni huku ubora ukiwa finyu. Hakika wakibadilika watauza kwani hapo nyuma walikuwa wakifanya vizuri katika soko hili hili la filamu. Kama nilivyosema hapo awali ni wakati wao kujiuliza ni wapi walipokosea na kujipanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge, nina tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye anawatangazia kwamba leo Kamati yake ya Bajeti itakuwa inajadili Taarifa ya Utendaji wa *RAHCO* kuhusu ujenzi wa reli ya Tanga- Arusha- Musoma ambayo ni ya kiwango cha *standard gauge.* Kwa hiyo, anaomba wale Wabunge ambao ni wadau wa reli ya Tanga – Arusha - Musoma au mahali popote lakini ni mdau wa jambo hilo mnakaribishwa kwenye Kamati ya Bajeti ili kwenda kufaidika na kinachoendelea huko.

Waheshimiwa Wabunge, tutarudi saa 11.00 jioni ambapo sasa tutampa fursa Mheshimiwa Naibu Waziri na

Mheshimiwa Waziri ili sasa wahitimishe hoja yao. Baada ya hapo tuweze kupitia mafungu na tuweze kuitendea haki Wizara hii baada ya kuijadili kwa siku mbili. Kwa kweli nawapongeza sana, mjadala umekuwa wa uchangamfu mkubwa, utamaduni, michezo na habari vyote vimejadiliwa. Kwa kweli ni moja ya Wizara ambayo katika bajeti ya mwaka huu imepata michango mingi tena yenye furaha kubwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo basi, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutupa fursa hii ya kuweza kujadili masuala yanayohusu maendeleo ya nchi yetu kwa muktadha wa uendelezaji wa Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Watanzania wenzangu wote kutoa pole kwa msiba huu uliotupata na Mungu atupe faraja kama wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kusimamia vizuri Serikali na hasa kwa upande wa mapato na matumizi hadi kupelekea Wizara yetu kuongezewa bajeti kwa asilimia 19 kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Pia nimpongeze Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kuliongoza Bunge kwa weledi, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa umoja na ushirikiano walionao katika kuwatetea wananchi na kuboresha bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wangu, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara aliyoitoa tarehe 5 Mei, 2017 ambayo utekelezaji wake utaleta matokeo na mageuzi makubwa katika kuimarisha sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wangu kwa ukarimu wake mkubwa kwangu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na watumishi wa Wizara yangu kwa ushirikiano wanaonipa katika kazi zangu za Naibu Waziri. Niwashukuru wanawake wote wa UWT wa Mkoa wa Mtwara kwa kuendelea kushirikiana na mimi na kuniombea pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nasema ahsante kwa familia yangu inayoongozwa na mume wangu mpenzi Laurent Werema, kwa kunivumilia, kunitia moyo na kuniombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, naomba na mimi nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na sekta ya habari. Katika sekta hii tuna kundi la kwanza ambalo ni *TBC* ambapo Kamati iliitaka Serikali kulipa shirika uwezo wa kujiendesha. Wizara na *TBC* tayari zimelifanyia kazi suala la tozo ya visimbuzi (ving'amuzi) na andiko kuhusu tozo hii mpya linafanyiwa kazi na Wizara ya Fedha na liko katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la Kamati ni kwamba *TBC* ijenge *studio* ya kisasa Makao Makuu Dodoma. Fedha za kuboresha *studio* za *TBC* Dodoma zimetengwa

katika bajeti ya mwaka 2017/2018. Tukiangalia ukurasa wa 79 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri fedha hizi zinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameitaka Serikali kuimarisha usikivu wa *TBC* na utendaji, lakini pia kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Ni kweli kwamba *TBC* inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa mitambo lakini hata hivyo Serikali imeanza kuchukua hatua zifuatazo katika kutatua kwa awamu changamoto za shirika. Katika mwaka ujao wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga fedha za matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo kutoka shilingi za Kitanzania bilioni moja hadi shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni moja kwa mwaka 2016/2017 imeshapatikana na hii ni kwa ajili ya kuboresha usikivu katika maeneo matano ya mipakani na moja ni Kakonko (Kibondo), Mheshimiwa Kasuku kama yupo amelipigia sana kelele suala hili kwa hiyo awaambie watu wake wakae mkao wa kula. Pia katika Wilaya za Nyasa, Longido, Rombo, Tarime na leo pia nimesikia Mheshimiwa Ngonyani akilipigia kelele, kwa hiyo, wananchi wa Nyasa nao wakae tayari kwa ajili ya usikivu wa *TBC. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kamati pia ambalo linaitaka Wizara ihamishe mashine ya zamani ya *TSN* ya kuchapia magazeti ifungwe Dodoma ili kurahisisha upatikanaji wa magazeti. Wizara itafunga mtambo mpya Dodoma na hii ni kwa sababu kitaalam mtambo wa zamani ukifunguliwa na kuhamishiwa Dodoma unaweza kuharibika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utamaduni; Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kukuza utalii wa kiutamaduni na majibu yake ni kwamba Serikali imeendelea kuratibu, kusimamia na kutangaza bidhaa za utamaduni na kufanya maonesho na matamasha ya fani mbalimbali za utamaduni ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuvutia utalii na kuingiza mapato.

Mheshimiwa Spika, kuna mchangiaji mmoja pia alipendekeza kwamba kila mkoa kuwe na makumbusho lakini hili ni suala la Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Kitengo cha Malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kudhibiti mmomonyoko wa maadili ambalo limechangiwa na Wabunge kadhaa. Maadili ni mwenendo unaokubalika na wengi katika utendaji kazi au uendeshaji wa maisha. Kwa hiyo, suala hili ni la watu wote na inatakiwa lianzie katika familia hadi katika taasisi. Hata hivyo, Wizara inaendelea kutoa elimu kuhusu uzingatiaji wa maadili ya Mtanzania na kuchukua hatua mbalimbali za kisheria pale panapotokea ukiukwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maendeleo ya sekta ya sanaa, Kamati imeitaka Wizara iendelee kupambana na wizi wa kazi za wasanii. Wizara inaishukuru Kamati kwa kuunga mkono jitihada za Wizara na pia kwa kutoa msimamo wake kwa kuwataka wote wanaohusika na uharamia wa kazi hizo kuacha mara moja. Aidha, Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati kuhusu uboreshaji wa kazi hizo na itaendelea kushirikiana na wadau kuwajengea uwezo ili kuboresha kazi zao ili waweze kuendana na maendeleo ya teknolojia na kushindana katika soko la ndani na la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati imehimiza uboreshaji wa filamu za ndani na wananchi pia kununua kazi za ndani. Ushauri huo wa Kamati umepokelewa na utafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kambi ya Upinzani katika sekta ya sanaa kwamba matumizi ya stempu za *TRA* kutofanya kazi vizuri kutokana na teknolojia ya mtandao. Stempu hizo hutumika kubandikwa katika *DVD* na *CD* ambazo kwa sasa ndiyo mfumo unaotumika kusambaza kazi hizi hapa nchini. Kutokana na ukuaji wa teknolojia tayari taratibu za kutengeneza stempu katika

nakala laini zinaendelea na stempu hizi toka zimeanza kutumika zimefanikisha kubaini na kukamata kazi zisizo halali zenye thamani ya shilingi bilioni 5.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilionesha kwamba kuzuia kazi za nje ya nchi sio kinga ya wizi wa kazi za filamu na muziki. Serikali haijazuia filamu za nje bali inazitaka kufuata sheria, kanuni na taratibu. Kwa hiyo, dhana hii kwamba tunazuia kazi za nje si kweli, tunataka utaratibu ufuatwe na sheria vilevile zizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Wizara ni kulinda mila na desturi zetu na kulinda kazi za wasanii na hatutakubali ukiukwaji wa utamaduni wetu na hatutakubali pia kazi za nje ziingie katika nchi yetu bila kufuata utaratibu. Wizara yangu iliwasilisha barua TAMISEMI kuwaomba wawasiliane na mikoa yote ili kuona namna bora ya kuondokana na filamu zisizofuata utaratibu. Kwa hiyo, utekelezaji wa maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni kwa nchi nzima. Kwa hiyo, tusichukulie kwamba kwa kuwa yeye ametekeleza kwamba ni uamuzi wake.

Mheshimiwa Spika, nimeshasema kwamba Wizara iliandika barua TAMISEMI na kuomba wawasiliane na mikoa yote ili kuona namna bora ya kuondokana na filamu zisizofuata utaratibu, kwa hiyo, mikoa yote inatakiwa kufuata na kuzingatia agizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la upatikanaji wa Vazi la Taifa ambalo nalo limechangiwa na Wabunge kadhaa. Suala hili lilifikia katika ngazi ya Baraza la Mawaziri na uamuzi ulikuwa kwamba Vazi la Taifa litokane na kuamuliwa na wananchi wenyewe. Nikitoa mifano tu ni kwamba hata kipindi cha zamani ilikuwa inatokea mama zetu tulikuwa tukiwasikia wanasema leo tuvae Kitaifa, lakini hapa katikati pia lilizuka vazi fulani ambalo linatokana na kitambaa cha kitenge *(makenzi)* likaenda mpaka kutaka kuwa kama Vazi la Taifa. Kwa hiyo, ni vyema wananchi wakaamua sasa tuvae vazi gani kama ndiyo Vazi la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuboresha soko la ndani la tasnia ya filamu na kusimamia mapato ambapo tayari wapo watayarishaji wa filamu ambao wameendelea kutengeneza filamu nzuri zilizoweza kuingia kwenye soko la ushindani la ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, hoja ya uwepo wa filamu za nje zisizofuata taratibu zimefanya soko la ndani kukumbwa na ushindani mkubwa na Serikali na wadau husika kukosa mapato. Serikali katika kuboresha soko la ndani imeendelea kuwajengea uwezo watayarishaji na wazalishaji wa filamu ili kufanya kazi zao kwa weledi na kwa ubora wa hali ya juu kama inavyoelekezwa kwa kina katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uboreshaji wa tasnia ya ulimwende ambalo limechangiwa na wachangiaji kama wawili hivi. Tasnia ya ulimwende imeendelea kuendeshwa nchini kutoka mwaka 1994 na imeendelea kuwa na mafanikio makubwa hasa katika kuitangaza nchi na vivutio vyake ndani na nje ya mipaka ya Tanzania. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na waandaaji kurekebisha dosari mbalimbali zilizojitokeza na kuwa na mfumo bora na uwazi wa uendeshaji wa mashindano mbalimbali ya ulimwende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Miss Tanzania,* Wizara katika kulinda hadhi ya shindano hilo imetoa maagizo yafuatayo kwa waandaaji wa shindano hilo *(Lino International Agency). Lino International Agency* ihakikishe kwamba Kamati ya *Miss Tanzania* inatoa zawadi ya gari kwa mshindi wa *Miss Tanzania 2016* na washiriki wengine wote wanaodai zawadi zao ndani ya mwaka huu kabla ya Juni, 2017 na endapo wakikaidi ama wakishindwa kutoa zawadi katika muda huo watakuwa wamejitoa wenyewe kwenye biashara hii na sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuitaka Serikali ikamilishe utungwaji wa Sera ya Filamu. Tayari maandalizi ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Filamu yamefikia hatua ya kupata rasimu ya sera. Wadau mbalimbali wametoa maoni na rasimu hiyo itawasilishwa katika ngazi za maamuzi

mwishoni mwa mwezi Juni, 2017. Rasimu hiyo ya sera imezingatia pamoja na mambo mengine umuhimu wa kuanzishwa kwa shule ya filamu *(film school).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya michezo. Katika sekta ya maendeleo ya michezo kuna hoja iliyojitokeza ya CCM kurejesha viwanja vyake Serikalini. Hili suala limetolewa ufafanuzi mara kadhaa hapa Bungeni lakini hata hivyo niendelee kusema tu tena kwamba viwanja hivi ni vya CCM kwa sababu hatimiliki ni ya CCM. Niseme tu tena kwamba haipo hati ambayo inaonesha kwamba kuna kiwanja kilikuwa cha mmiliki mmoja kikahamishiwa kwa CCM, kwa hiyo tuelewe wazi kwamba hivi viwanja ni vya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameitaka Serikali ijenge na kulinda viwanja na maeneo ya wazi. Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 inaelekeza kuwa jukumu la ujenzi wa viwanja linashirikisha wadau wote ikiwemo Serikali na wadau wengine. Serikali katika juhudi zake za kuboresha miundombinu ya michezo inashirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje kujenga miundombinu kwa ajili ya matumizi ya michezo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha azma hiyo, Serikali imejenga Viwanja vya Taifa na Uhuru na sasa inajiandaa kujenga Uwanja wa Dodoma. Aidha, mamlaka mbalimbali na wadau nchini wanahamasishwa kushiriki kama walivyoanza baadhi kama vile Azam, Halmashauri ya Bukoba Mjini, Liwale, Lindi na kadhalika na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wadau mbalimbali wa michezo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kuwa halmashauri zao zinatenga maeneo na bajeti kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya michezo. Aidha, natoa wito kwa mamlaka zinazohusika kuhakikisha kuwa viwanja vyote vilivyovamiwa katika maeneo yao vinarejeshwa ili viweze kutumika kwa shughuli za michezo na burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba yupo mdau mmoja muhimu sana katika kuendeleza viwanja vya michezo ambaye ni *TFF.* Kwa taarifa ni kwamba kwa sasa ule Uwanja wa Tanga uko mbioni kuanza kujengwa mwaka huu, wanasubiri tu bajeti ipitishwe ili waweze kuujenga. Vilevile kama nilivyosema hapo awali, viwanja vya Lindi na *Memorial Moshi* viko kwenye *list* ya ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tena naunga mkono hoja, ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuruKamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushauri na mapendekezo yake yanayolenga kuimarisha utendaji wa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Joseph Osmond Mbilinyi na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hotuba yangu kwa kauli na maandishi. Natambua kuwa Waziri Kivuli tuliyenaye safari hii ni mdau mkubwa wa sekta ya sanaa nchini hususani tasnia ya muziki, hivyo, maendeleo ya sekta hii yanamgusa moja kwa moja kiasi ambacho hata jina la Wizara yangu ameligeuza kwenye hotuba yake yote, badala ya kuita Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo anaiita Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo, nafikiri anajifikiria mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kuwa Wizara yangu inaupokea ushauri wote uliotolewa hapa na itauzingatia katika utekelezaji wa bajeti yake ya mwaka 2017/2018. Hotuba yangu imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 67 ambapo waliochangia kwa maandishi ni 30 na kwa kauli ni 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri sana aliyofanya Naibu Waziri, Mheshimiwa Anastazia Wambura ya kuzitolea ufafanuzi baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge bado naamini kuwa muda nilionao ni mfupi sana sitaweza kuzitolea ufafanuzi hoja zote. Hivyo, naahidi kuzitolea ufafanuzi kwa maandishi na nitahakikisha kila Mheshimiwa Mbunge anapata nakala yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na baadhi ya hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwanza Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ukurasa wa tatu na wa nne wa hotuba yake anaeleza kuwa katika suaa la ulinzi wa uhuru wa habari, Tanzania tumepoteza sifa kabisa katika medani za Kimataifa na hivyo tuko kwenye orodha ya nchi zinazokandamiza uhuru wa habari duniani. Ushahidi wake ni utafii uliofanywa na *Reporters Without Borders* ambao amedai Mheshimiwa Waziri Kivuli kuwa umeiweka Tanzania nafasi ya 122 kati ya nchi 198 duniani zilizofanyiwa utafiti kuhusu uhuru wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma taarifa hiyo ya utafiti kwa makini *(Press Freedom Index)* inayoandaliwa kila mwaka, lakini mimi nimepata picha tofauti kidogo kwamba Tanzania tuko nafasi ya 83 badala ya 122 kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti huo. Kama ilivyo kila mwaka, Tanzania inaongoza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika nafasi hiyo ya 83 maana Kenya inatufuatia nafasi ya 95 pamoja na kwamba waandishi wengi wa habari wanaotuma taarifa kuhusu ukandamizwaji Tanzania wengi wako Nairobi, lakini wao ni 95, Uganda wako 112, Sudan ya Kusini wenzetu wako 145 wamejitahidi sana nchi mpya ile imepata uhuru hivi karibuni, Rwanda 159, Burundi 160, nchi nyingi tunazoziheshimu nazo tumeziacha kwa mbali, Brazil ni 103, Nigeria ya 122, India 136, Malaysia 144, Urusi 148, Singapore 151, Uturuki 155 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kushika nafasi ya 83 basi tumefanikiwa sana, hapana hata kama tumezipita nchi 107 duniani. Ninachosema na naomba Waheshimiwa Wabunge mnielewe, laiti hawa *Reporters Without Borders*

wangekuwa wanafanya utafiti wao kisayansi nina uhakika Tanzania tungekuwa tumeshika nafasi bora zaidi, nasema hivyo kwa sababu kuu tatu.

Kwanza, utafiti wanaoufanya hauangalii *quality of journalism* (ubora, weledi katika uandishi wa habari) ni kama wanaendekeza matumizi ya watu ambao hawajasomea uandishi wa habari (makanjanja) ambao hawajui maadili ya taaluma. Matokeo yake tunapata uandishi ambao hauna *accuracy* na nasema hili kwa masikitiko sana maana mimi ndiyo mwenzao katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikwenda kwenye sherehe za uhuru wa vyombo vya habari Mwanza. Amini usiamini nimetoa hotuba tena kwa pole pole, kwa kuzingatia hali ya magazeti yetu sasa hivi, magazeti yote sasa hivi yanashindwa kuuza hata asilimia 50 ya kile wanachozalisha ni kutokana na vyombo vya elektroniki kusoma magazeti hayo kwa undani mno, sasa kuna haja gani ya kununua magazeti? Kwa hiyo, nikaeleza jamani hebu tufuate kama nchi zingine zilivyo, tusome vichwa vya habari. Baada ya dakika 30 tu kutoka hapo taarifa ya chombo cha habari cha siku nyingi inasema Mwakyembe kapiga marufuku usomaji wa magazeti. Sasa niko mimi pale, tunaongelea uhuru wa vyombo vya habari na uhuru ndiyo huo *inaccuracies.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, wiki iliyopita ilikuwa siku ya Ijumaa, gazeti kubwa kabisa hapa ukurasa wa 30, sitalitaja wataona kama nawaonea lakini mliosoma mmeona. Ipo taarifa inasema, mke wa Malkia wa Uingereza astaafu. Hivi Malkia wa Uingereza ana mke? Unajua inaweza kutuletea matatizo makubwa hata ya kidiplomasia, gazeti linaandika hivi? Unajua katika uandishi wa habari tunahitaji sana sana uangalifu, mnafanya kazi muhimu ambayo watu wote wanategemea na Watanzania na dunia inawaamini, sasa mkifanya vikosa vidogo vidogo kama hivyo heshima itakuwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe angalia tu leo hii tuna msiba mkubwa katika Taifa letu, tena niwape pole sana

Watanzania wote na wazazi waliopoteza watoto na ndugu zetu wote ambao leo wapo huko wakiomboleza, lakini mwandishi yeyote ambaye amesomea taaluma ya habari hawezi akatoa mbele mapicha tu ya watoto wamezagaa pale wameumia, wamelazwa, majani yamefunikwa unakuwa *insensitive*.

Mheshimiwa Spika, katika uandishi wa habari tunasema *you have to minimize harm.* Huo ndiyo uandishi wa Tanzania, ukiwaita kesho kuwahoji oooh uhuru wa habari unaingiliwa, wewe kasome *brother* ndiyo hicho tu utaelewa. Sasa hivi tuna mitandao ya jamii ambayo kila mtu tu ni mwandishi, jana alikuwa anauza sijui mikate kesho na yeye ni mwandishi, ni matatizo makubwa. Kwa hiyo, tuna kazi ya kudhibiti sekta hiyo lakini wenzetu hawa *Reporters Without Borders* hawaangalii haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, utafiti huu haurutubishwi na ushahidi wa kimazingira *(circumstantial evidence)* kwamba inakuwaje kwa mfano nchi ina ukandamizaji mkubwa wa uhuru wa vyombo vya habari kama Tanzania inavyosemekana bado ni moja ya nchi bora katika Bara la Afrika ambayo inavutia uanzishwaji mkubwa wa vyombo vya habari, ni moja ya nchi inayoongoza katika Bara la Afrika hata duniani tupo katika orodha. Leo hii Tanzania ina majarida 428, ina redio 148, vituo vya *television* 32, watumiaji wa mitandao wako takribani milioni 20 na *line* za simu milioni 41, ni nchi gani yenye ukandamizaji unaweza ukakuta rutuba ya namna hiyo ya vyombo vya habari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, *freedom index* inaangalia vigezo vitatu vikuu; cha kwanza wanaangalia uhuru wa vyombo vya habari; pili, wanaangalia ulinzi na usalama wa waandishi wa habari, lakini kwa kuangalia kwanza sheria zilizopo nchini na kuongea na wadau mbalimbali. Kigezo cha tatu wanakiita *level of pluralism* hata kwa kiswahili kutafsiri vizuri, ni uhuru pengine wa ujumla katika jamii *(diversity).* Katika hicho kigezo Watanzania muelewe mtapoteza *point* kila siku. Mimi nitatoa mfano kwa sababu

tunawaudhi wakubwa, Watanzania shida yetu ambayo mimi nasema lazima tujivunie ni kwamba hatuwezi kukubali kuyumbishwa tukaua utu, uhuru na utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, mwaka jana Tanzania iliitwa Geneva mbele ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kutetea rekodi yake ya Haki za Binadamu, tulikuwa tunakabiliwa na masuala 227. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mwamasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria, Profesa Mchome na wataalam wote wa sheria walioko pale kwa sababu ilibidi kukaa chini kuangalia je, tukubali kuyumbishwa ama tusimamie misimamo ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tulikubali kutekeleza masuala 131 ambayo yamo kwenye programu ya utekelezaji wa nchi yetu, ni mengi tu kwa mfano, kuondoa tozo kwa ajili ya vyeti vya watoto, kushughulikia kwa mfano suala la Sheria ya Ndoa ambalo na sisi wenyewe *it is a problem*, sisi tuko tu kwenye mchakato lakini masuala mawili tulikubali kidogo tukasema tuyaangalie lakini masuala 94 tuliyakataa katakata ili kulinda utu, uhuru na utamaduni wetu. Nitawatolea mifano ya baadhi ya mashinikizo kama ifuatavyo:-

(i) Kuhalalisha utoaji mimba, tukasema msitushinikize sasa hivi. *(Makofi)*

(ii) Kufuta ndoa za wake wengi, tukasema hapo mnaingilia utamaduni wetu, mnaingilia imani zetu, hatukubali. Hata kama mnaondoa sijui hiyo misaada iondoke. *(Makofi)*

(iii) Tukubali ndoa za jinsia moja, tukasema hilo *over our dead bodies* pengine tufe wote kizazi hiki waingie hao ambao watakubali upuuzi wa aina hiyo, tumekataa Tanzania lakini ukikataa wakubwa wapo. *Lobbying* ya masuala hayo ni kubwa katika dunia. *(Makofi)*

(iv) Tukubali haki za mashoga na tuutambue ushoga kama ni haki ya binadamu, tukasema hapana. *(Makofi)*

(v) Tuliondoe suala la ushoga kwenye Sheria zetu za Adhabu, tukakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwambia Watanzania, *the gay and lesbian lobby in the world is very strong,* wana pesa hao. Ukiwafanyia fujo wanakuyumbisha kila sehemu. Mimi nilijua tutapunguziwa *marks* ndiyo wanaotoa pesa kwenye mashirika mengi yanayotufanyia *assessment.* Kwa hiyo, Watanzania tuwe macho, mara nyingine hizi *statistics* lazima tuziangalie kwa macho mwili kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbile suala lingine muhimu ambalo Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani amenukuu ukurasa wa tano wa hotuba yake akisema Ibara ya 19(2) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa na kuonyesha jinsi ibara hiyo inavyotoa haki ya kujieleza, ya kutafuta, kupata na kusambaza taarifa kwamba haina vikwazo vyovyote na kwamba maudhui yake yamerudiwa katika Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi nimekubaliana naye kabisa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu ile Ibara ya 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii aliisisitiza zaidi Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kusema Ibara ya 18 haina *clawback clause* yaani kipengele kinachobana au kudhibiti haki hiyo. Picha hii ya kwamba vipengele hivi vinabeba haki na uhuru usio na mipaka inatokana na mdogo wangu Mbilinyi, Waziri Kivuli kusoma Ibara moja tu yaani Ibara ya 19(2) ya huo mkataba hakwenda Ibara ndogo ya (3). Angeenda Ibara ndogo ya (3) angekuta kuna masharti ya kutekelezwa, masharti hayo yanasema, kwanza, haki hii utaitekeleza lakini kwa kuheshimu haki na heshima ya watu wengine na pili kwa kulinda usalama wa Taifa, afya na maadili. Kwa hiyo, hakuna haki isiyo na mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vilevile katika kutafsiri Katiba, najua Mheshimiwa Tundu Lissu amefanya makusudi tu, anaelewa, huwezi ukatafsiri Katiba kwa kipengele kimoja kimoja. Kila kipengele cha Katiba ni sehemu ya tungo moja ambapo vipengele vyote lazima uviweke juu ya meza, uvisome kwa pamoja kuelewa maana ya kila kipengele. *Any constitutional provision is but a component in an ensemble of interacting provisions which must be quote or brought into play as part of a larger composition.* Hii ni *principle* wanasheria wote wa *constitutional law* wanajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 lazima isomwe na Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema, katika kufurahia haki na uhuru wako hakikisha huathiri haki na uhuru wa wengine, huathiri maslahi ya umma na huathiri usalama wa Taifa lako. Kwa hiyo, hiyo ndiyo mipaka nilitaka tu kusisitiza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote hapa kwamba mwaka 2004, nchi za Kiafrika ziliamua kuunda Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika. Nchi zilikuwa 30 na mojawapo ilikuwa Tanzania. Tungekuwa nchi ya ukandamizaji wa haki za binadamu tusingeweza kukubali kuanzisha mahakama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, kuna kipengele kinachosema, nchi lazima ikubali ili raia wake wanapokuwa wamekwazwa wataleta mashauri yao kwenye mahakama hii. Ni nchi saba tu toka mwaka 2004 zimesaini kuweza kushtakiwa na watu wake Tanzania nayo imo. Sasa jamani nchi ambayo inajiona kwamba iko *notorious* katika ku-*abuse human rights* inaweza kweli ikakubali kuingia kwenye kifungu hicho?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia yote haya unaweza hata kushangaa kwamba hii ndiyo Serikali ya kuteka waandishi wa habari? Nafikiri tunabangaiza tu hoja mpaka jana nimeshangaa tu kusikia hata eti Katibu Mkuu

wa CCM ametekwa? Yaani imekuwa sasa utani nchi hii ukiitwa na polisi umetekwa, mtu amefumaniwa huko ametekwa, tunafanya mzaha kwenye kitu muhimu sana katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Edward Snowden ambaye amekimbia nchi yake 2013 kujificha Urusi hakimbizwi na Serikali ya Tanzania, anakimbia Marekani kwa kuvuka mipaka, unavuka mipaka. Siyo hivyo tu, tuna Julian Assange ambaye toka mwaka 2012 nafikiri anakaa kwenye kachumba kamoja tu kwenye Ubalozi wa Equador, anakimbia wakubwa, kote kuna mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipokuwa Mwanza tumekaa kidogo na kijana wangu mmoja mwandishi nikamwambia nakupa swali. Je, ni nchi gani ambayo watu 230 pamoja na waandishi sita walikamatwa kwa kufanya maandamano wakati wa kuapishwa kwa Rais wa nchi yao? Akasema Tanzania.Nikamuuliza lini? Akafikiri sana. Baadaye nikamwambia hapana, huyo Rais ameapishwa mwaka huu, akashindwa. Nikamwambia ilikuwa ni Marekani. Alisema haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ndiyo tatizo tulilonalo Waafrika tunaamini kwamba chochote cha nje ni bora cha kwetu siyo bora. Watu 230 walikamatwa na wakiwa waandishi wa habari sita na wakafunguliwa mashtaka. Hayo tunafikiri yanafanyika Tanzania tu, yanafanyika nchi za Kiafrika lakini sisi kwa kweli tuko katika nchi inayojitahidi sana katika kuheshimu haki za binadamu za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii vilevile imebaini kuwa Kanuni za Urushaji wa Matangazo ya Dijitali na Kanuni za Leseni zitazuia uwepo wa *channel* za umma yaani *public broadcaster* katika vifurushi vya matangazo ya *Direct To Home (DTH).* Jambo hili hili limeongelewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kweli kwenye majibu yangu ya maandishi nitawataja wote.

Mheshimiwa Spika, naona kama tumewahi kidogo lakini naomba niseme kwamba kanuni mpya ambazo zinapendekezwa hapa hazitaawaathiri watumiaji wa *channel* za umma kwa kuwa wataendelea kuwa na haki ya kupata matangazo ya televisheni za umma hata baada ya vifurushi vya kawaida vya kulipia kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita Waheshimiwa Wabunge kilikuwa cha mpito, kwa hiyo, kilikuwa na matatizo mbalimbali ambayo lazima tuyavumilie. La msingi hapa ni kuwa hizo zinazoitwa kanuni ni mapendekezo ya kanuni ambayo wamepelekewa wadau wayaangalie halafu wayarudishe Serikalini, halafu kinaendeshwa kikao cha pamoja cha kujadiliana. Nafikiri tumewahi mno, tumeleta wasiwasi mapema sana kabla ya kufika tunakotakiwa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na suala la upungufu kwenye Sheria ya Haki Miliki. Wizara yangu imeona umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria, sio tu ya Haki Miliki lakini sheria zote katika sekta hizi kwa mfano sheria inayogusa tasnia ya filamu na sanaa ikiwemo Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Namba 4 ya mwaka 1976 na Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Namba 23 ya mwaka 1984. Tayari Wizara imeshaanza kuchukua hatua kwa kuanza uandaaji wa marekebisho ya sera ili kukidhi matakwa ya sasa. Kwa upande wa Sheria ya Haki Miliki tunashirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tuweze kuifanyia marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na suala la Serikali iwezeshe timu za Taifa ili ziweze kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali, hayo ni mawazo ya Kamati. Sisi tunaikubali hiyo changamoto na tayari tunafanya hivyo. Serikali imeendelea kutenga bajeti kila mwaka hata kama sio toshelezi. Mfano mdogo tu ni kwamba mwaka 2016/2017 tuliweza kugharamia wanamichezo wote saba walioshiriki katika *Olympic* nchini Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka kesho mwezi Aprili tuna mashindano ya Jumuiya ya Madola yatafanyika Australia. Tayari Serikali ipo kwenye mazungumzo ya mwisho na nchi za Ethiopia kwa ajili ya kupeleka wakimbiaji wetu (wanariadha wetu); Cuba kwa ajili ya kupeleka timu yetu ya ngumi na vilevile China kwa ajili ya wachezaji wetu wa mpira wa meza. Hizo zote ni juhudi za Serikali na mwaka 2019 nilishalisema hili kwamba sisi ni wenyeji wa mashindano ya *AFCOM* kwa vijana wa chini ya miaka 17. Tayari timu yetu ya vijana wa miaka 13 – 14 ipo kambini. Ikifika mwaka 2019 watakuwa tayari wana miaka 16 - 17. Kwa hiyo, Serikali inafanya juhudi na tumelizingatia hilo vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala la Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa vilevile Mheshimiwa Devotha Minja alilisema hili kwamba kuyumba kwa uchumi kunakotokana na sera za Serikali za Awamu ya Tano, kumeiathiri sekta binafsi ya habari na vyombo vya habari sasa hivi vinapunguza wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu mnielewe, si kweli hatua za kimageuzi zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwamba zimeleta matokeo hasi. Mageuzi haya yameleta matokeo mengi chanya ikiwemo kuongezeka mapato ya Serikali na kutekeleza miradi mingi tena mikubwa ya maendeleo ambayo wote tunaijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai kwamba ni sera za Serikali ya Awamu ya Tano zinafanya vyombo vya habari kuanza kupunguza wafanyakazi, kwa kweli kama nilivyosema si kweli. Naomba niulize kama wote mnafuatilia vizuri mitandao na vyombo vya habari, mwezi Julai, 2015 Shirika la Utangazaji la Uingereza *(BBC)* lilitangaza kupunguza wafanyakazi 1000, Serikali ya Awamu ya Tano ya Tanzania haikuhusika.

Mheshimiwa Spika, Machi 2017, Shirika la Habari la *ESPN* lilipunguza wafanyakazi 100, mtandao wa *Twitter* ulipunguza asilimia tisa ya wafanyakazi wake wote, tena ilikuwa ni Oktoba, 2016. Kati ya mwaka 2010 hadi 2016 *CNN*

yenyewe imeshapunguza zaidi ya wafanyakazi 100 wakiwemo wahariri na wachambuzi waandamizi. Yote haya ni matokeo tu ya uchumi wa dunia hayahusiani kabisa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Bunge live* ambalo tumelijibu, tumelijibu, tumelijibu imefika mahali naomba sasa nilielekeze kwa Bunge, *after all* nina taarifa kwamba tayari *TCRA* imewakabidhi Bunge leseni sasa hivi wana uwezo wa kufanya chochote wanachotaka. Kwa hiyo, naomba hili nilielekeze huko badala ya mimi kujibu baadaye mtasema ulisema, ulisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Serikali iache kuangalia mtandao wa kijamii kwa jicho hasi bali ionekane kama sehemu ya ajira ili kukuza kipato. Hivyo ndivyo tunavyofanya, tumejenga mazingira mazuri ya mitandao na Watanzania ambao wapo kwenye mitandao kwa sasa ni mamilioni. Tunachosema hapa ni matumizi mabaya ya mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanasiasa maarufu wa Marekani nafikiri Hillary Clinton alisema mwezi Desemba, 2016 kuwa matumizi mabaya ya mitandao ni ugonjwa hatari unaoweza kuteketeza dunia. Alisema hivyo kwa sababu mwezi Desemba 2016 kulikuwepo taarifa kwenye mitandao kwamba Serikali ya Israel inasema itaipiga Pakistan ikipeleka askari Syria. Pakistan wakajibu jaribu na sisi tutakushughulikia, kuja kugundua ni maneno wala hayajatoka Israel. Kwa hiyo, kwa kweli mitandao ya jamii kama hatujaidhibiti inaweza kutuingiza katika matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi mtakumbuka kisa cha kijana wa kiingereza aitwaye Liam Stacey aliyetumia vibaya uhuru wake wa habari na mnajua kwamba hivi karibuni tu amemaliza kifungo chake baada ya Mahakama ya Mjini Swansea kumkuta na hatia ya kumkashifu mchezaji wa zamani wa Bolton Wanderers mwenye asili ya Afrika Fabrice Muamba aliyekuwa ameanguka uwanjani baada ya kupata shambulizi la ghafla la ugonjwa wa moyo. Kwa hiyo, sio sisi

tu ambao kwa kweli tunahangaika namna ya kudhibiti hata wenzetu wanafunga lakini tunaambiwa sisi tu Tanzania ambao tumewapeleka watu mahakamani, lazima tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani na Mheshimiwa Profesa Jay (Mheshimiwa Joseph Haule) na Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema Serikali inawapuuza wadau wa masuala ya sanaa hasa baada ya kuwatumia kwenye chaguzi mbalimbali. Serikali haijawahi kuwapuuza wasanii nchini na kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwa kweli tumechukua hatua mbalimbali ya kuwajengea weledi, kwa kuwatambulisha na kuwakutanisha na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito tu kwa baadhi ya vyama vya siasa ambavyo kwa kweli wanasiasa wao wanawachochea hawa vijana kuimba nyimbo za kisiasa, hii ni *entertainment industry*. Mimi naomba vijana wangu wanisikilize, nimewaambia wanipe mfano wa mwanamuziki yeyote duniani aliyefanikiwa kwa kutukana viongozi, nimewaambia hivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeenda Nigeria, wasikilize P-Square, Tiwa Savage, Davido, Don Jazzy, ni vijana ambao wengine wamenunua mpaka ndege, *very successful* lakini nimewaambia hebu niambie umewahi kusikia wanasema *ooh Mr. President your wrong. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia wewe imba nyimbo ambazo zitakuletea mafanikio mwenyewe. Kama unataka siasa nenda kagombee Udiwani huko au kagombee nafasi yoyote huko, hii ni*entertainment industry* siyo *political industry* na wengi wamenilewa. Angalia Afrika Mashariki akina Chameleon kuna wimbo wowote Chameleon anaongelea Serikali ya Uganda? Nani *successful musician* hapa anafanya hivyo, namfahamu mmoja tu, alijitia mwanasiasa Fela Ramsome Kuti lakini aliishia pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna vijana wanang'ara hapa kina Diamond, Ally Kiba, sikiliza nyimbo zao hakuna hata moja wanaongea mambo ya kipuuzi sijui anajifanya mwanasiasa, utakuwa mwanasiasa wewe? Mimi naomba kazaneni kuboresha vipaji vyenu, *let me tell you* vijana wangu *the sky is the limit.* Mimi nimewahakikishia nitawasaidia kwa kila hali muweze kufika anga ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja hapa ambayo imeongelewa na Mheshimiwa Sakaya, Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Sixtus Mapunda kwamba Serikali iwekeze katika michezo kwani haiwezi kutegemea mafanikio bila kuwekeza fedha. Nafikiri hili suala nimeshaliongelea, kwa kweli uwekezaji ni suala ambalo tunaliona ni muhimu sana tena sana na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kimoja tu, nilikuwa naongelea kuhusu vijana wangu wa muziki tunapenda mno kulalamika. Nichukue fursa hii kuwapongeza vijana wawili wasanii, Ndugu Hamis Mwinjuma (Mwana FA) na mwenzake Ndugu Ambwene Yessaya (AY) ambao badala ya kulalamika wameibeba Kampuni kubwa ya Tigo kuipeleka mahakamani kwa sababu imekuwa ikitumia miziki yao kama *ringtones* kwa muda mrefu na Mahakama ya Ilala ikaiamuru Kampuni ya Tigo kuwalipa wale vijana zaidi ya shilingi bilioni 2.185, wame-*appeal* iko *High Court*. Mimi nasema vijana wa Tanzania tukiwa namna hiyo *(pro-active)* siyo kukaa tu kutunga ngonjera za kulalamika, tutafika mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetunga sheria kandamizi za uhuru wa habari mfano *Cyber Crime Act*, Sheria za Huduma za Habari hivyo zibadilishwe. Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Devotha Minja, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa John Mnyika na wengine ambao nitakuwa nimeruka majina yao wameliongelea suala hili. Tofauti na mtizamo wa watu wachache sheria hizi zinalinda uhuru wa wanahabari na wananchi na kwa sasa zimethibitishwa hata na Mahakama Kuu kuwa ni sheria nzuri na hazikiuki Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza katika uamuzi wake nimeona niupitie huu wa Machi 9, 2017 kuhusu Shauri la Madai Na. 2 la mwaka 2017, Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania na *Hali Halisi Publishers Ltd.* dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji De-Melo alitupilia mbali shauri la kupinga Sheria za Huduma za Habari kwa kuwa walalamikaji hawakuwa na hoja za msingi na taratibu za kisheria kupinga sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam katika Shauri la Kikatiba Na. 6 la mwaka 2016 kati ya *Jamii Media Company Ltd.* dhidi ya *Attornery General* na *IGP*, kwa kweli uamuzi uliotolewa na Majaji Kitusi, Koroso na Khalfani ulikuwa ni mzuri. Uamuzi huo ulisema licha ya kasoro ndogo ya utoaji wa dhamana walifikia hitimisho kuwa Sheria ya Makosa ya Mitandaoni ya mwaka 2015 haikiuki misingi ya Katiba wala haki za watu kujieleza. Hukumu hii imezima rasmi hisia na mawazo ya kuwa sheria hizi ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele imegonga sipendi sana uniambie mara ya pili. Mambo mliyoyasema ni mengi, naomba nizungumzie lugha ya kiswahili. Tumempongeza Mheshimiwa Rais kwa kutumia lugha ya kiswahili mara kwa mara na naomba viongozi wote tuige na tuongee kiswahili sanifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa upande wetu Baraza la Kiswahili la Kitaifa nalo linafanya juhudi kubwa, limetoa kamusi nyingi na sasa wametoa *Kamusi standard,* hii hapa, ningetamani kila Mheshimiwa Mbunge apate. Ni kamusi ya kisasa, ni kubwa na imekubalika na nchi nyingi za Kenya, Uganda na nchi zingine. Naomba Mwenyekiti ufikishe ombi langu kwa Mheshimiwa Spika ukimkata Mheshimiwa Mbunge hela kidogo tu shilingi 25,000 kila mmoja atakuwa kwenye *pigeon hole* ana kamusi hii, naomba sana iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala moja ambalo ameliongelea mdogo wangu Kubenea, mwandishi

wa habari wa siku nyingi, analalamika kwamba nimewakatisha tamaa wanahabari kwa kusema asilimia 90 hawana weledi. Sio mimi, ndiyo shida hiyo, sasa huyu anayeongea ni mwandishi wa habari wa siku nyingi lakini amekaa na hiki kitabu siku tatu hata kuelewa hajaelewa, ananishangaza sana Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Spika, naomba nisome, wala siongelei magazeti hapa, yeye anasema nimewasema watu wa magazeti. Nimesema kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kusimamia ubora wa huduma za utangazaji *(broadcasting quality of service)* na ndiyo waliofanya utafiti kwa vituo vyote vya redio na *television,* yeye anamfikiria Mwanahalisi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania wanasema katika ukaguzi uliofanywa asilimia 90 ya wafanyakazi wamebainika hawana sifa stahiki katika taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji katika vituo vya redio na *television.* Vilevile nimkumbushe Mheshimiwa Kubenea hiyo inakuja pia kwa waandishi wa habari, tumewapa miaka mitano nendeni shule ndugu zangu, dunia imebadilika sasa hivi. Haiwezekani umetoka darasa la saba tu unakuwa mwandishi wa habari eti nawe unatafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliona *clip* moja kijana mmoja anatafsiri alikuwa anaongea na Mmarekani mmoja mtalii, yule mtalii anasema waambie Watanzania nchi yao ni nzuri, yeye anasema ninyi Watanzania mnapenda kuomba chakula tafuteni ninyi wenyewe chakula. Kwa hiyo, mimi naomba tuwe na weledi katika tasnia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie tu kwa kusema hoja zenu zote sisi tutazifanyia kazi na kuzigawa kwa kila Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mgt*..................Sh. 3,985,517,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majina nimeshapata, tunaanza na Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Sugu kaa vipi?

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vilio vya muda mrefu vya watu wenye ulemavu hususani jamii ya viziwi kuhusiana na matumizi ya lugha ya alama kwenye vyombo vya habari hasa luninga. Kwenye hotuba hii tulitegemea tuone tamko ama kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili ila hotuba imekuwa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufafanuzi wa jambo hili kuhusu Serikali kutoa tamko kuhusiana na suala hili. Kama ufafanuzi hautaniridhisha, nimueleze tu baba yangu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwamba nitatoa shilingi kwenye mshahara wake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri namshukuru sana Mheshimiwa Ikupa kwa suala lake ambalo amelileta kwetu. Ni kweli Wizara inatambua kwamba kuna tatizo la watafsiri wa lugha za alama, Serikali imekuwa ikufuatilia katika vyombo mbalimbali vya habari, *tv* mbalimbali na kuona kwamba hili kweli ni tatizo, majibu ambayo tumekuwa tukipata ni kwamba hawa ni wachache na gharama zao ni kubwa. Kwa upande wa *TBC* tumeshatuma maombi ya kuruhusiwa kupata vibali vya ajira, kwa sababu wale wanaoajiriwa kwa siku wana-*charge* gharama mpaka shilingi 80,000 kwa siku. Kwa hiyo, tunachotaka ni kwamba waajiriwe wapate ajira ya kudumu ili kusudi waweze kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tamko la Serikali ni kwamba hivi karibuni tutawapata watafsiri wa lugha ya alama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ikumbukwe kwamba tayari ilishatolewa hata ile tusime ukomo wa kuajiri hawa wakalimani ambapo ilikuwa ni mwaka huu mwezi wa tatu. Sasa tatizo liko wapi? Kwa sababu akiongelea *TBC* kuna vyombo vingine mbalimbali kuna *ITV, Channel 10* na vyombo vingine, tatizo liko wapi? Kwa nini mpaka sasa wakalimani hawa hawajaajiriwa. Sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hiyo natoa shilingi na ninatoa hoja kwamba wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa. Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Magdalana Sakaya, Mheshimiwa Susan, Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma na *Chief Whip.*

Tunaanza na Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. nami naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Ikupa, Serikali tunaomba mtusaidie kwa sababu *TCRA* ndiyo wanaosajili vyombo vyote hivi vya habari. Ni jambo dogo tu kwamba ni kuwawekea kipengele ambacho kwamba kitawabana ili waweze kuweka watafsiri wa hizi lugha za alama bila hata kusumbuana, kwa sababu hapa ukisema tutashughulikia ni lini? Toa tamko hapa *TCRA* wawabane hawa watu ili vyombo vyote viweze kufanya hivyo. Ahsante.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninamuunga mkono Mheshimiwa Ikupa kwamba, Serikali sasa ifikie wakati iweze kuweka hizi alama kwa ajili ya wengine ambao wanaangalia kwa kutumia *body language.* Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie ni jinsi gani inavyoweza kuweka alama hizi kama *TBC* na *television* zingine ili watu hawa waweze kupata haki yao ya msingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namuunga mkono Mheshimiwa Ikupa. Kwanza Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi sasa hivi inawahitimu wengi sana wa elimu maalum ambao wanaweza hata wengine kufanya hizi shughuli kwa kujitolea, kwa sababu wengi wamemaliza kozi, lakini hawana shughuli. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba Serikali lazima ifanye jitihada za maksudi kuhakikisha kwamba wenzetu hawa wenye ulemavu nao wanapata usawa wa haki ya kupata taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nisingesimama lakini majibu ya Naibu Waziri yamenifanya nisimame. Naibu Waziri anasema kwamba hawa walemavu ni wachache. Sasa mimi nasema kwa kuwa niwachache tuwapuuze? Hii haiwezekani wala haikubaliki, halafu anasema gharama za kuajiri, gharama za kuajiri, gharama za kuajiri maana yake nini, kwa sababu hii ni ajira kama ajira nyingine mimi nafikiri Serikali ingeweka sharti

kwamba ni lazima kila chombo cha habari kiajiri watu kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho amezungumza habari ya *TBC* kwamba hawa wako *TBC,* leo tulikuwa na mazishi ya Kitaifa Arusha, *television* ambazo zilikuwa zinaonyesha ni Azam, *Star TV* na *Clouds,* lakini *TBC* hawakuwa *live,* ina maana kwamba hawa wenzetu hawakushuhudia jambo hili. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali isitishwe wala isibabaishwe na hivi vyombo vya habari, Serikali iweke sharti kwamba lazima hawa watu wawepo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini lakini hakusema walemavu wako wachache amesema wataalam ndiyo wako wachache, nafikiri wakalimani wako wachache kwa hiyo siyo walemavu ni wataalam wa ukalimani wako wachache, *that is what she said*. Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami ninamuunga mkono Mheshimiwa Ikupa kwa hoja yake ya msingi sana. Ni suala la Kikatiba kila Mtanzania apate haki ya kupata habari kama wengine. Kwa hiyo, kundi hili ambalo ni kundi maalumu wana haki ya kupata habari kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali tayari imeshaanza kutoa maagizo kwamba majengo yanayojengwa kuwepo na njia ambazo wanaweza wakapita walemavu na kila mahali wamejitahidi kwenye maeneo mengi. Na hili pia walipe uzito unaostahili kwamba kila chombo cha habari kihakikishe kinaweka alama ili wenzetu waweze kupata habari kama Watanzania wengine, hili ni suala la msingi Serikali ilipe uzito unaostahili. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi kipekee ninamuunga mkono sana Mheshimiwa Ikupa kwa hoja yake ambayo ina mashiko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulemavu ni suala la muda tu, sasa hivi hapa tunajiona ni wazima lakini unaweza ukafika hapo ukapofuka macho. Kwa hiyo, jambo hili liangaliwe kwa mapana yake.

Pili, ni suala la Kikatiba haki ya kila mtu kupata habari, inasikitisha kuona kwamba sasa hivi tuko kwenye enzi ya teknolojia lakini bado wenzetu hawa pamoja na kwamba ni wengi kweli, walemavu ni wengi sana. Walemavu wana haki ya msingi ya kupata habari hasa tukizingatia kwamba sasa hivi ni zama za sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba wataalam ni wachache sikubaliani nalo, kwa sababu Serikali hii hata kama ni wachache wamo ndani lakini huko nje wako wengi. Kwa hiyo, Serikali inaweza kuleta fedha, ikaajiri watu kutoka nje ili kundi hili ambalo ni *marginalize* lipate haki yake ya kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Ikupa kwa sababu moja, hili jambo kama walivyosema wenzangu ni jambo la Kikatiba, ni haki yao ya msingi ya kisheria ambayo Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba wanaipata. Tukikubaliana na majibu ambayo ametoa Naibu Waziri ya kwamba wale wataalam ni wachache na kwa sababu hiyo wanaajiriwa kwa gharama kubwa, tutakuwa tume-*set precedent* mbaya sana ambayo hata kesho linaweza likatokea watu wakapata maradhi fulani halafu tukapewa *excuse* kwamba jambo hili ni ghali sana. Kwa hiyo, naomba tuachane na hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, hizi *tv* ziko ngapi katika nchi hii mpaka ishindwe kugharamiwa? Naomba ama kuwepo na sheria ambayo itahakisha

kwamba hawa wataalamu wanapatikana kwenye hizo TV au Serikali itoe ruzuku.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kushuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Na mimi pia naomba niungane na Mheshimiwa Ikupa, kwakusema kwamba *the government moves on paper,* Serikali inakwenda na maandishi. Kwa hiyo, naiomba tu Serikali kwamba leo hii itoe tamko hapa hadharani na pia tena iende ikaandike ili vile vyombo vya habari vyote viweze kufuata Waraka wa Serikali. Hatuwezi tukaendeshwa na watu wachache Serikali ndiyo inayoongoza watu wengine nini wafanye. La sivyo wafungiwe kwa sababu hata kama ni wachache wana haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iweze kuchukua wazo la Mheshimiwa Ikupa na kuweza kulifanyia kazi kwa namna hii.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitambue mchango mkubwa sana ambao umekuwa ukitolewa na Mheshimiwa Ikupa ndani la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuwawakilisha watu wenye ulemavu katika nchi yetu ya Tanzania, amekuwa akifanya kazi nzuri sana na ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi ya pekee na mimi kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili la tafsiri ya lugha za alama kwenye vyombo vya habari ili kuwawezesha Watanzania wenye ulemavu, kuweza kufuatilia matukio mbalimbali ambayo yamekuwa yakitokea katika nchi yetu ya Tanzania, ni jambo la kimsingi kabisa na ninawashukuru Wabunge kuliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme jambo

moja kwamba Mheshimiwa Ikupa anafahamu, toka Serikali hii ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani, imekuwa ikifanya juhudi kuhakikisha sheria ya mwaka 2010 ambayo ndiyo inasimamia haki za wenye ulemavu katika nchi yetu ya Tanzania, yale masuala yote ya kimsingi yanatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Ikupa anajua tumeshafanya mambo mengi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumeshafanya mambo mengi na hivi juzi tu tumetoa taarifa hapa wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tulikuwa hata na tatizo la vifaa vya kutumiwa na watu wenye ulemavu katika shule zetu ili kuwawezesha kupata elimu kama wanavyopata watoto wengine wa Kitanzania. Kwa mfano, tumeshanunua takribani kama *braillers* (mashine za kuandika za watu wenye ulemavu wa kuona) kama 1400 hivi, na mambo mengine mengi tumeanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Ikupa akubali na aruhusu kwamba jambo hili kwa sababu limeshaanza kufanyiwa kazi na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya habari, ofisi yetu, lakini na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya *TCRA* atuachie tuendelee kufanya kazi, tukutane na vyombo vya habari vya *private* na vyombo vya habari vya Serikali ili sasa tutafute njia nzuri ya kuweza kulitekeleza jambo hili kwa pamoja na hivyo basi haki ya wenzetu wenye ulemavu yakuweza kupata habari iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwambia Mheshimiwa Ikupa jambo hili limeanza kufanyiwa kazi na kwa kweli tutalitekeleza ili kuona kwamba haki hiyo inapatikana na ninamuomba sana aamini anajua mengi tumekwisha kuyafanya hata hili tutalifanya amuachie shilingi Mheshimiwa Harrison Mwakyembe na sisi tutakwenda kulitekeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, una jambo la kuongeza?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kwa kweli

hakuna ambaye anampinga Mheshimiwa Ikupa, Serikali inaelewa. Katika jambo hili Serikali ilitaka ioneshe uongozi wa mfano, hatukutaka tushinikize vyombo vya *private* wakati sisi wenyewe vyombo vyetu havijaanza hilo. Kwa hiyo, kama unakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa agizo mapema hapa hapa Bungeni kwamba hili lazima lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kupitia *TCRA* tumejipanga kukutana na wadau Mei, 2017 utakuwa ni mkutano pamoja na vyama vya walemavu na vilevile tutakuna na vyombo vya waandishi wa habari na wadau mbalimbali. Hili suala tumelichukulia *very seriously.* Tutaanza kwa kuajiri wachache tu kwa ajili ya vipindi vichache kama taarifa ya habari tu, kwa sababu tunahitaji watu zaidi ya sita kwa kituo kimoja cha *television,* hawakuwa wengi tunaendela ku-*train.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ikupa, *commitment* ya Serikali umeisikia.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wameniunga mkono na kwa umuhimu ambao wameuona kuhusiana na jambo hili na niendelee tu kuishukuru Serikali kwa majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu bila utekelezaji unakuwa hauna moto sana. Kwa hiyo, niiombe Serikali kile ambacho kimeahidiwa kwenye Bunge lako Tukufu, basi kitekelezwe kwa haraka kwa sababu hiki ni kilio cha muda mrefu. Narudisha shilingi ya Mheshimiwa Mwakyembe ili aendelee kufanya kazi katika Wizara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimuomba Waziri anifafanulie kuhusu suala la sanaa za ufundi ambazo zinamchanganyiko mbalimbali kwamba kunawachongaji, kuna tingatinga, wabunifu, wasusi na wengine wengi. Na

wachongaji hasa hawa mara ya kwanza na wewe unafahamu walikuwa wakifanyia shughuli zao nchi zima, *center* yao ilikuwa Nyumba ya Sanaa, na eneo lile walipewa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza, wakanyang'anywa. Bado walipewa eneo la Mwenge baada ya kupisha ujenzi wa Ally Hassan Mwinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameendelea tena kunyang'anywa eneo hilo, sasa hivi Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na wadau ambao hawafahamiki wanataka kuwanyang'anya eneo lile. Wanapoenda kutaka kusafirisha bidhaa zao nje, bado wakifika *airport* wananyang'anywa vinyago vyao, wanaponyang'anywa Tume ya Ushindani huwa inachoma bidhaa zinazonyang'anywa, lakini vinyago hivi hujui hata vinachomwa wapi ...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hali imekuwa ni mbaya sana kwenye sanaa, kwenye tasnia hii ya uchongaji. Nilikuwa naomba Mheshimiwa anifafanulie vinginevyo naenda kutoa shilingi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Martha Mlata kwa kulileta suala hili na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba mwishoni mwa mwezi wa nne, Mheshimiwa Waziri aliniagiza nitembelee eneo hilo analolizungumzia Mheshimiwa Mlata na nilifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba yote anayoyazungumza ni ya kweli, tuliyakuta pale yapo na tulichokubaliana na Mheshimiwa Waziri ni kwamba baada ya Bunge hili, baada ya Bunge la bajeti tuweze kukutana

sasa na wadau wote wa eneo lile la sanaa za ufundi ili kusudi tuweze kupanga mikakati ya kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli matatizo ni mengi ikiwa ni pamoja na matatizo ya tozo za maliasili ambapo tulikwishazungumza pia hata na Wizara ya Maliasili na tukakubaliana kwamba hata tutakapokwenda mara ya pili itabidi twende pamoja, Wizara ya Habari pamoja na Wizara ya Maliasili na wao walitambua kwamba ni tatizo. Ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, lakini bado hali ni tete. Naomba Waheshimiwa Wabunge wanisaide tujadili jambo hili ili tuweze kuokoa tasnia hii kwa sababu pale walipo hakuna amani pale Mwenge. Watu wanafanya kazi lakini hawajui hatima yao itakuwa ni nini naomba kutoa shilingi, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Mabula, Mheshimiwa Susan vipi huku vipi haliwahusu hili? Halina nguvu? Tuanze na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata, kwa sababu ndugu zangu Wamakonde wengi ndio wachongaji wazuri wa vinyago. Pia jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri limenihuzunisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wanapojibu hoja ukiwabana humu ndani wanasema, ikishapita bajeti, baada ya bajeti, kwa nini hawaji na hoja kwamba tulifanya kabla ya Mkutano huu wa Bajeti maana yake ni kama wanatulaghai tuwapitishie bajeti, ili *business* iwe as *usual. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata kwa sababu majibu aliyotoa Naibu Waziri siyo majibu ambayo yanaonesha kwamba mbele kuna utekelezaji wa suala hili. Naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi namuunga mkono Mheshimiwa Martha Mlata kwa sababu hii ni Wizara ambayo inajumisha sanaa, wakati mwingine pengine tunapitiwa tunadhani kwamba sanaa ni masuala ya filamu ni masuala ya muziki, hata hawa wasanii wanaochonga hizi zana za namna hii ni watu muhimu. Kwa hiyo, naomba kabisa kama walitoka kule kulikokuwa Nyumba ya Makumbusho, sasa wapo Mwenge wanataka tena waondolewe, Serikali iseme wazi kwa sababu hii pia ni chanzo cha mapato lakini pia ni kivutio cha utalii. *(Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niunge hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata mkono, kwa sababu ukiangalia kwa kweli kila sanaa ina kazi yake na kila kazi ina ubunifu wake. Mtu huyu amebuni kwa kiwango cha kutosha, sasa kutokana na majibu haya mimi naomba Mheshimiwa Waziri ni mwanasheria atusaidie ni namna gani hasa ya kuwasaidia hawa wachongaji ili sanaa hii iweze kuwa na mashiko na watu waione ni kazi kama kazi zingine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mabula.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hoja kwa Wizara husika, pia katika hii hoja ya Mheshimiwa Mlata naomba kusema pia ninatambua na ina mashiko kwa namna alivyoiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba pengine taarifa walizonazo siyo sahahi. Siyo kweli kwamba Wizara ya Ardhi inataka kuuza kiwanja kile, Wizara ya Ardhi imeweka zuio ili kile kiwanja kisiuzwe. Kwa sababu tunatambua wazi na tuna-*records* ambazo zinaonesha kiwanja kile kilitolewa na Mheshimiwa Rais enzi hizo kwa ajili wa hao wasanii wachongaji. Kulitokea mgogoro kati ya wachongaji na wale wauzaji, Serikali ikawashauri waunde chama ambacho kita–*accommodate* wote wachongaji na wauzaji ili waweze kumiliki kiwanja kile Namba Moja na Namba 13 Kitalu Namba 46 pale Kijitonyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho wanatakiwa kufanya wao wazingatie kila ambacho Serikali ilielekeza na Rais wa Awamu ya Nne aliridhia kuwanyang'anya wale walikuwa wanaitwa CHAWASAWATA ambao walikuwa ni wachongaji tu, walikuwa wakiwatenga wale wauzaji na akasema kile kitakachoundwa kitakabidhiwa. Vile viwanja bado kwa kazi ile ile ya uchongoja na uuzaji na siyo uchongaji tu.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Martha Mlata kwamba eneo lile bado lipo kwa kazi ile, linatambuliwa na Wizara na Wizara imeweka zuio ili wale CHAWASAWATA wasiuze hiki kiwanja na wenzao wakakosa. Kwa hiyo, naomba tu arudishe tu shilingi kwa sababu liko katika mikono salama.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kuna nyongeza?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki moja tu baada ya kuingia hii Wizara nilimtuma Mheshimiwa Naibu Waziri kuwatembelea wasanii wetu hapo Mwenge. Alikutana na uongozi wao na akaorodhesha matatizo yote nilipopata hiyo taarifa niliwakaribisha hapa Dodoma uongozi mzima wa ndugu zetu hao wa Mwenge ulikuwa hapa wakati nawasilisha bajeti. Tumepanga vikao vya kuweza kupitia kila tatizo kwa kuishirikisha Wizara ya Ardhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, pale kwenye jengo la sanaa ilikuwa siyo vinyango tu, kulikuwa na ngoma za asili, *entertainment,* sasa na *compensation* ukifikiria na eneo lile ambalo lina *commercial command* mmekuja kuweka Mwenge, kuna habari yoyote ya kuwafidia watu waliopewa eneo lile ili chama hiki sasa na watu wale waone na wao ni sehemu ya Taifa hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *volume* ya *document* nilizoletewa hatuwezi kulisema hapa, hebu tuache, tukae

na wahusika, mimi nina uhakika kwa sababu dhamira ni nzuri upande wa Serikali, tutalimaliza tatizo hilo katika muda siyo mrefu.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru wote ambao wamechangia hoja yangu, lakini nikushukuru na wewe kwa sababu umeongezea hoja ambayo ni nzito. Kwa kweli naomba tu nisisitize kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe wewe ni mwanasheria uliyebobea hebu naomba uiokoe tasnia hii. Kwa sababu ile kupigwa dana dana wakienda, kwanza uniambie hata hivyo vinyango vikikamatwa kule wanataka watoe nje vinachomwa wapi, vinapigwa mnada wapi, yaani tasnia imetelekezwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, amenihakikishia kwamba Wizara ndiyo ambayo imezuia pasiuzwe nilikuwa naomba pasiuzwe kweli. Wale wahusika waachwe, jengeni kituo cha Kimataifa ili wale watu wafanye biashara zao pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudisha shilingi yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Masikio ya Watanzania husikia waandishi wa habari wamepata matatizo hayajaanza jana, hayajaanza juzi, utakumbuka tuliwahi kusikia hapo awali, Ndugu Saed Kubenea akimwagiwa tindikali, tuliwahi kusikia Absalom Kibanda akitekwa, kuteswa na kuumizwa. Lakini hivi juzi tumesikia kituo cha *Clouds tv* kimevamiwa, juzi tena waandishi wa habari waliohudhuria kwenye mkutano wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kule Mabibo wakavamiwa, wakapigwa na wengine wakaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo ya Serikali hasa kwa matukio haya mawili ya hivi karibuni, ni kitu gani wamefanya kuhakikisha kwamba wamelishughulikia

jambo hili kwa *level* ambayo aliyevamiwa atajiridhisha kama kweli kuna Serikali nyuma yake, lakini aliyetenda atajutia kwa nini alifanya hicho alichokifanya. Kama nisipopata majibu ya kuridhisha nitashika mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama hizi dakika mbili zitatosha kueleza haya yote mawili, lakini la kwanza ni kwamba Serikali, Wizara hasa ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo haijawahi hata siku moja kufurahia vitendo vyovyote vya unyanyasaji wa waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilipotokea tukio la *CUF* Wizara tumetoa *statement* kali sana, lakini magazeti nadhani yanapenda kusikia tu tukilaumiwa, lakini vilevile tumelifuatilia hili suala Idara ya Polisi, sisi hatuwezi kupeleleza, watakapokamilisha tutachukua hatua kali *accordingly*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine ameliongelea la *Clouds* huyu ndugu yangu hapa, sijui kama utanipa muda wa kutosha, lakini kwa kifupi sana tulichofanya Wizara ni kikubwa na tulikuwa tayari sasa tuweze kukiwasilisha rasmi, sasa hivi suala hilo limeshafikishwa mbele ya chombo ambacho kisheria tunakuita *Quasi-Judicial Body* ambalo ni Baraza la Tume ya Maadili ambalo linakaa Kimahakama hatuwezi wakati Sekretarieti ya Maadili inafanya uchunguzi na sisi huku tunajadili suala hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado siridhishwi na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake, kati ya mambo ambayo alikuwa anafahamu kabisa kwamba yako *hot* na Watanzania wangependa kupata maelezo ya kina ni hizi *issues* za uvamizi wa waandishi wa habari, kukosa

kuyaweka haya kwenye hotuba yake, kuyaelezea kwa kina na kutaka hizi dakika mbili ndiyo atoe maelezo ya kina, maana yake hakuona kama jambo hili ni jambo zito ambalo linahitaji kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kwa pamoja, mniunge mkono tujadili hoja hii, ili Serikali iwahakikishie usalama waandishi habari wanapokuwa wakifanya kazi zao. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Huku vinyago hamtaki hizi mnataka. Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Kasuku Bilago, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Kabudi na Mheshimiwa Mbarouk. Tuanze na hawa kwanza, Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe taarifa kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Wizara iliyoko mbele yetu ni moja ya Wizara zetu. Vilevile ni miongoni mwa Wajumbe waliofika *Clouds Tv.*

**MWENYEKITI:** Suala ambalo liko kwenye uchunguzi mliache, suala la mambo mengine unaweza kusema, ukweli ndiyo huo Kanuni ni Kanuni Mheshimiwa Mnyika, Waziri amejibu *issue* wameshafanya uchunguzi Serikali, wameishaipeleka kwenye Baraza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** *No,* msinibishie. Mheshimiwa, usitafute Kanuni saa hizi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana hii *issue* haipo mahakamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago *issue* ya *Clouds* limeshapelekwa kwenye chombo maalum na taarifa imepelekwa. Kwa hiyo, sasa tuzungumze hayo mengine. Tuendelee.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sijui ilikuwa ni taarifa au ilikuwa ni nini, lakini niseme *issue* ya *Clouds Tv* haiko mahakamani kwa hiyo inaruhusiwa kujadiliwa humu kama *issue* ya kawaida. Mimi ni miongoni mwa Wajumbe waliofika kwenda kuona walivyovamiwa waandishi wa habari wa *Clouds Tv*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja, Mheshimiwa Bilago hebu kwanza kaa chini. Waheshimiwa Wabunge tuelewane, Waziri amejibu vizuri, taarifa ya *Clouds* Wizara imeshaipokea wameshaifanyia kazi na imeshapelekwa kwenye chombo cha maamuzi iende ikashughulikiwe, sasa humu ndani tuna-*discuss* kitu gani.

Mheshimiwa Bilago hiyo ndiyo *ruling* yangu, sasa tuende kwenye hoja nyingine ya magazeti, Kama huna kaa chini. *(Makofi)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mjumbe wa Kamati ninayo haki ya kueleza jinsi waandishi walivyotekwa na kuvamiwa wa *Clouds Tv.* Taarifa ya Kamati tulizungumzia.....

**MWENYEKITI:** Mheshimia Bilago hebu kaa kwanza. Haki yako, unajua usitake kujibishana vitu vya haki na vya msingi, hiki kitu kimeshakwenda kwenye chombo cha maamuzi, subirini sasa maamuzi yakiwa hayawaridhishi ndiyo mtaanza ku-*discuss* hii kitu, huu ndiyo utaratibu. Waheshimiwa msitake ku-*complicate* vitu *unnecessary*. Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bilago anazungumza kwamba hiyo siyo mahakama, lakini Katiba hii Ibara ya 13(6) na hii Ibara inazungumza juu ya usawa mbele ya sheria inasema; "Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamalaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba:

(a) Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote inapohitajika kufanyiwa maamuzi na Mahakama au chombo

kingine chochote kinachohusika *underline* chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya muktadha wa hii Katiba si Mahakama tu kama Mahakama, hata haya Mabaraza kama huko ili suala lililopo. Ndiyo Katiba yenyewe ilivyo na anapaswa asikilizwe huko asije akaonewa. Sasa mnavyozungumza humu ndani mnaingilia kule, kwenye sheria tunaita *mis-trial* mnataka kumhukumu kabla chombo kile ambacho kimewekwa mahsusi kwa ajili hiyo hakijamuhukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge, katika hili ni suala la msingi hakuna haja ya kubishana hapa. Sasa kama wote tutageuka kuwa Mahakimu hapa sijui na vitu gani. Kwa hiyo, naomba kushauri kwamba nakubaliana na mwongozo ambao umekwisha kuutoa na ndiyo ushauri wangu kwamba tuliache hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoche jambo hili limepelekwa na Meya wa CHADEMA Ubungo kama hivyo msingepeleka kule mlete hapa. Kwa hiyo, hamuwezi mkafanya hivi, mmepeleka ninyi wenyewe kule halafu mnaleta tena hapa, haiwezekani, lazima tuheshimu. Naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakupa nafasi Mheshimiwa Mnyika, ngoja Mheshimiwa Bilago kaa kwanza. Mheshimiwa Mnyika nakupa nafasi ujibu kama una hoja kuhusu *procedure.*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ambayo inazuia Bunge kujadili ni Kanuni ya 64(1)(e) ambayo inazungumzia mambo yaliyoko Mahakamani. Haihusiani kabisa na jambo ambalo lipo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, amemtaja Meya wa Ubungo, binafsi nilikaa na Meya wa Ubungo kabla hajapeleka hayo mashauri, shauri lake limejikita katika suala la Bashite ku-*forge* vyeti, suala la uvamizi wa *Clouds FM* siyo jambo kuu katika shauri lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa zaidi Mheshimiwa Waziri amepewa ripoti na mtangulizi wake Mheshimiwa Nape, ambayo imeeleza bayana ukiukwaji wa sheria uliofanyika. Kama Waziri angekuwa hajaridhika na hiyo ripoti, kwa maana ya kwamba ripoti haifai, Waziri ndiyo angeeleza utaratibu gani umefuatwa sio Meya Boniphace Jacob ambaye amepeleka mashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokitaka hapa Bungeni sasa hivi ni majibu ya hatua ambazo wasimama na naona Waziri wa Sheria anataka kusimama. Waziri wa Sheria utakaposimama tueleze, aliyevamia *Clouds FM* amekiuka Kanuni ya Adhabu Kifungu cha 89 kwa kutoa vitisho, amekiuka *Penal Code* Kanuni ya 89, amekiuka Kanuni ya 285 kwa kuingia na silaha, amekiuka sheria ya...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha.

Mheshimiwa Mnyika unajua tatizo lako unakaa sana nje ya Bunge halafu ukirudi unajisahau kama uko Bungeni, sasa natoa nafasi nyingine ya *procedure* siyo ya kuchangia, nani anataka kusimama mwanasheria mwingine huko, halafu nimpe Waziri wa Sheria, Mheshimiwa Msigwa kwenye *procedure* siyo kuchangia. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisimamia...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijamaliza!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago kaa chini hatujaanza mjadala, subiri kwanza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisimamia bila kupoteza muda katika masuala aliyozungumza Mheshimiwa Mnyika katika Kanuni zetu, tunachozungumzia hapa kwenye *proceeding* unazozisema, Mwanasheria anachanganya mambo mawili. Suala la Boniphace ni suala la vyeti na mali ambazo amedanganya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, mimi siko kwa Mwanasheria wala siko kwa nani. Waziri wa Habari amesema uchunguzi uliofanywa mwanzo na Waziri Nape, wameuchukua, wao wameongeza uchunguzi mwingine wamepeleka kwenye chombo kingine ambacho kina mamlaka ya kufanya maamuzi ya masuala ya habari, hiyo ndiyo kauli ya Waziri au siyo hivyo?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Ngoja basi, Waziri umeipeleka wapi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokieleza hapa ni kwamba nilipokea ile taarifa, nikaiona ina mapungufu, tumeifanyia kazi ili kusikiliza upande wa pili, lakini wakati tupo katika kusaili kuikamilisha huyu Meya wa Ubungo akapeleka hili suala Sekretarieti ya Maadili.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *No, no!* sikilizeni, haya ni mambo ya kisheria tunakaa darasani *brother,* siyo ya kubobea tu.

**MHE: JOHN J. MNYIKA:** Mashauri mangapi yamekuwa kwenye.......

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, huwezi kusimama tu kama upo sokoni, kaa chini. Waheshimiwa Wabunge, hebu sikilizeni kwanza. Endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa nimejiandaa chini ya kifungu cha 24(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kuitwa na hilo Baraza ambalo linakuwa *chair*ed na Jaji wa Mahakama ya Rufani niweze kueleza nimegundua vitu gani na kuiwasilisha. Sasa nikifanya hivyo hapa kuna haja gani ya kuwa na Baraza la Maadili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa haya endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Mheshimiwa Mwakyembe anajaribu kukimbia hoja. Hili ni Bunge tunao wajibu kama Bunge kuihoji Serikali, maadam hatujavunja sheria kwa mujibu ya Kanuni ambayo inatukataza tusizungumze mambo ya Mahakamani. Kama vile haitoshi Kamati ya kina Mheshimiwa Bilago hili suala ililileta humu ndani, kwenye hotuba yao walilileta humu ndani, kwa hiyo lilijadiliwa humu ndani na halikutolewa wakati wa kujadiliwa. Hapa ni Serikali kutaka kukimbia majukumu na sisi ni Bunge, sasa tumekuja kufanya nini hapa? Mimi ninachoomba hili suala tulijadili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, Mheshimiwa Kubenea hebu kaa kwanza. Sasa hivi tumezuia mijadala tupo katika *procedure*, subiri basi kwanza mbona una nini? Mheshimiwa Kabudi.

**MHE. SAED A. KUBENEA**: Mheshimiwa Mwenyekiti Taarifa tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge subiri utapata nafasi yako.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi ulioutoa ni sahihi kabisa. Na mimi ningemshangaa sana Waziri wa Habari kama angetoa jibu tofauti. Kwa sababu moja ya masomo ambayo Dkt. Harrison George Mwakyembe amelifundisha ni *Administrative Law, it is a lecture room*.

**MBUNGE FULANI:** *No*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** *It is.* Sekretarieti ya Maadili ya Umma inapofanya kazi yake ya kusikiliza mambo, inakuwa na sifa ya kitu kinaitwa *Quasi-Judicial* na ikishakuwa *Quasi-Judicial* tayari imekuwa Mahakama, sasa tuache uzumbukuku. Tuache uzumbukuku! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana shauri hilo litakaposikilizwa kwa mujibu wa kifungu cha 24 Waziri wa Habari ataitwa mbele ya Baraza kwenda kutoa ushahidi na kuhojiwa. Kwa hiyo, hayo wanayoyataka sasa ile Sekretarieti ambayo siku hizi iko wazi na Mwenyekiti wake ni Jaji wa Mahakama ya Rufaa, ataitwa ataeleza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, uamuzi wako ulikuwa sahihi ile ni Mahakama na suala lile lipo. Mashtaka yaliyopelekwa yanahusu maadili, yanahusu vyeti yote hayo yameorodheshwa kwenye yale mashtaka, ina maana Sekretarieti itayahoji yote hayo na Bunge tukiamua kuyajadili sasa tunaharibu hiyo hoja. Ndiyo maana tunasoma sheria miaka minne tuache uzumbukuku!*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika kaa basi kwanza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika hakuna, huwezi kusimama bila kuruhusiwa, hebu kaa kwanza. Unajua Mheshimiwa Mnyika unaweza kuwa na hoja nikakuruhusu uiseme kwa utaratibu unaotakiwa, wewe nitakupa, Mheshimiwa Kubenea nitampa subirini tu. Ahsante. Tuendelee Mheshimiwa Kubenea.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Subiri kaa chini. Mheshimwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa *order please! Order in the Parliament, Law Makers should not be Law Breakers*.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nimemsikiliza vizuri sana Profesa Kabudi na nimemsikiliza sana Dkt. Harrison Mwakyembe na nimemsikiliza Mheshimiwa Mnyika. Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo imepelekewa mashtaka hayo, kwanza hukumu yake haisomwi hadharani. Kwa hiyo, siyo kweli pamoja na kwamba hicho chombo kina mamlaka ya kimahakama lakini siyo kweli kwamba kinafanya kazi kama Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Bunge hili katika Bunge lililopita lilijadili suala la *Escrow* humu ndani, wakawatuhumu watu humu ndani, wakawapeleka watu hao kwenye Tume ya Maadili na Tume ya Maadili ikafanyia kazi malalamiko ambayo yalitolewa ndani ya Bunge hili. Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mama yangu Tibaijuka walipelekwa kwenye Tume ya Maadili kwa mchango uliotokea kwenye Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo Waziri anazuia tusijadili kuhusu Bashite kwa sababu eti suala hilo liko Tume ya Maadili, Tume ya Maadili na Bunge ni vitu viwili tofauti. Katiba yetu na Kanuni zetu zinataja Mahakama, zinataja Rais, hazizungumzii mahala popote Tume ya Maadili, Mwanasheria

Mkuu anakuja anatafsiri yake yeye. Mwanasheria Mkuu kazi ya Mahakama ndiyo kutafsiri siyo yako wewe, wewe utusaidie hapa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kubenea. Mheshimiwa *AG*.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa Mnyika, subiri. Sugu sema.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Sheria, kwanza zumbukuku mwenyewe na Mawaziri wenzako. Pili, hii siyo *lecture room,* hii ni *debate room*, *if you didn't know*. *(Kicheko/ Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba, Taarifa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimueleze kwamba bahati nzuri na kamusi ipo, mimi ni zumbukuku wa muziki, kwenye muziki mimi ni zumbukuku, lakini siyo kwenye sheria, neno zumbukuku halina maana hasi lina maana chanya. Kwa hiyo, kwenye muziki mimi ni zumbukuku lakini siyo kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusu *lecture room*...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kabudi kaa chini. Mheshimiwa Mtolea funga hoja yako.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana hoja hii haikupewa nafasi ya

Waheshimiwa Wabunge kuijadili kwa kina ili kuweza kuibana Serikali iweze kutoa majibu. Sasa kwa sababu tumekosa fursa ya kuijadili mimi naomba ulielekeze Bunge lituhoji ili waandishi wa habari wenyewe ambao tunawatetea wako hapa, waone ni Wabunge wangapi wanapenda kuona wanaonewa wanapatwa na madhara haya na Wabunge wangapi tuko tayari kuwatetea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa, kwanza ngoja, hoja yako wewe ni ipi, hoja yako ni ipi ili tulihoji Bunge waandishi wanaonewa au kitu gani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, subirini, tulieni hapo wala msipate taabu.

**MHE. ABDALLAH O. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nilikuwa nahitaji *commitment* ya Serikali katika kuwalinda waandishi wa habari hasa wanapokuwa kazini. Sasa Serikali imeshindwa kutoa hiyo *commitment* na imesema kwamba iko kwenye *Quasi-Judicial,* iko hivi majibu ambayo hayawafanyi waandishi wa habari wajione wako *safe* katika kutekeleza majukumu yao katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu mjadala haukupata muda mzuri, haukupewa nafasi vizuri ya kujadili, kwa sababu uliusimamisha mjadala ikawa vinajadiliwa vifungu vya kisheria na baadae umetoka huko umerudi kwamba nifunge hoja yangu, sasa ndiyo naomba uhoji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea ume-*modify* hoja yako, umeileta kwa maana sasa unataka kuiweka kwenye *flow* kama kuleta lawama fulani, kitu ambacho hakipo. Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tumekuwa na mjadala wenye afya kwa

pande zote mbili, lakini msingi wa kusimama kwangu ni utaratibu wa kikanuni. Wakati hoja hii inaanza kujadiliwa ilikuwa ni hoja ambayo wewe ulishaitolea maelekezo kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapata shida tunahojiwa sasa kwa hoja ile ambayo kwa mujibu wa Kanuni haikupaswa kujadiliwa ama tunahojiwa kwa mujibu wa hoja ya mabadiliko ambayo anataka kuieleza Mheshimiwa Mbunge kwa sasa? Hapa ni suala la kikanuni ni lazima tuelewane na ndipo tuweze kuhojiwa kwa sababu tayari Kiti chako kilishatoa mwongozo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *ruling* yangu ni *very simple*, Serikali imeshatoa majibu mazuri na majibu kesi hii iko katika mjadala maalum, mtoa hoja hajaridhika na majibu ya Serikali. Kikanuni ni kupiga kura tu, *ruling* yangu ni kupiga kura tu. Kwa hiyo, wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mtolea, ilishajadiliwa, nilishafunga mjadala.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waliosema siyo wameshinda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante niseme mwanzoni kabisa kwamba nakusudia kukamata mshahara wa Waziri endapo nitakachokisema hakitapata majibu yenye uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Serengeti Boys* wamefanikiwa kucheza fainali za Afrika wanaanza mwezi huu na wamekuwa alama ya Taifa, ili alama hiyo tuiendeleze iwe kinyume na ambavyo tulipoteza ile alama ya vijana wa *Copa CocaCola* walivyochukua ubingwa Brazil na wale vijana wa mitaani walivyochukua ubingwa Brazil ni lazima tuwe na mkakati maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua msimamo wa Serikali kwa hoja yangu kwamba vijana hawa wakirudi tuweke mkakati wa kuwaingiza ama kuweka kanuni ya kulazimisha klabu zote za *Vodacom Premier League* vipokee walau vijana wawili na Serikali ikishirikiana na *TFF* na wadau kwa maana ya wadhamini wawahudumie wakiwa kwenye vilabu hivyo kwa namna ya kuwatunza, ama kuwapeleka kwenye klabu mbili au tatu zinazowania kuingia *Vodacom Premier League* na Serikali na wadhamini.....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oscar Mukasa, zungumzia jambo moja tu.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba vijana wa *Serengeti Boys* watakavyorudi Serikali ikae na wadhamini na *TFF* kuwaingiza kwenye kila klabu kwa kanuni za *Vodacom Premier League* walau wawili-wawili au watatu ili tulazimishe kuwatunza wakiwa huko kwa kushirikiana na vilabu na Serikali. Vinginevyo tutawapoteza kama tulivyowapoteza wale wa *Copa CocaCola* na wale wa mitaani, kama nilivyosema endapo sitapata majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi na kuomba wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mukasa nashukuru sana kwa ushauri wako mzuri, lakini naomba nikuhakikishie kwamba ni dhamira ya Serikali kuiona timu ya Serengeti ikirudi baada ya mashindano haya ambayo yanamalizikia India Novemba ambapo najua tutakwenda tuendelee kuilea hii timu kwa mazoezi kwa sababu hiyo ndiyo timu yetu ya Taifa kwenye *Olympic* 2020.

Kwa hiyo, suala la kwamba tukae chini kulazimisha waingie kule, hilo halitakuwa na afya, timu zenyewe kubwa zikiangalia kiwango cha wale vijana, wao wenyewe watakuwa wanagongana mlangoni kuwatafuta, lakini tutahakikisha kama Serikali hawa vijana tunawa-*maintain*

kwa ajili ya 2020, wakati huu sasa tume-*develop* timu ndogo ya vijana wa miaka 13 ambao tunawaandaa kwa ajili ya michezo ya vijana wa *Under 17* mwaka 2019 ambapo Tanzania tutakuwa wenyeji wa michezo ya *AFCON* Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaongelea dhamira, mimi nachanganya hiyo dhamira na historia. Mwaka 2008 vijana wetu wa *Copa CocaCola* walichukua ubingwa Brazil, hivi leo tunavyoongea kati yao ni watatu tu ambao tunajua wako wapi. Himid Mao yuko Azam na mwingine anaitwa Kenny Ally kama sikosei yuko *Mbeya City* na mmoja yuko Zanzibar sasa hivi ni mvuvi, hakuna zaidi ya hao ambao tunajua wako wapi. Pia vijana wa mitaani nao wakachukua ubingwa Brazil mwaka 2014 hakuna hata mmoja tunayejua yuko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ni lazima tuiambatanishe na historia ili tuone kama kweli kinachosemwa kitatekelezeka, mimi naomba kutoa hoja Wabunge waniunge mkono tujadili hili, ili tuweze kuweka vizuri mawazo yetu kwa pamoja. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Lugola, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Boni, Mheshimiwa Nswanzugwako, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Rehani. Mheshimiwa Kubenea umo au umejitoa? Unangoja Mengine? Hata Mheshimiwa Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mukasa ukiitazama kwa sura moja ni nzuri lakini ukiitazama kwa sura mbili hoja yake siyo nzuri sana. Ninasema hivyo kwa sababu tunahitaji Serikali iweke mfumo na utaratibu mzuri wa kuweza kuwapata vijana abao watalisaidia Taifa hili na vijana wengi bado wako kwenye timu ambazo ziko mikoani ni wazuri sana, tena wakati mwingine wanacheza kuliko hata wa *Serengeti Boys.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ambao ukitumika utaratibu mzuri usio wa upendeleo tunaweza tukawalea kwenye zile timu ambazo zinacheza mikoani. Kwa hiyo, lengo hapa Serikali iwalazimishe kila klabu kwenye mikoa wawe na timu za vijana wadogo ambao Serikali itakuwa inawasaidia kuwalea, kuliko ku-*target Serengeti Boys* peke yao hatutafanikiwa. Kwa sababu *Serengeti boys* peke yao hawawezi wakalifikisha Taifa hili mbele. Vijana wako kule Mwibara, wengine wako Lindi, wengine wako Nachingwea. Hoja yake ni nzuri lakini Wizara ilitazame kwa mapana kuliko ku-*target Serengeti Boys*.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mukasa kwa sababu ni kweli hata hawa wenzetu wa *Airtel Rising Star* wanaandaa vijana lakini baadae vyombo vyetu vinashindwa kuwatunza. Nikubaliane naye kabisa kwamba tena ninaweza nikaenda mbali zaidi kwamba badala ya kuwaweka katika vilabu vyetu vya hapa nchini, ikiwezekana Serikali iwatafutie mawakala wa nje hawa vijana waweze kwenda huko, baadae watatusaidia hata kwenye timu ya Taifa ya wakubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mukasa. Ninaloliona mimi ni tofauti ya kulea, leo tukisema kwamba tuanze kutafuta wachezaji kutoka huko maeneo mengine tofauti, hao vijana wa *Serengeti Boys* wameshapata *exposure*, wameshakwenda mbali. Kwa hiyo, hoja hapa kwa Serikali ni namna gani tuwatunze, tukisema tuwapeleke kwenye vilabu kwa kuweka shinikizo haitawezekana kwa sababu vilabu navyo vina masharti yake, kwa bahati mbaya zaidi duniani hakuna Serikali inayoingilia mambo ya michezo.

Kwa hiyo, ninachokiona ni kwamba tuwatafutie hao vijana nafasi ya kwenda kucheza nje, tuwatambue kwa

majina lakini tuwatambue kwa nafasi watakapokuwa wanacheza ili tunapohitaji tuwapate. Kwa hiyo, namuunga mkono kwa hoja hiyo lakini naona baadae tu arudishe shilingi ili Serikali ifanyie kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi namuunga mkono mia kwa mia bwana Mukasa.

Mheshimiwa Waziri hoja ya Mukasa hatutaki kusikia dhamira ya Serikali hapana! Anachozungumza mtoa hoja anataka *commitment* ya Serikali mnafanya nini na vijana hawa baada ya kutoka Gabon? Ndiyo hoja iko mezani, hii habari ya kuwa na dhamira, tutawalea tunasikia sana, tunataka *strategy* ili vijana hawa ambao wanafanya kazi nzuri wasipotee. Ndio hoja anayoijenga Mheshimiwa Mukasa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, wamesema mengi lakini ukweli ni kwamba hakuna mkakati endelevu wa kulea michezo katika Taifa letu, lazima wakati ufike sasa Serikali mje na *strategy* mezani hapa namna gani bora ya kuweza ku-*sustain* vijana hawa, ndiyo hoja ya Mheshimiwa Mukasa ambayo ni ya msingi sana na wala siyo dhamira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwamoto, ajiandae Mheshimiwa Rehani na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mukasa.

Tatizo kubwa ambalo lipo hapa mbele yetu ni kwamba Mheshimiwa Waziri ana vyombo ambavyo vinapaswa kufanya hiyo kazi likiwepo Baraza la Michezo la Taifa, lakini Baraza la Michezo la Taifa halipo kwa maana halina bajeti yoyote. Leo unapozungumza kwamba unataka kufanya hayo unayotaka kufanya itakuwa siyo rahisi.

Mheshimiwa Waziri tunakupa ushauri, umepata shilingi bilioni 28, hii ni fedha tu ya maandalizi ya timu ya Bunge ya mwaka huu ya mashindano ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikushauri Mheshimiwa Waziri umwambie Waziri wa Fedha michezo ya kubahatisha ya bahati nasibu ihamie kwako uwe na fedha, hayo unayozungumza mazuri hayatawezekana kama huna fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto hebu tusaidie bajeti ya *Bunge Sports* ni shilingi bilioni 21.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa mashindano mazima yale ambayo yanakuja kufanyika hapa, yanaweza yakazidi.

**MWENYEKITI:** Mashindano yale ya Afrika Mashariki?

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo na yanaweza yakazidi, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa aombe hela tumpe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami naunga hoja ya Mheshimiwa Mukasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiona Mheshimiwa Waziri kama nchi hakujawa na mipango sahihi inayoweza kuelezeka au tukapata moyo kwa vijana wale wa *Serengeti Boys* baada ya kurudi, kilichokuwa kinatakiwa tuone mwendelezo wa vijana wale ili baadae liwe tegemeo la timu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wale wakirudi tukiwaachia Simba na Yanga baada ya miaka miwili wale wamekufa hakuna kitu kitakachoendelea, kwa hiyo wazo la kutuambia tutakaa na vilabu hatukubaliani nalo, tunachotaka ma-*promoter* nje wapo na Tanzania wameshakuja mara nyingi Sweden, Belgium na nchi nyingi

tu za Ulaya zipo, tuwaendeleze tuwaite ma-*promoter* tukae nao tuwapeleke wale vijana wakaongeze vipaji vyao, watatusaidia nchi hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wenzangu sana, lakini nimepata shida kidogo kwamba hatutaki kupanga lakini tunataka kuvuna. Mimi nilidhani hoja ingekuwa tuna vijana wetu wa *Serengeti Boys* tumewekeza kiasi gani kifedha ili huko wanakoenda waende wafanye vizuri, sasa mnataka warudi ndiyo tuanze kupanga mikakati ya hao, wakati wameshaenda huko wameshindwa wakirudi ndiyo tupange mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani tumuombe Waziri awe na mkakati wa kifedha wa kuiandaa timu yetu huku inakoenda Gabon iende ifanye vizuri, halafu ndiyo tujadili namna tutakavyowasimamia hao vijana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mukasa na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye fainali za Gabon, wenzetu waliotangulia kule walitutaarifu kwamba mawakala wa timu kubwa duniani wanagombea hoteli kule. Sikutegemea kwamba vijana wetu ambao wanasifika sasa hivi Afrika ya Kati na Magharibi kwamba sasa waje tuanze kuwalazimisha kuingia timu sijui *Mbeya City, Serengeti*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu kwamba tumelichukua wazo la Waheshimiwa Wabunge kwamba tunahakikishe kwamba tunalazimisha timu zetu kuwa na vijana wa kuanzia miaka 18, 19, na 20 katika timu zao. Hilo tumelitengenezea Kanuni, tumelipeleka *TFF* tayari. Kwa upande wa Serengeti, naomba tusiwe *local* mno, tuka-*localize* kuhusu *future* ya hawa vijana. Waache hawa vijana, tunawaandaa kwa ajili ya *Olympics 2020* wakati huo huo

tutakuwa tunahangaika nao hawa watoto wapate fursa kama za Ndugu Mbwana Samatta, lakini siyo kwenda kwa Mwigulu *Singida United,* ndiyo tuishie hapo. Ahsante. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mugasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio Mugasa ni Mukasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na baadhi ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri na nawashukuru Wabunge waliotangulia. Naomba niweke rekodi kidogo hapo. Hatuna maana ya kuwafanya *local* vijana wetu wakirudi wote warudi hapa, kitakwimu ni hesabu ya kawaida tu haiwezekani mawakala wakachukua wote 23, lazima kuna watakaobaki. Pia historia inaonesha kwa maelezo ya Mheshimiwa Serukamba nataka naye nimpe taarifa kidogo, *Copa CocaCola* iliwekwa mikakati wakashinda, wakarudi hapa sasa hivi ni watatu tu tunajua wako wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana wa mitaani wakashinda Kombe la Dunia, sasa hivi hatujui hata mmoja yuko wapi. Kwa hiyo, uwezo wa timu zetu za watoto kushinda tayari tuna historia mara mbili wanashinda, kwa hiyo na *Serengeti Boys* watashinda. Kwa hiyo, lazima tuwaandae baada ya kushinda ili historia isijirudie. Narudisha shilingi kwa sababu tumepata fursa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bunge lako Tukufu linaendeshwa kwa Kanuni, pia Bunge lako lina Kamati za Kudumu za Bunge ambazo zinaendeshwa kwa Kanuni. Mpira wa miguu nimesikia sasa hivi hapa watu wamechangia sana, mpira wa miguu unatoa ajira, ni utalii, mpira wa miguu kama utasimamiwa vizuri, nchi hii itasifika zaidi. *TFF* ndiye baba wa vilabu vyetu hapa nchini. *TFF* kwa sasa ndiyo imekuwa kinara wa kutokusimamia Kanuni ambazo ziko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua *TFF,* kwa sababu imeshindwa kusimamia Kanuni zake, lakini imeshindwa kusimamia Kamati hata ile ya masaa 72...

**MBUNGE FULANI:** Aah!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Usiseme aah! Niache nizungumze. Nazungumza kama *Senator* humu ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kujua, Mheshimiwa Waziri tuambie, tungependa sana mpira wa miguu uendelee na uendelezwe, lakini kwa *TFF* hii ambayo sasa ndiyo inaboronga, inafinyanga Kanuni zake yenyewe. Nini msimamo wa Serikali? Na kama hutalijibu inavyotakiwa, nakusudia kundoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri na juzi uliambiwa kwenye michango wanasiasa wamejiingiza kwenye mpira na wanaharibu mpira, wanachafua mpira, tujibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata malalamiko mengi sana. Naomba nikiri kuhusu yanayoendelea kwenye shirikisho letu.

Nilichokifanya ni kuiagiza BMT iwaite *TFF* wakae nao na nafikiri tatizo moja nililo nalo kuhusu BMT ni kwamba wakati natoa agizo hilo siku tano zilizopita, walikuwa wamesambaa sambaa kidogo lakini nimetaka waniletee sasa taarifa ya matokeo ya haya malalamiko yote na wao wanasema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hicho tu, kumetokea na maneno mengi sana hapa, mengine kutoka kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge, yako mambo mengine ambayo tayari tumeshayawasilisha kwenye vyombo vingine vya Serikali kwa uchunguzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika bado na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Kama kweli tunataka mchezo wa mpira wa miguu uendelee na nchi hii inataka mpira wa miguu uendelee kwa *TFF* hii, chini ya uongozi wa viongozi waliopo hata kama tukidanganyana, kwa mfano, sasa hivi Mheshimiwa Waziri anasema amewaagiza BMT, BMT hao pia mpaka leo *TFF* haijapeleka mahesabu yake ya ukaguzi kwa mujibu wa BMT. Tena hao ndiyo uwapelekee...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka mpira wa miguu uendelee na mpira wa miguu huu utusogeze kwenye ajira na utalii naomba majibu ya kutosha. Hivi Mheshimiwa Waziri kwa *TFF* hii, wewe mwenyewe uko *comfortable nayo? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi naomba wenzangu mniunge mkono. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Bulembo, Mheshimiwa Mkuchika umo? Simama Mzee mdau wewe. Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa King. Tunaanza na Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoa hoja bila shaka *scenario* yake aliyoizungumza ilikuwa ina muktadha maalum ambao unatokana na maamuzi ya *TFF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema kwamba kwa aina ya uongozi wa *TFF* soka halitaweza kwenda mbele. Tusisahau kwamba *scenario* ambayo tumeitumia siyo soka zima la Tanzania na tukisema soka zima la Tanzana tukaweka katika *scenario* ambayo imetumika kuulizia swali au kutolea

hoja ina maana kwamba moja kwa moja tunajihusisha na vilabu viwili na maamuzi ya rufaa ya Kamati iliyokaa masaa 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo, moja kwa moja kama tunataka kulizungumzia soka la Tanzania ina maana kwamba hoja isiwe hii kwa sababu vinginevyo likizungumzwa jingine au ingekuwa iko upande wa pili wa shilingi ina maana kwamba isingekuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuomba mtoa hoja kwamba tungezungumzia mazingira yote ya mpira wa Tanzania na siyo *scenario* hii ndogo, kwa sababu hii ni *scenario* ndogo kabisa na haiwezekani moja kwa moja ikaenda ikalenga katika *TFF* nzima na katika bajeti hii. Kwa hiyo siungi mkono hoja yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mtoa hoja anajaribu kuonesha umuhimu wa soka, anajaribu kuonesha ni jinsi gani watu wanao-*deal* na soka wako *committed* na kuinua mchezo wa mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sasa imefika wakati Mheshimiwa Waziri aongee na watu wa *TFF* na naomba ku-*declare* na mimi vile vile ni Mwenyekiti wa *TFF* Mkoa wa Simiyu. Wadau mikoani hawaridhiki na hali halisi inavyokwenda, basi ifike wakati, mipango ya kuendeleza michezo ya soka iwe wazi, tuone. Kuliko sasa hivi unakuta kwa mfano, *premier league,* timu nyingi zinazocheza ni za kutoka Dar es Salaam wakati kule mikoani hakuna hizo timu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waangalie utaratibu mpya wa kufanya wachezaji wanaotoka mikoa mingine na wao waweze kuonekana, pawe na programu zinazoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *TFF* kuna mpango

mzuri sana ulioandaliwa na akina Sunday Kayuni wa kuweza kupeleka soka kwenye maeneo ya vijijini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kusema ni kwamba *TFF* ni wanadamu, wana mapungufu yao na wana jitihada zao ambazo wamezifanya. Kwa kuwa Waziri ndiyo kwanza ameingia Wizarani na kwenye rekodi zake sijawahi kumuona Dkt. Mwakyembe akishindwa, tumpe fursa hii, tumpitishie bajeti yake, aende pamoja na timu yake wasaidiane kurekebisha pale ambapo yatakuwepo mapungufu na kuendeleza kwa pale ambapo yamekuwepo yaliyo mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwanamichezo nimefuatilia sana michezo ya hapa Tanzania, mara zote siyo *TFF* tu, mara zote kwenye nchi yetu hii wanamichezo wa nchi yetu walio wengi huwa wanaona sheria imekiukwa pale tu wanapoona upande wao ndiyo ulioathirika. Sasa kwa namna hiyo tutamtwisha mzigo Waziri bila sababu, tutawatishwa lawama *TFF* bila sababu, lakini mimi niwaambie *TFF* wanafanyakazi kwa mazingira magumu sana ya watu ambao wanaitafsiri sheria kuwa njema pale ambapo imekuwa imewatendea mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira yale, kwa sababu huyu ni mwanasheria tumpe muda akatafsiri sheria kama zilivyo na zinyooke kama zilivyo. Hivi hapa sasa hivi tu ligi hii iliyotoka kupita tungeamua kuitafsiri vilivyo; kwa mfano, msimu uliopita wachezaji wawili wa Yanga na Makocha wawili, wachezaji watano wa Simba na makocha wao msimu mzima uliopita walifanyakazi bila vibali, lakini wao wanachoangalia ni kama vile klabu ya *African Lyon* hana kibali ndiyo sheria hiyo imekosewa. Sasa mambo hayawezi yakaenda namna hiyo, sasa mambo hayawezi yakaenda namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri Wabunge kwenye hili tumeona kuna mapungufu, tumeona *concern,* tumruhusu Waziri kwa sababu ndiyo kaingia tu ofisini, ndiyo kazi yake, aende akashughulike na mapungufu na siyo kwenye mpira wa miguu tu na siyo kwenye *level* ya Ligi Kuu tu, hata kwenye ngazi zingine ili aweze kuyafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ngoja, simama hapo hapo. Hii ya *African Lyon* mbona hatujaiona, unaijua wewe peke yako tu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *African Lyon?* Msimu uliopita kulikuwepo na hayo malalamiko ya *African Lyon...(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Basi kaa chini, tumeshakuelewa wa huko huko. Mheshimiwa Bulembo. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza Mheshimiwa Mbunge na Waziri aliyemaliza kuongea suala la Yanga usilitangulize sana kuliko maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri, mimi ni mdau wa *TFF,* nimekaa sana pale *FAT* miaka mingi sana nikiwa mdogo, naomba ni-*declare interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri umeagizaje Baraza la Michezo kushughulikia *TFF* ambao Baraza halina mamlaka nao? Katika chombo hapa Tanzania ambacho kinafanya mambo yake yakifanyika hapa kama kuna tatizo wanaenda Ulaya, Ubelgiji, Uswiss ni *TFF.*

Sasa Mheshimiwa Waziri unaagizaje wafanye nini? Kwa sababu Katiba yenu mliyonayo imempa mamlaka *TFF* kufanya mambo yake bila BMT kusema chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sheria iliyounda BMT ipo, tuirudishe hapa ndani, Msajili wa Vilabu ndiyo anapitisha Katiba ya *TFF,* aende aibadilishe Katiba ya *TFF*

awaambie Serikali ina mamlaka kwa sababu mchezo unachezwa Tanzania haki ya vilabu katika nchi hii ibaki kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumeliacha na watu wanaona rahisi, wanawapenda Simba, wanawapenda Yanga, hapana. Kuna kipengele kimeondolewa cha Serikali kushughulika na *TFF.* Kwa hiyo, unachokisema umewaagiza hawana meno ya kuuma. Hata wakienda mwaka mzima, Katiba ile imewaondoa wakiwa na shida wanahamia Uswiss. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo yaliyosemwa hivi unawezaje ukatunga Kanuni, ukawapa watu mamlaka, wakifanya maamuzi ndiyo watu mnaamka asubuhi. Mbona kuna Kamati nyingi humu za Bunge…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bulembo. Mheshimiwa Kakunda, wajiandae Mheshimiwa Chumi, na Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ndassa na nimesikitishwa kidogo na mchango wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa sababu amekiri kwamba kuna uzembe pale *TFF* ambao pengine unanufaisha baadhi ya klabu na baadhi ya klabu hazinufaiki, yeye mwenyewe kakiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tutaendelea na wazembe wa aina hii…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu kaa chini.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Unaingilia bila ruhusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzembe wa aina hii ambao Waheshimiwa Wabunge wamekiri humu ndani, ninaomba sana, mpira wa miguu unachezwa hadharani siyo chumbani

na katika sakata ya hivi karibuni watu wanakaa wanabishania kadi ya njano ilitolewa au haikutolewa, watu wazima na akili wamekwenda shule. Hiyo kadi ya njano kwa nini ibishaniwe wakati rekodi za mchezo zipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni uzembe wa hali ya juu sana wa *TFF* na ndiyo maana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ndasa hawa *TFF* inatakiwa Waziri awafanyie kazi kisawasawa kwa sababu wameshindwa kuongoza mpira wa nchi hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ndassa kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kwenye mchango wangu nilisema hapa, ili uweze kuhakikisha kwamba unaweza kwenda kucheza Kombe la Dunia au Kombe la Mataifa ya Afrika lazima uwe miongoni katika viwango vya *FIFA* kati ya namba moja hadi mia moja. Mpaka sasa hivi timu ambazo zinacheza katika hatua ya mwisho ili ziweze ku-*qualify* kwenda Kombe la Dunia Russia mwaka 2018 ziko mia moja na tano tu. Sisi hapa Afrika tulianza 54 tukang'olewa wengine zimebaki 20 tu. Sasa ili uwe katika mambo kama haya ni lazima uwe na *TFF* na chombo ambacho kinasimamia mpira katika maana halisi ya mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Neymar alipewa kadi nyekundu Barcelona wakawa wanahaha wakati El-Classico inakaribia ile kadi ifutwe. Chama cha Mpira cha Hispania hakijamuita Neymar kumuuliza, hivi ulipewa kadi au hukupewa kadi. Sasa ndiyo tunayoyasema kwamba mambo haya kama kuna *match commissioner* taarifa zifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TFF* inapoteza muda na ndiyo maana viwango vya *FIFA* hatupandi, ndiyo *point* yetu na nadhani ndiyo *point* ya Mheshimiwa Ndassa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nafasi yangu nampa Mheshimiwa Mwamoto, tafadhali. Kwa idhini yako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Kubenea kwa kunipa nafasi. Mimi ningeomba hivi, Mheshimiwa Waziri umeingia katikati, hali imeshaharibika kule *TFF* na wanakwenda kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, mahali pazuri pa kuanzia ni hapo kwenye uchaguzi. Lakini pia angalia Baraza lako la Michezo ndilo ambalo linatakiwa liwe karibu, lakini Baraza la Michezo halina fedha na halina ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono shilingi yako urudishiwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sana, wazo la Mheshimiwa Bulembo ni zuri sana. Huu ni muda pengine wa kusahihisha mapungufu na niombe tu Mheshimiwa Ndassa anielewe kwamba kisheria kwa sasa sina njia ya mkato na sina chombo kingine chochote kukipa kazi ya kupata maelezo ya kina ya kinachoendelea sasa hivi katika soka zaidi ya BMT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sina mamlaka Mheshimiwa Ndassa kubadilisha uongozi uliopo. Hii ni kazi ya wadau wa soka, ila naomba tu kwa Waheshimiwa Wabunge mniruhusu nipate hayo maelezo ya kina toka BMT na matokeo ya mchakato tulionao sasa hivi mtayaona. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ndassa, kubali tu maelezo ya Waziri analifanyia kazi ili mrudishie hela yake.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nikubaliane na maelezo lakini kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote hata wale ambao hawakuniunga mkono, nia yangu ilikuwa ni nzuri kwamba tunataka mpira wa Tanzania uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ile nilisema kwamba bahati nzuri au mbaya tupo wanasiasa hata humu ndani na mwingine amekiri wazi sasa hivi kwamba yeye kazi yake ndiyo hiyo, ameweza kutoa kibali cha kumtoa mchezaji gerezani au amemtoa kwenye kifungo wakati hakuwa na *working permit,* kasema mwenyewe hapa. Sasa tabia hii siyo nzuri sana, tukiendelea na utaratibu huu hata huko tunakokwenda kwenye timu yake hiyo nyingine sijui kama itafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni vizuri kanuni na sheria zifuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, namrudishia Waziri shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nishike mshahara wa Mheshimiwa Waziri japo sitegemei kwenda nao nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lililonisimamisha ni suala zima la lugha yetu ya kiswahili. Kiswahili ni lugha ya Taifa na tumeamua sasa hivi kutumia kiswahili ipasavyo, nimpongeze Rais wetu kwa kuwa mstari wa mbele katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wanajifundisha lugha kupitia vyombo vya habari kama *tv,* redio na hata magazeti. Kwa kiasi kikubwa Mheshimiwa ukifuatilia hao walioko kwenye vyombo vya habari ndiyo wanaongoza kukiharibu kiswahili chetu, ndiyo maana hata wakati mwingine tunashindwa kushindana na majirani zetu kwa sababu

ukiangalia wanazungumza vizuri wakati mwingine kushinda sisi. Ninachotaka kujua kwa Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuhakikisha kwamba anatoa sheria au kanuni au maagizo kwenye hivyo vyombo kuhakikisha kwamba wanaoajiriwa ni wale tu wanaojua lugha ya kiswahili kwa ufasaha kuwa kwenye vyombo vya habari ambavyo wananchi wanavisikiliza.

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli rai ya Mheshimiwa Ghasia ni nzuri sana siwezi kuikataa. Nimueleze tu kwamba sasa hivi Wizara inajiona imebeba mzigo mkubwa sana kwa sababu kwa kweli macho yote ya dunia yanatuangalia kama ndiyo *standard bearers* wa lugha ya kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kwa mfano, tumeshaanzisha kukusanya kanzidata ya wafasili na wakalimali wa lugha mbalimbali, siyo tu kiswahili lakini kutoka Kiswahili kwenda lugha nyingine nyingi. Kwa mfano, kireno, kifaransa, kichina, kijerumani na kispaniola, tumeshafanya hivyo na nimetoa mfano sasa hivi kwamba tumetoa kamusi mpya ya standard ambayo imeanza kukubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu waandishi wa habari wa Tanzania, kwa kweli mimi amenipa wazo zito la kwamba pengine tukae chini wa Idara ya Habari - Maelezo na wenzangu wengine wadau pamoja na vyombo vya habari hasa kwa magazeti ya kiswahili na vyombo vya habari vya kiswahili kwa kweli tumekuwa walimu mara nyingine wa kupotosha badala ya wakujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Ghasia kwa kweli tunalichukua na kulizingatia kama Wizara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa hujaridhika bado?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Sijaridhika nilitaka niongeze…

**MWENYEKITI:** Maana hujatoa shilingi, ulitoa shilingi kweli? Haya endelea.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia Kaka yangu akinihakikishia ni mikakati ipi hasa kwa wale ambao wapo kwenye redio na *tv* ambako wananchi wanawasikiliza. Ni jambo la kawaida kumsikia mtu anasema 'Mlima Kirimanjaro, Mwalimu Nyelele' juzi nilikuwa nasikiliza redio mtu anatangaza *Miss UDOM* kama wengine mtafuatilia anasema kwamba kutakuwa na maeneo ambayo watakutana kwenye viwanja vya Mwalimu Nyelele. Sasa unafanyaje pamoja na kamusi na imeandikwa Nyerere lakini mtu anatamka Nyelele. Sasa hilo nadhani ni suala katika ufundishaji, kwa sabau unavyojifundisha lugha ya kiarabu kwenye sarufi kama ni 'r' unafundishwa kabisa kama ni 's' unaambiwa funga meno yaumane ndipo useme 's', kama ni *'earth'* toa ulimi nje.

Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuhakikisha kwamba Walimu wetu wanawafundisha hata namna ya kutamka huko ndiko ambako kuna matatizo makubwa, kuhakikisha kwamba wanaoajiriwa ni wanaoweza kutamka vizuri.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa Mheshimiwa Ghasia kwa mawazo yake mazuri, tuna chombo chetu cha BAKITA ambacho huwa kinatoa semina kwa waandishi wa habari mara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna wakati nilishawahi kujibu swali hapa Bungeni liliulizwa na Mheshimiwa Mukasa kuhusu suala la matamshi linachangiwa pia na lugha zile za asili maeneo ambayo mtu ametoka, kuna wengine ukimuambia atamke 'r' hawezi, lakini yupo mtu ambaye ukimuambia atamke 'l' hawezi, masuala kama hayo kama anavyosema mashuleni walimu wajitahidi kufanya hivyo na sisi Serikali tunashauri kwamba mashuleni wajitahidi

kuwazoeza wanafunzi kutamka kuendana na jinsi kamusi inavyotuonesha. Kwa hiyo, mawazo yake ni mazuri na tunakubaliana nayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala langu ni usikivu wa *TBC*. *TBC* imekuwa ni janga na leo ni ushahidi wazi kwamba haikuwa hewani katika tukio muhimu sana hili la Kitaifa ambalo tumepoteza vijana wetu. Nakusudia kabisa kuondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri kama sitapata majibu yanayoridhisha, ni lini sasa *TBC* itaweza kupatikana hasa kwa maeneo ya pembezoni mwa nchi yetu kama kule Madaba, Kakonko, Lushoto, Pangani na kwingineko. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shangazi ameniletea changamoto nyingine ya nyongeza kwamba leo hatukuwa hewani, nashukuru kwa taarifa hiyo, naomba nimuahidi tu kwamba nitafuatilia suala hili ilitokea kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Shangazi anaelewa kwamba tuna changamoto kubwa ya kuirejesha katika hali yake *TBC* sasa hivi na ndiyo maana tumekuja na hii bajeti tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtupitishie, siyo bajeti ya kuweza kutatua matatizo yote, lakini ni mwazo tu wa kuweza kuangalia tufanye nini tuweze kupata *solution* ya kudumu au jibu la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya mikakati yetu ambayo tumeiwasilisha Serikalini ni kuomba tozo maalum tuweze kuipata kutokana na baadhi ya vifaa vinavyotumika kwenye *tv*, hiyo tozo nina uhakika itatufikisha mbali sana *TBC* ikiwa itapitishwa na vyombo husika na Serikali, tayari tumeshawasilisha Wizara ya Fedha na tuna matumaini makubwa kwamba inaweza kutupeleka mbali sana katika kuirejesha *TBC* katika hali yake hasa kivifaa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

majibu kama haya tuliyapata mwaka jana na tuliambiwa wazi kwamba kuna Halmashauri zaidi ya 81 ambazo *TBC* haisikiki ingekwenda kufikika. Kwa hiyo, sikubaliani kabisa na maelezo ya Waziri na ninaomba kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono tujadili ili tuone sasa suala hili linaisha na *TBC* kama kilivyo chombo cha umma kinapatikana nchi nzima.

Waheshiwa Wabunge, naomba mniunge mkono, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Boni, Mheshimiwa Almas, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Massare, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Susan, Mheshimiwa Jackline, Lugola...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini unaniacha mara kwa mara? Mheshimiwa Haonga umeniacha mara ya kwanza unataka kuniacha tena.

**MWENYEKITI:** Hamuwezi wote mkasema hatuna muda, Mheshimiwa Vulu, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Chumi tayari? Tunaanza na Mheshimiwa Jafo na baadae Mheshimiwa Vulu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimesikia hoja ya Mheshimiwa Shangazi ambayo ni hoja ya msingi sana kwa mustakabali wa usikivu wa maeneo mbalimbali nchini mwetu. Pia ninataka nitumie fursa hii kumshawishi Mheshimiwa Shangazi na Wabunge wote kwamba ni kweli tunaona ni haja ya kuhakikisha jinsi gani tunafanya tuboreshe chombo chetu cha *TBC*, kwa sababu Mheshimiwa Waziri hapo ameshazungumza maelezo kadhaa jinsi gani inafanya chombo hiki kiweze kufanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa sababu ni lazima tujue wazi kwamba Waziri mwenye dhamana ni Waziri ambaye si muda mrefu amepata nafasi hii, hata nikiangalia katika chombo hiki hata Mkurugenzi wake Mkuu ni mpya,

ambaye kipindi cha hivi karibuni katika ufuatialiaji wa aina mbalimbali alikuwa akipita maeneo mbalimbali kubaini changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri Mheshimiwa Shangazi aliridhie *speed* ya Mheshimiwa Waziri anayoenda kuifanya jinsi gani waweke mikakati ya pamoja na kufanya *resource mobilazation* kutafuta fursa mbalimbali kama watu makini, kubadilisha chombo hiki lakini asizuie shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili Mheshimiwa Waziri atekeleze majukumu yake. Ni hilo tu.

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko sambamba na hoja ya Mheshimiwa Shangazi. Sina nia mbaya, nia ni kutaka kujenga na hasa chombo chetu cha Kitaifa cha Utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kauli za watu kwamba Waziri ni mpya katika Wizara hiyo, makabrasha na maandishi yapo, matatizo yanaeleweka, shida zinaeleweka, kwa nini Serikali inashindwa kuweka mkakati kutokana na hoja zinazotolewa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia kila mara hoja hii na mimi nilikuwa naizungumzia, sijaona mabadiliko na wala sijasikia kwamba safari hii labda tumeweka mkakati huu, naiomba Serikali itueleze leo ni nini mkakati ambao umeweka ili chombo kile kiwe imara na kifanye kazi zake kwa umakini, vyombo vyake wafanyakazi na wasikilizaji waweze kuwasikia nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naungana na mtoa hoja hii kwamba chombo

hiki cha *TBC* hasa *TBC* Taifa, imekuwa haisikiki maeneo mengi ya nchi hii, Mheshimiwa Mwenyekiti maeneo ya Mikoa mingi ikiwemo Mkoa wa Singida, tumekuwa tukiuliza maswali majibu yamekuwa mepesi, mkakati wa Wizara hii hauonekani hata katika kitabu chake, katika ukurasa wa 52 *paragraph* ndogo, hakuna nia ya dhabiti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono mtoa hoja Serikali ije na maelezo ya kutosha wananchi wa Tanzania wanapenda kusikiliza redio yao ya Taifa, lakini haisikiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Mollel.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi. *TBC* ni chombo cha wananchi na wananchi wanakatwa kodi kwa ajili ya *TBC*, kama tatizo ni mitambo, ni kwa nini sasa Serikali haioni mkakati wa kutengeneza hii mitambo ili wananchi wa pembezoni wakapata habari na hasa hasa kwenye masuala kama matukio ya Kiserikali bado *TBC* kama *TBC* haionekani, unakuta sana inashughulika na mambo ya kupiga muziki, ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate tamko la Serikali ni kwa nini Tbc haiwajibiki kwa jamii kuonesha habari, kuonesha matukio hata kama kwenye mambo hata leo kulikuwa na maafa, kulikuwa na maziko huko Arusha lakini *TBC* ilikuwa haipo kama tatizo ni mitambo tujue hii mitambo tutafanya marekebisho na kama tatizo ni fedha, kuna fedha ambazo zinalipwa za walipakodi ambacho ni chombo kinaingia kwenye Serikali, hizi pesa zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iweke mikakati mipamgo ya kuhakikisha *TBC* kama *TBC* inakuwa ni chombo cha Taifa na siyo chombo cha binafsi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* ni taasisi na ni Shirika la Serikali, na hili shirika linaendeswa na kodi ya wananchi kwa msingi huo *TBC* ni mali ya wananchi. Inavyoonekana Serikali haitoi kipaumbele kwa ajili ya *TBC*, ukiangalia usikivu wake ni mbaya sana vilevile ukienda kwenye *recording rooms* zao ni za zamani hazifai, ukienda kwenye chumba kile cha kutunzia kumbukumbu zile *cassettes* kwa mfano, *cassette* za Mwalimu Nyerere haziko vizuri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahitaji kwa kweli kutenga pesa ya kutosha kuifanya hii taasisi ya Serikali iwe ya mfano. Kwa nini taasisi ya Serikali isiwe mfano, wanashindwa na taasisi za watu binafsi? Na hii ni chombo cha wananchi? Mheshimiwa Mwenyekiti nataka Serikali iipe kipaumbele *TBC* iwe ni chombo cha mfano kuliko vyombo binafsi. Ahsante.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wameniambia mahitaji ya jumla ya *TBC* kuweza kuirejesha kwenye viwango vya kimataifa ni shilingi bilioni 93. Ningeshukuru sana Waheshimiwa Wabunge wangenieleza jinsi gani niweze kupata hizo pesa, lakini hoja ya nguvu ambayo nimeipata kutoka kwenye Bunge hili kutoka kwenye Kamati inayohusika ni kuanzisha tozo kwa visimbuzi yaani *decoders.* Mkakati ambao unatumika na vyombo vingine vya Serikali kama *BBC*, *VOA, DW (Deutsche Welle)* na tayari Wizara imeshawasilisha maombi hayo kwenye mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba kwa sababu tumewasilisha hayo maombi, hatuwezi tukakaa tu tukisubiri kupata bilioni kadhaa, ndiyo maana tumeanza na shilingi bilioni moja ambayo sasa hivi nilikuwa naongea na Mheshimiwa Naibu Waziri hapa tunarekebisha usikivu wa *TBC* - Kakonko, Rombo, Tarime, Nyasa na Longido kwa shilingi

bilioni moja ambazo tayari tumepata, vilevile tutafanya maendeleo zaidi kwa shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea pole pole kwa bajeti hii tuliyonayo hapa, lakini mkakati wa muda mrefu ni ule ambao tumeuwasilisha Serikalini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri tumekuelewa. Mheshimiwa Shangazi mipango ya Serikali imefanywa na Serikali imetoa *commitment*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeturuka huku watu wawili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi mipango ya Serikali imefanywa na Serikali imetoa *commitment* kwenye Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti wanapeleka pesa na hoja yako ni ya msingi, nakuomba tu mkubalie Waziri sasa ajitahidi kutafuta hela zingine.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hiyo kutoka Halmashauri 81 kwa Halmashauri Saba alizozitaja ina maana itatuchua miaka mingi sana kupata mawasiliano *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nitoe tu masikitiko kwamba hili jambo kila mwaka tunalizungumza hapa kwenye Bunge, hiki ni chombo cha Taifa na kama wameshindwa kuingia kwenye teknolojia ya *digital* waturudishe kule kwenye *analogue* kwa sababu zamani walivyokuwa masafa yale ya *AM, Short Waves* na ya *Medium Waves* walikuwa wanasikika nchi nzima, kama tatizo ni digitali waturudishe kwenye *analoguey. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante namrudishia hiyo shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shangazi. Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *guillotine*

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 - Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kif. 1001 - *Admin. & HR Mgt.*..................Shs. 3,985,517,000/=
Kif. 1002 - *Finance & Accounts*.................Shs. 320,097,000/=
Kif. 1003 - *Policy & Planning*...................Shs. 362,076,000/=
Kif. 1004 - *Gvt. Comm. Unit*.......................Shs. 88,563,000/=
Kif. 1005 - *Procurement Mgt. Unit*..............Shs.131,939,000/=
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit*....................Shs. 106,743,000/=
Kif. 1007 - *Info. & Comm. Tech. Unit*..........Shs. 169,907,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit*.....................Shs. 73,630,000/=
Kif. 6001 - *Culture Dev. Division*..............Shs. 3,539,788,000/=
Kif. 6002 - *Youth Dev. Div.*.........................Shs. 414,000,000/=
Kif. 6004 - *Sports Development*...............Shs. 1,399,399,000/=
Kif. 7003 - *Info. Services*.........................Shs. 11,301,036,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 - Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kif. 6001 - *Culture Dev. Division*..............Shs. 1,500,000,000/=
Kif. 6004 - *Sports Dev.*...............................Shs. 1,820,000,000/=
Kif. 7003 - *Information Services*...............Shs. 3,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limepitia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, fungu kwa fungu na kuipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2017/2018 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda na bajeti imepita. Mheshimiwa Waziri hongera sana, niwapongeze Wabunge wote kwa kazi nzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna tangazo dogo hapa, Waheshimiwa Wabunge Wakristo wote wanatangaziwa kwamba kesho tarehe 9 Mei, saa 7 mchana, kutakuwa na Ibada kayika eneo la wazi la *basement.* Aidha katika Ibada hiyo kutakuwa na Mtumishi wa Mungu, Mtume na Nabii Josephat Mwingira ambaye atahudhuria katika Ibada hiyo, ikiwemo na kwaya ya Efatha. Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa.

Sasa ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne Tarehe 9 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*